1 SEPTEMBA, 2026

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Tano – Tarehe 1 Septemba, 2026

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Daniel B. Sillo) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae.

Katibu.

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa Mwaka 2026 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2026]*.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita, kama ifuatavyo:-

1. Toleo Na. 13 la tarehe 27 Machi, 2026;
2. Toleo Na. 14 la tarehe 03 Aprili, 2026;
3. Toleo Na. 15 la tarehe 10 Aprili, 2026;
4. Toleo Na. 16 la tarehe 17 Aprili, 2026;
5. Toleo Na. 17 la tarehe 24 Aprili, 2026;
6. Toleo Na. 18 la tarehe 01 Mei, 2026;
7. Toleo Na. 19 la tarehe 08 Mei, 2026;
8. Toleo Na. 20 la tarehe 15 Mei, 2026;
9. Toleo Na. 21 la tarehe 22 Mei, 2026;
10. Toleo Na. 22 la tarehe 29 Mei, 2026;
11. Toleo Na. 23 la tarehe 05 Juni, 2026;
12. Toleo Na. 24 la tarehe 12 Juni, 2026;
13. Toleo Na. 25 la tarehe 19 Juni, 2026;
14. Toleo Na. 26 la tarehe 26 Juni, 2026;
15. Toleo Na. 27 la tarehe 03 Julai, 2026;
16. Toleo Na. 28 la tarehe 10 Julai, 2026;
17. Toleo Na. 29 la tarehe 17 Julai, 2026;
18. Toleo Na. 30 la tarehe 24 Julai, 2026;
19. Toleo Na. 31 la tarehe 31 Julai, 2026;
20. Toleo Na. 32 la tarehe 07 Agosti, 2026;
21. Toleo Na. 33 la tarehe 14 Agosti, 2026;
22. Toleo Na. 34 la tarehe 21 Agosti, 2026;

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa Mwaka 2026 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2026]*.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Chikambo, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati.

Katibu.

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI).

Mheshimiwa Kakulu Buchard Kakulu, Mbunge wa Mbagala, sasa aulize swali lake.

Na. 56

Ujenzi wa Shule ya Msingi Mtaa wa Barabara ya Mwinyi Kata ya Kiburugwa

MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y. MHE. KAKULU B. KAKULU aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa shule ya msingi mitaa ya Barabara ya Mwinyi, Kata ya Kiburugwa – Mbagala?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Kakulu Buchard Kakulu, Mbunge wa Jimbo la Mbagala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mitaa ya Barabara ya Mwinyi katika Kata ya Kiburugwa – Mbagala katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke haina shule ya msingi, hali inayowalazimu wanafunzi takribani 1,500 kutembea umbali wa kati ya kilomita mbili hadi nne kwenda shule za msingi zilizopo katika maeneo mengine ya Jiji la Dar es Salaam. Ili kutatua changamoto hiyo, katika mwaka wa fedha

2025/2026 Halmashauri ya Manispaa ya Temeke imelipa fidia ya shilingi millioni 306.89, kwa ajili ya kutwaa eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 3,758 litakalotumika kujenga shule mpya ya msingi katika Mitaa ya Barabara ya Mwinyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa shule hiyo utagharimu shilingi bilioni 3.49 na utakua na miundombinu ya madarasa 27, ofisi 15, stoo moja, maktaba moja, chumba cha TEHAMA kimoja na matundu ya vyoo 84, ambapo katika mwaka wa fedha 2026/2027 shilingi bilioni moja zimetengwa, kwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa awamu ya kwanza. Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushuru sana. Naanza kwa kuipongeza Serikali na kushukuru kwa kuona umuhimu huo wa kujenga shule ya msingi katika eneo la Barabara ya Mwinyi katika Kata ya Kiburugwa. Pamoja na hayo, ninalo swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, changamoto kama hiyo ameipata katika Kata ya Kiburugwa, bado kuna changamoto katika Eneo la Goroka na Kata ya Tuangoma, Jimbo la Mbagala. Eneo hilo ni kubwa na halina kabisa shule ya msingi. Je, Serikali haioni haja sasa ya kuwaangalia Wananchi wa Goroka nao waweze kupata shule ya msingi, kama walivyopata Wananchi wa Kiburugwa?

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza naanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa, mama yangu, Mariam Kisangi, Mbunge wa Jimbo la Temeke, kwa namna ambavyo anafanya kazi kwa dhati kabisa kuwakilisha Wananchi wa Temeke. Namhakikishia tu kwamba, Serikali hii ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt.

Samia Suluhu Hassan, imeendelea kutenga fedha, kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya sekta ya elimu; elimu msingi na sekondari, ili kuhakikisha kwamba, wanafunzi wetu wanapata elimu bora katika mazingira bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi; katika Shule hii ya Msingi ya Barabara ya Mwinyi katika Jimbo la Mbagala, tayari tumetenga shilingi bilioni 100 katika mwaka huu wa fedha. Tutaendelea kutenga fedha katika kila mwaka wa fedha kuhakikisha kwamba, tunajenga shule hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shule ya Msingi ya Goroka katika Kata ya Tuangoma; namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, mpango huu wa Serikali ni endelevu. Tumeendelea kutenga fedha kwa awamu na tumetambua maeneo yote, ambayo yana wanafunzi wengi na wanahitaji shule mpya. Tutaendelea kupeleka fedha kwa kutenga kwenye bajeti zetu, ili kuhakikisha kwamba, shule zinajengwa katika maeneo hayo na kuondoa umbali kwa wanafunzi, ikiwemo katika Eneo la Goroka, Kata ya Tuangoma.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Faraji Nandala, swali la nyongeza.

MHE. FARAJI B. NANDALA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Tatizo la wanafunzi kuacha shule kutokana na utoro, hasa unaosababishwa na kusafiri umbali mrefu kufuata elimu kwenye Jimbo la Ndanda, umekuwa ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kwenye Kijiji cha Namarembo, mwaka uliopita wanafunzi 50 walidahiliwa waweze kujiunga na kidato cha kwanza na mpaka kufika mwezi uliopita, wanafunzi 15 pekee ndio waliobaki. Hii ni kutokana na umbali uliopo kutoka Namarembo kwenda Makao Makuu ya Kata ya Msikisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu kwa Serikali, ni upi mpango mahususi wa kuanza kujenga shule za sekondari, hasa

kwenye vijiji ambavyo vinapatikana mbali kutoka makao makuu ya kata?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, swali la msingi ni ujenzi wa shule ya msingi kwa hiyo, tunaendelea.

Mheshimiwa Anna Lupembe, swali la nyongeza.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi. Kata ya Nsimbo, kwenye Halmashauri ya Nsimbo, Kijiji cha Mwenge, wananchi wameanza kujenga shule ya msingi na Mbunge naye ametoa kwenye Mfuko wa Jimbo. Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi huo, ili watoto wasitembee umbali mrefu? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nampongeza sana Mheshimiwa Anna Lupembe, Mbunge wa Jimbo la Nsimbo, kwa namna ambavyo mara kwa mara amekuwa anafuatilia ustawi wa sekta ya elimu katika Jimbo la Nsimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia nafasi hii kupongeza Menejimenti ya Halmashauri ya Nsimbo, Wananchi wa Kata ya Nsimbo, pamoja na Mheshimiwa Mbunge, kwanza kwa kutambua eneo, kwa ajii ya ujenzi wa shule mpya ya msingi. Pili, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kutoa Fedha ya Mfuko wa Jimbo, ili kuchangia nguvu za wananchi katika ujenzi wa shule hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Nsimbo kwamba, Serikali imeweka mkakati na katika kipindi cha Aprili mpaka Agosti mwaka huu 2026, Serikali tayari imepeleka fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, jumla ya shilingi bilioni 188.3, kwa ajili ya ujenzi wa shule za msingi na sekondari. Kati ya hizo, tumejenga shule mpya 189; shule za msingi 28 na za sekondari 161.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Nsimbo kwamba, Serikali tutaendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya Shule ya Msingi ya Nsimbo kulingana na vigezo vya mahitaji ya wanafunzi. Tutapeleka fedha kwa awamu, kwa ajili ya ujenzi na kuhakikisha kwamba, tunapunguza umbali wa wanafunzi kwenda shule katika eneo hilo.

NAIBU SPIKA: Asante. Waheshimiwa tunaenda swali linalofuata.

Mheshimiwa Jackson Gideon Kiswaga, Mbunge wa Kalenga, sasa aulize swali lake.

Na. 57

Kukamilisha Ukarabati wa Shule Kongwe ya Sekondari Tosamaganga

MHE. JACKSON G. KISWAGA aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha, ili kukamilisha ukarabati wa Shule Kongwe ya Sekondari Tosamaganga ambao ulishaanza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Gideon Kiswaga, Mbunge wa Jimbo la Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea na zoezi la kukarabati shule zote kongwe nchini. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016 hadi 2022/2023 Serikali imetumia shilingi bilioni 97.92, kwa ajili ya ukarabati wa shule kongwe za sekondari 89 nchini, ikiwemo Shule ya Sekondari ya Tosamaganga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho Shule ya Sekondari Tosamaganga imepelekewa shilingi milioni 867, kwa ajili ya ukarabati wa vyumba vya madarasa 20, ofisi za walimu tatu, karakana moja, majengo ya utawala mawili, mabweni mawili, maktaba, kumbi mbili, jiko, stoo ya chakula na matundu ya vyoo sita. Miundombinu ya Shule ya Sekondari Tosamaganga, ambayo haijafanyiwa ukarabati, ni mabweni sita, vyumba vya madarasa viwili na nyumba za walimu 28, ambapo Serikali itaendelea kutenga fedha za ukarabati wa miundombinu hiyo, pamoja na shule nyingine zote kongwe kote nchini.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Asante sana. Kwanza ninashukuru sana juhudi za Serikali za kuleta fedha katika Jimbo la Kalenga, hasa Shule ya Tosamaganga, kufanya ukarabati ambao umefanyika. Kwa kuwa, shule hii itatimiza miaka 100 mwezi wa kumi na tutafanya sherehe kubwa, ambapo Mgeni Rasmi atakuwa Prof. Kabudi, mwanafunzi mojawapo aliyesoma Tosamaganga. Tunatamani basi, tupewe fedha tunaposherehekea miaka 100 tukamilishe sehemu iliyobaki. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kutuletea fedha, ili tukamilishe hapo palipobaki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Zipo shule nyingine kongwe za msingi, ikiwepo Shule ya Nyamihuli, Shule ya Ibumila na Shule ya Ifunda ambazo ni chakavu sana, zimejengwa miaka ya 1960/1970. Je, kwa kuwa, halmashauri yetu uwezo wake ni mdogo, Serikali haioni haja sasa ya kutuletea fedha kidogo kidogo, hata katika shule tano kwa mwaka, ili tupunguze ukarabati katika shule hizo ambazo ni kongwe sana?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Jackson Kiswaga, Mbunge wa Jimbo la Kalenga, kwa namna

ambavyo anachapa kazi kuwasemea Wananchi wa Jimbo la Kalenga na kwa namna ambavyo anafuatilia ustawi wa Shule ya Sekondari ya Tosamaganga. Shule yenye usajili namba moja hapa nchini na shule kongwe, ambayo inakwenda kutimiza miaka 100 ifikapo tarehe 10 Oktoba, 2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ku-*declare interest* kwamba, mimi ni miongoni mwa wanafunzi ambao tumesoma Shule ya Sekondari ya Tosamaganga. Natumia nafasi hii, kumpongeza sana Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Mheshimiwa Kheri James, pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mheshimiwa Benjamin Sitta, pamoja na Mkuu wa Sekondari ya Tosamaganga na menajimenti nzima; kwanza kwa kuweka wazo bora la kuhusisha wadau mbalimbali na wanafunzi, *alumni* wa Tosamaganga, waliosoma pale. Nina uhakika katika ukumbi huu wapo wadau na *alumni* waliosoma Tosamaganga tukiongozwa na Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao viongozi katika taasisi mbalimbali na tunao viongozi katika taasisi binafsi. Natumia nafasi hii kuwaomba na kutoa wito kwamba, wadau wote twendeni kuanzia tarehe 8, 9 na 10 Oktoba, tukajumuike na Jumuiya ya Tosamaganga katika *jubilee* ya miaka 100. Lengo la *jubilee* hiyo ni kuchangiza shilingi bilioni moja, kwa ajili ya ununuzi wa basi la Shule ya Sekondari ya Tosamaganga na pia, kuchangia nguvu za Serikali katika ukarabati wa baadhi ya miundombinu ya shule hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Serikali inaona umuhimu wa kupeleka fedha mapema, ili angalau tuendelee kukarabati miundombinu iliyobaki. Pia, Serikali inaendelea kuhamasisha wadau kuiga mfano wa mpango wa Tosamaganga Sekondari katika kuchangia nguvu katika ukarabati wa shule hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, kuhusiana na shule za msingi chakavu. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba,

tutaendelea kupeleka fedha. Tunatambua ziko shule chakavu na katika kipindi hiki cha miezi mitatu, tayari shule chakavu 75 zimepelekewa fedha na ukarabati unaendelea. Zoezi hili ni endelevu, tutahakikisha shule za Jimbo la Kalenga pia, zinapewa kipaumbele. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Yagi Kiaratu, swali la nyongeza.

MHE. YAGI M. KIARATU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi. Shule ya Sekondari Mwenge, iliyoko Manispaa ya Singida, pia, ni moja ya shule kongwe, ambayo ukarabati umeanza, lakini bado haujakamilika. Sasa ni lini Serikali italeta fedha, ili kukamilisha ukarabati huo? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, Serikali imepeleka fedha, kwa ajili ya ukarabati wa shule hiyo na tunafahamu kwamba, fedha zile hazitakamilisha ukarabati kwa kadiri ya mahitaji. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunakwenda kwa awamu. Tumekwenda awamu ya kwanza ya ukarabati, lakini Serikali itaendelea kutenga fedha, kwa ajili ya kukamilisha ukarabati kwa sehemu iliyobaki.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi nami niulize swali dogo la nyongeza. Ni kweli kabisa, tumepiga hatua sana katika kujenga shule za *primary* na sekondari na Katika hii Awamu ya Sita, zimejengwa shule nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utafiti ambao umefanywa, kwa *primary* peke yake, zinahitajika shilingi trilioni 3.8, ili kukarabati miundombinu, ambayo haiko kwenye hali nzuri, ni chakavu na kwa sekondari pia, zinahitajika fedha nyingi. Nini mkakati wa Serikali

kuhakikisha tuna fungu maalum, kwa ajili ya ukarabati kwenye miundombinu chakavu, ili hata hii tunayoijenga iweze kubaki kwenye ubora wake? Nini mkakati wa Serikali? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nampongeza sana Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Jimbo la Bunda, kwa kazi nzuri na kubwa anayoifanya. Ni kweli, kama alivyosema vizuri Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunazo shule nyingi chakavu, za msingi na sekondari. Serikali imeendelea kutenga fedha kila mwaka wa fedha kuhakikisha kwamba, shule zinaendelea kukarabatiwa. Kama ambavyo nimesema, jumla ya shilingi bilioni 188 katika kipindi cha miezi hii mitatu zimepelekwa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kwa ajili ya kukarabati shule za msingi na sekondari, chakavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza zoezi hili ni endelevu, tutaendelea kutenga fedha kwenye bajeti, lakini mpango wa Serikali ni tayari tumefanya tathmini ya shule zote kongwe na chakavu za msingi kote nchini. Tumeweza kufanya *estimate* ya gharama zinazohitajika, kwa ajili ya ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, tumewasilisha Tume ya Mipango, Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, ili tuweze kuratibu na kuja na njia nzuri na mwafaka ya kukarabati shule hizo na pia, kuwa na njia endelevu ya kuwa na mpango wa kukarabati shule zetu zinazojengwa, ili zisifike hatua ya kuwa chakavu sana badala ya kuzikarabati mara kwa mara. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali hii itaendelea kutenga fedha na kutathmini mipango madhubuti, kwa ajili ya kukarabati shule zote chakavu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cornel Magembe, swali la nyongeza.

MHE. CORNEL L. MAGEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa Naibu Waziri. Ziko shule nyingi ambazo kwa kweli, zimechakaa katika maeneo mengi, ikiwemo Shule ya Sekondari Kachwamba na Shule ya Sekondari Nyamirembe. Nini kauli ya Serikali juu ya kupeleka fedha kwenda kukarabati shule hizo, ili zirudi kwenye ubora wake, kama zilivyokuwa hapo awali? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba, kweli shule za Jimbo la Chato Kaskazini, kwa Mheshimiwa Magembe, zimechakaa. Mheshimiwa Mbunge amewasilisha kwa maandishi na amefika Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, kuzisemea shule hizo. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwanza tumezitambua na tumeziingiza kwenye orodha ya shule chakavu ambazo zinahitaji ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kauli ya Serikali ni kwamba, tunaendelea na taratibu za kibajeti. Kama nilivyosema, tuko na taratibu, kupitia Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha, ili tuweze kuwa na mpango wa uhakika wa kupeleka fedha katika shule chakavu zote nchini, zikiwemo shule hizo, ili tuweze kuzikarabati. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Getere, swali la nyongeza.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Katika Shule ya Sekondari ya Sanzati, shule ile imejengwa, ina madarasa nane tu, haina kitu chochote kilichopo hapo. Imejengwa na wananchi wakasaidiwa na Serikali kidogo na taarifa zake zimekuja TAMISEMI kwa muda mrefu. Sasa, ni lini Serikali itatoa hela za kutosha kujenga ile shule ikamilike, ili ifanane na shule nyingine? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Getere, Mbunge wa Jimbo la Bunda kwamba, Serikali inatambua Shule ya Sekondari ya Sanzati imepelekewa fedha na baadhi ya miundombinu imejengwa imekamilika, lakini tunatambua kwamba, kuna upungufu wa baadhi ya miundombinu. Nakuhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, safari ni hatua, tunakwenda kwa awamu, na katika bajeti zetu tutatoa kipaumbele katika shule hiyo, ili tuweze kukamilisha miundombinu yote inayotakiwa, shule hiyo iendelee kutoa huduma kwa wanafunzi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Faraji Nandala, swali la nyongeza.

MHE. FARAJI B. NANDALA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Ni lini Serikali itapeleka fedha kwenye shule zinazopokea wanafunzi wenye mahitaji maalumu, kama vile Chidya *Secondary*, hali ya kuwa pale mwaka uliopita wamepokea wanafunzi 185, lakini mazingira ya pale siyo rafiki, kwa ajili ya wale wanafunzi wenye ulemavu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka mpango ambao unaendelea na utekelezaji wa kutambua na kuziweka katika kundi maalumu shule zote zenye wanafunzi wenye mahitaji maalumu, kwa ajili ya kujenga miundombinu wezeshi, kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi hao kusoma na kuishi, katika shule hizo, katika mazingira bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, shule hiyo aliyoitaja, ambayo ina wanafunzi wenye mahitaji maalumu tutaipa kipaumbele katika bajeti zetu, ili kuboresha miundombinu hiyo na kuwawezesha watoto wetu kusoma katika mazingira bora zaidi.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na swali linalofuata.

Swali la Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini. Litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Dkt. Lazaro Komba, Mbunge wa Peramiho.

Na. 58

Kukamilisha Ujenzi wa Kituo cha Afya Myangayanga, Mbinga

MHE. DKT. LAZARO K. KOMBA K.n.y. MHE. JONAS W. MBUNDA aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya cha Myangayanga, Kata ya Myangayanga, katika Jimbo la Mbinga Mjini?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, Afya. Mheshimiwa Dkt. Jafar, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Jimbo la Mbinga, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imetoa jumla ya shilingi milioni 250, kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Myangayanga. Aidha, kiasi hiki cha fedha kimejenga jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje *(OPD),* pamoja na jengo la maabara. Kituo cha Afya cha Myangayanga ni miongoni mwa vituo 364 ambavyo vina upungufu wa miundombinu muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali imetenga bajeti ya jumla ya shilingi bilioni 23.37, kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu kwenye vituo vya afya 111, kikiwemo Kituo cha Afya Myangayanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa awamu, kwa ajili ya kukamilisha miundombinu muhimu, ikiwemo jengo la upasuaji, wodi na jengo la kufulia katika vituo vya afya 364, ili viweze kutoa huduma bora za afya. Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Lazaro Komba, swali la nyongeza.

MHE. DKT. LAZARO K. KOMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru na ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina nyongeza ya maswali mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ni kwamba, Serikali ilikuwa na mpango wa ujenzi wa Kituo cha Afya Utiri. Sasa, je, ni lini mpango huu wa ujenzi wa kituo hiki cha afya utaanza kutekelezwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kwamba, wananchi wa Jimbo hili la Mbinga Mjini wanaishukuru sana Serikali kwa kuwajengea Kituo cha Afya Mbangamao, lakini bado baadhi ya majengo katika kituo hiki cha afya hayajakamilika, ikiwemo wodi kwa ajili ya wagonjwa na kichomea taka. Ni lini sasa Serikali itapeleka fedha, kwa ajili ya kukamilisha miundombinu katika Kituo hiki cha Afya cha Mbangamao? Ninakushukuru sana kwa nafasi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Najibu maswali madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, chini ya Mheshimiwa Prof. Riziki Shemdoe, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge tunaendelea kuangalia vipaumbele vya vituo hivi vya afya kwa kuangalia tathmini na kukidhi vigezo. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wanajimbo la Mbinga, tutaendelea kutenga bajeti kuhakikisha kwamba, tunajenga vituo hivi kulingana na uhitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Ninapokea pongezi kwa niaba ya Serikali, lakini tunaendelea kutenga fedha na kuhakikisha kwamba, tunaongeza majengo katika vile vituo 111 na hiki cha Mbangamao, yale ya wodi, jengo la kufulia na kichomea taka. Tutaendelea kutenga bajeti na kuhakikisha kwamba, wananchi wa Jimbo la Mbinga Mjini wanaendelea kunufaika na matunda ya Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tutampa ushirikiano wa dhati na kumuweka katika vipaumbele kuhakikisha kwamba, kwenye vile vituo vya afya 111 na hiki cha Mbangamao na chenyewe kinatengewa fedha na kukamilisha miundombinu hii. Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali ya nyongeza yawe mafupi.

Mheshimiwa Zacharia Paulo, swali la nyongeza.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Ninaishukuru Serikali kwa kujenga kituo cha afya katika Kata ya Murray, Halmashauri ya Mji wa Mbulu. Kwa kuwa, kituo cha Afya Murray kiko tayari sasa, nini mpango wa Serikali kupeleka vifaatiba na vifaa tendanishi katika vituo vyote vya afya nchi nzima, ikiwemo Kata ya Murray, Halmashauri ya Mji wa Mbulu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zacharia Paulo, Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tumetenga fedha kwa awamu kuhakikisha kwamba, tunaanza kujenga miundombinu katika vituo hivi vya afya na baada ya hapo nimewasiliana na wenzetu wa Wizara ya Afya kuendelea kupeleka vifaatiba katika vituo vyetu vya afya. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge pamoja na wana-jimbo, tutaendelea kupeleka vifaatiba katika vituo hivi, ili vitoe huduma kwa wagonjwa wetu. Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaishukuru Serikali kwa kupatia Wilaya ya Kilolo, Kituo cha Afya cha Ruaha Mbuyuni, *ambulance*, Mungu akubariki sana. Je, lini sasa Serikali itajenga vituo vya afya katika Kata ya Ilole, Ibumu, Image na Ukwega kwa sababu, wananchi wa Kilolo wamekuwa wanapata shida sana kwenda kufuata matibabu katika vituo vya afya, ambavyo viko mbali kutokana na changamoto iliyopo katika Wilaya ya Kilolo kwamba, imetawanyika sana? Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkr. Ritta Kabati, kama alivyoliuliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapokea pongezi za Mheshimiwa Dkt. Rita Kabati, Mbunge muungwana kabisa, mama yangu, kwa shukrani za *ambulance,* ambayo imekwenda kutoa huduma. *Ambulance* hizi ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan

Mwenyewe, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameelekeza kwenye maeneo yenye vipaumbele, yenye uhitaji mkubwa, kuhakikisha zinatoa huduma kwa mama zetu, hasa wale wajawazito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na swali ambalo Mheshimiwa Dkt. Kabati ameuliza, Serikali tunaendelea kutenga bajeti kwa awamu kuhakikisha kwamba, tunajenga vituo hivi. Tunaitisha taarifa kuona tathmini na vigezo, ambavyo vituo hivi vya afya kwenye kata zetu vimefikia, ili tutenge bajeti na kuhakikisha tunaanza ujenzi mara moja. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Thomas Maganga, swali la nyongeza.

MHE. THOMAS K. MAGANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Hospitali ya Wilaya ya Mlele imejengwa kwa kiwango kikubwa sana, lakini swali hili nimeliuliza leo ni mara ya sita. Kipindi hiki wakati mvua zinanyesha, namna ya kuhamisha wagonjwa kuwatoa wodi moja kuwapeleka kwenye majengo mengine imekuwa ni kazi sana. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali, ni lini watapeleka fedha, kwa ajili ya kuweka njia, zile *walkways,* ili kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Katavi? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Thomas Maganga, Balozi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge. Hata katika kipindi cha Bunge lile la bajeti tumekaanaye hapa Bungeni na pia, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, chini ya Mheshimiwa Profesa Riziki Shemdoe. Tumemwahidi Mheshimiwa Mbunge tutaangalia katika bajeti na kuhakikisha kwamba, tunaanza kukamilisha miundombinu ya ujenzi katika hospitali yetu ile

ya wilaya, ili wananchi waweze kupata huduma, hasa kujenga zile *walkways* na miundombinu mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Maganga kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, itaendelea kumpa ushirikianao na kuhakikisha kwamba, tunatenga bajeti ya kukamilisha zile *walkways* na miundombinu mingine. Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru sana Serikali kwa kutujengea kituo cha afya Kata ya Mbasa, Tarafa ya Ifakara. Kwa kuwa, Serikali inaendelea kukijengea uwezo kituo hicho cha afya Kata ya Mbasa, bado wananchi wengi wa kata tisa wanaendelea kupata huduma za matibabu katika kituo cha afya cha Kibaoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge lililopita tumeiomba Serikali itujengee jengo la *OPD* katika Kituo cha Afya cha Kibaoni na Serikali ilikubali ombi hilo. Je, ni lini Serikali itatekeleza maelekezo yake ya ujenzi wa *OPD* katika Kituo cha Afya cha Kibaoni?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asenga, pamoja na shukrani ambazo amezitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli na dhahiri kwamba, Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imejizatiti kuhakikisha kwamba, inajenga vituo hivi vya afya, inakamilisha zahanati na hospitali za wilaya na kuhakikisha zinatoa huduma inayotarajiwa kwa wananchi wetu. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge Asenga kwamba, katika vile vitio vya afya 111

tutakamilisha kwa awamu hii ya kwanza ya mwaka 2026/2027 na kituo cha afya ambacho amekitaja, tunakipa kipaumbele kuonesha kwamba, tunakitengea bajeti, shilingi bilioni 23.37, kuhakikisha tunakwenda kujenga hiyo wodi na kukamilisha miundombinu inayotakiwa pale. Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, sasa aulize swali lake.

Na. 59

Taaluma ya Udereva Kuwa na Staha, Hadhi na Heshima

MHE. RASHID A. SHANGAZI aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha taaluma na kazi ya udereva ina kuwa na staha, hadhi na heshima, sawa na kada nyingine?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Mheshimiwa Regina Ndege, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha taaluma na kazi ya udereva inakuwa na staha, hadhi na heshima, sawa na kada nyingine, Serikali pamoja na mambo mengine imeendelea kuboresha muundo wa maendeleo ya utumishi wa kada hiyo,

kuboresha mafunzo ya kitaaluma na viwango vya elimu, kuimarisha motisha na maslahi ya kada ya udereva, ili kukidhi na kumudu mazingira ya utendaji kazi, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, swali la nyongeza.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Shirika la Kazi Duniani *(ILO)*, ambalo Tanzania kama nchi tumeridhia maazimio mbalimbali, ikiwemo mikataba ya hali na mahusiano bora kazini, kwa kupitia Sheria ya Taasisi za Kazi Namba 07 ya Mwaka 2024, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Namba 06 ya Mwaka 2006. Sasa ninataka kujua, ni kwa kiwango gani Serikali imekuwa ikisimamia kada hii ya udereva, hasa katika maeneo ya mikataba ya kazi, mishahara, hifadhi ya jamii, usalama kazini na likizo, ili tuweze kuona kazi hii ya udereva ina staha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa, eneo hili la udereva limejaa dhuluma na unyanyasaji mkubwa na tumeona mara kadhaa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inaenda katika maeneo mbalimbali, kwa mfano migodini, kwenye maziwa na maeneo ambayo yanakiuka misingi na haki za binadamu. Je, Serikali iko tayari kushirikiana na Tume hii ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwenda kuona na kuichunguza kwa kina sekta ya udereva hapa nchini, ili wafanyakazi katika sekta hii waweze kupata haki stahiki? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali haya ya nyongeza.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza natumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge

Rashid Shangazi kwa namna ambavyo ameendelea kuwatetea au kusemea kada hii muhimu ya udereva.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kuona umuhimu wa kada hii ya udereva imeendelea kutoa miongozo na kusisitiza usimamizi mzuri wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366, ambayo inatamka wazi kwamba, wafanyakazi wanapokwenda kuajiriwa kwenye mambo ya udereva wapewe elimu na taarifa sahihi ya kazi yenyewe wanayoenda kuifanya, ikiwepo muda wa kazi na stahiki zao za kazi. Pamoja na hayo, Serikali inaeendelea kusisitiza kwamba, wamiliki wote wa magari pamoja na *private sector* wahakikishe wanatoa mikataba ya ajira pale ambapo wanaajiri madereva.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo ni, ili waweze kupata stahiki zao na kuelewa kwamba, kazi wanayoenda kuifanya inazingatia hali halisi ya kazi hiyo. Kuzingatia staha na pia, inakuwa ni kazi ambayo wanaifanya wakiamini kwamba, wanapata stahiki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Kazi, Mahusiano na Ajira, Serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu kuhakikisha kwamba, watu wote wanaoajiriwa kwenye hizi *private sector* wanafuatiliwa kwa karibu. Miongozo iendelee kutolewa na pia, kusimamia mikataba itolewe kwa wakati, ili wale madereva wapate stahiki zao. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Husna Sekiboko, swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mbunge, subiri. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Uwekezaji amesimama!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana. Ninasimama kwa nafasi yangu hiyo, lakini pia, kama Kaimu *Chief Whip,* kupongeza kwa niaba ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu mambo mawili matatu. La kwanza, ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake makini sana kwa swali la Mheshimiwa Rashid Shangazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili. Niseme kwamba, sekta ya usafiri na usafirishaji ni muhimu sana katika uchumi wa Tanzania. Ni moja ya sekta tano ambazo zinachangia pakubwa katika uchumi wetu, asilimia 8.5, kwa hiyo, ni sekta ambayo hatuwezi kuiweka pembeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, madereva ndiyo ambao wanaishikilia sekta ya usafiri na usafirishaji. Katika ajira ambazo tunazo, asilimia 4.4 zipo katika sekta ya usafiri na usafirishaji na zote zinashikiliwa na madereva. Tunazungumzia madereva takribani milioni 1.1 mpaka milioni 1.3 kwa hiyo, ni kubwa. Kwa sababu hiyo, katika mpango wetu wa maendeleo ambao tumeuwasilisha hapa, wa miaka mitano, unalenga, dhima yake kubwa ni kutengeneza ajira zenye staha. Kwa hiyo, tunaambia madereva kwamba, nyie ni sekta muhimu, Serikali itaendelea kuweka jicho lake hapo na tuchukue ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuchukue ushauri wa Mheshimiwa Rashid Shangazi kwamba, kama kuna dhuluma na uonevu, kama ambavyo Mheshimiwa Shangazi amesema, basi Tume yetu ya Haki za Binadamu na Utawala Bora itaangalia jambo hili kuhakikisha kwamba, sekta hii ya usafiri inasimama na madereva wanaendelea kuheshimiwa katika nchi yetu. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, Prof. Kitila Mkumbo. Mheshimiwa Husna Sekiboko, swali la nyongeza.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana, lakini *Chief Whip,* Mheshimiwa Prof. Mkumbo amejibu swali ambalo nilitaka kuuliza. Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Tunaendelea. Mheshimiwa Dkt. Emanuel Qambaji Nuwas, Mbunge wa Mbulu Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 60

Kada ya Afya Ngazi ya Ubobezi Kutambulika Kwenye Muundo wa Utumishi wa Umma

MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutambua kwenye Muundo wa Utumishi wa Umma, Wataalamu wa Kada ya Afya wenye elimu ngazi ya ubobezi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ninaomba kujibu swali ya Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miundo ya maendeleo ya utumishi huandaliwa kwa kuzingatia mahitaji ya kiutumishi, majukumu ya kada, pamoja na viwango vya elimu na sifa za kitaaluma vinavyotolewa na taasisi za elimu zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yetu inayosimamia utumishi, imepokea mapendekezo ya Muundo wa Utumishi kwa Wataalamu wa Kada ya Afya wenye Elimu ya ngazi ya ubobezi na taratibu, kwa ajili ya uchambuzi wa kina na kupata idhini zinazoendelea, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas, swali la nyongeza.

MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza; hakika ninatambua mchango mkubwa ambao umewekwa na Serikali ya Awamu ya Sita katika kuwaendeleza watumishi hawa na kuwaajiri katika hospitali zetu za Taifa, kanda, mikoa na pia, wengine katika ngazi ya halmashauri. Je, Serikali haioni haja ya kuelekeza hospitali na taasisi zilizoajiri hawa watumishi kwa kutumia mapato ya ndani kuwalipa posho mbalimbali za kutambua juhudi zao wanazoziweka katika kuwahudumia Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili. Katika hospitali zetu za halmashauri na vituo vya afya, Serikali imewekeza vifaa mbalimbali kama *X-ray, Ultrasound,* vifaa vya dawa za usingizi na ganzi. Je, ni nini mpango wa Serikali kuajiri watumishi ambao ni wataalamu wa mionzi na wa dawa za usingizi na ganzi, ili kupeleka huduma za upasuaji karibu na wananchi katika halmashauri zetu na vituo vya afya?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuhakikisha kwamba, watumishi ambao wanafanya kazi katika kada hiyo ya afya wanaendelea kuzingatiwa na kupata stahiki zao, ikiwemo motisha mbalimbali. Serikali, kupitia Ofisi yetu ya Utumishi, imeendelea kutoa miongozo mbalimbali katika kuhakikisha kwamba, kada hii ya afya watumishi ambao wanafanya kazi katika muda wa ziada wanapata ile *on call allowance*. Pia, imeelekezwa, watumishi ambao wapo katika kada hii ya afya kupata posho ya sare *(uniform allowance)* na pia, posho ya uchunguzi wa maiti *(postmortem allowance)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo yote yamefanyika na maelekezo yametolewa. Pia, ruzuku mbalimbali ambazo zinatoka Serikalini, pamoja na fedha za ndani zimeendelea kutumika kuhakikisha kwamba, watumishi katika kada hii ya afya wanapata stahiki zao, ikiwa ni sehemu ya motisha ya kuendelea kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili. Kama unavyofahamu, Serikali yetu, chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kipindi hiki imejenga vituo vingi vya afya na kuboresha hospitali zetu za wilaya kwa kiwango kikubwa na pia, imepeleka vifaatiba vikiwemo vifaa vya kupima, kama *X-ray* na *Ultrasound*. Pamoja na hayo, Serikali imeona umuhimu wa kupeleka wataalamu katika maeneo hayo, ili wakafanye kazi hiyo kwa kutumia vifaa ambavyo vimepelekwa katika vituo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuona hivyo, Serikali imetenga katika bajeti yake kuajiri watumishi 10,009 katika kada zote za afya na kuhakikisha kwamba, tunapata wataalamu *(technologist)* takribani zaidi ya 200 watakaopangwa katika vituo vyetu vya afya pamoja hospitali zetu za wilaya, ili waweze kutoa huduma hizo za afya.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Rashid Habib Ali, Mbunge wa Mtambwe, sasa aulize swali lake.

Na. 61

Suala la Mafuta na Gesi Kuondolewa Kwenye Orodha ya Masuala ya Muungano

MHE. RASHID HABIB ALI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa suala la mafuta na gesi kwenye orodha ya masuala ya Muungano?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Habib Ali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali zote mbili zimekubaliana kuondoa jambo la 15 la maliasili ya mafuta, pamoja na mafuta yasiyochujwa ya motokaa, mafuta ya aina ya petroli, aina nyinginezo za mafuta au bidhaa pamoja na gesi asilia katika orodha ya mambo ya Muungano. Kwa sasa, suala la mafuta na gesi asilia linasimamiwa na kila upande, ambapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetunga Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia ya Mwaka 2015, ambayo chini ya Kifungu cha 11 imeanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli *(Petroleum Upstream Regulatory Authority - PURA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi imetunga Sheria ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia, Namba Sita, ya Mwaka 2016, iliyoanzisha Mamlaka ya Udhibiti, Utafutaji na Uendeshaji wa Mafuta na Gesi *(Zanzibar Petroleum Regulatory Authority - ZPRA)* na Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar *(ZPDC)*. Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rashid Habib Ali, swali la nyongeza.

MHE. RASHID HABIB ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kutokana na majibu mepesi ya Serikali, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, mwaka 2009 Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kwa kauli moja liliazimia kuondoa suala la mafuta na gesi kwenye orodha ya mambo ya Muungano. Je, ni ipi kauli ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kutekeleza azimio hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali namba mbili. Kwa mujibu wa Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya Nne, ikisomwa pamoja na nyongeza ya kwanza, Kifungu cha 15, inaeleza wazi kwamba, suala la mafuta na gesi ni suala la Muungano. Kutokana na Ibara hiyo, je, ni upi mgao wanaoupata Zanzibar kutokana na gesi inayochimbwa Tanzania Bara?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naungana na Mheshimiwa Mbunge, ambaye amesema kwamba, Baraza la Wawakilishi liliridhia na liliwasilisha kutaka suala hili liondolewe. Ndiyomaana Baraza la Wawakilishi limetunga sheria mwaka 2015, ambayo chini ya Kifungu Namba 11, wameanzisha Mamlaka ya Udhibiti na kwamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili hivi sasa linashughulikiwa pande zote mbili; Zanzibar linashughulikiwa kivyao na huku Tanzania Bara linashughulikiwa kwa upande huu kwa hiyo, suala hili halina hoja kinzani yoyote kati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Mheshimiwa Mbunge ametaka kufahamu mgao unaotokana na uchimbaji wa mafuta na gesi. Kama ambavyo nimejibu kwenye swali langu la msingi, suala hili, pande zote mbili, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zilikubaliana kwamba, litashughulikiwa kila upande kwa kadiri ambavyo sheria zilizotungwa zinavyoruhusu.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Mheshimiwa Mbunge. Tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 62

Mkongo wa Mawasiliano Wilaya ya Tabora – Mlele

MHE. TASKA R. MBOGO aliuliza:-

Je, lini Serikali itaweka Mkongo wa Mawasiliano Kijiji cha Ipole, Wilaya ya Tabora hadi Kata ya Inyonga, Wilaya ya Mlele, kwani eneo hili lina wanyama wakali?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Katavi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa uwekaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwenye wilaya zote nchini, ili kufikisha huduma za intaneti ya kasi. Aidha, Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unaunganishwa na miundombinu ya watoa huduma wote wa mawasiliano nchini, ili kufikisha huduma hiyo kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2025/2026, Serikali imekamilisha ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kutoka Tabora kwenda Mpanda, kupitia Sikonge, Ipole

na Inyonga. Aidha, Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano umeunganisha Kituo cha Rungwa kutokea Ipole. Mkongo huo umejengwa kupitia miundombinu ya umeme ya *TANESCO*. Hatua zinazoendelea hivi sasa ni kuunganisha watoa huduma za mawasiliano kwenye maeneo hayo, ili waweze kufikisha huduma kwa Wananchi. Ninashukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Taska Mbogo, swali la nyongeza.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza. Swali hili nimekuwa nauliza humu Bungeni takribani miaka mitano; Wananchi wa Mkoa wa Katavi wanapofika yale maeneo ya Ipole kwenda Inyonga mpaka Mpanda, hakuna mawasiliano. Eneo hilo ni la hifadhi, kuna wanyama wakali na wamekuwa wanapata shida miaka yote hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu. Kwa kuwa, Serikali imesema imekamilisha ujenzi wa Mkongo wa Mawasiliano na wameuweka Rungwa. Je, Serikali itatumia muda gani kuwaunganisha wadau wa mawasiliano, kama *Airtel*, *Vodacom*, *Halotel* na *Yas,* ili Wananchi wa Mkoa wa Katavi waweze kupata mawasiliano?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwenye Mkoa wangu wa Katavi ukitoka Inyonga kwenda Mpanda ni eneo la hifadhi, kilometa 120, halina mawasiliano; kutoka Inyonga kwenda Majimoto, kilometa 138, halina mawasiliano; kutoka Kibaoni kwenda Mpanda Mjini, kilometa 120, hakuna mawasiliano; kutoka Mpanda Mjini kwenda Uvinza, zaidi ya kilometa 250, hakuna mawasiliano; je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wananchi wa Mkoa wa Katavi wanapata mawasiliano wanaposafiri katika maeneo hayo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayho mawili ya nyongeza.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la kwanza. Mkandarasi sasahivi yupo katika hatua ya ujenzi wa majengo yatakayotumika kufunga vifaa vya mawasiliano. Ujenzi wa majengo hayo unatarajiwa kukamilika ifikapo Mwezi Novemba mwaka huu na pia, sasahivi zoezi la utengenezaji wa vifaa vya kufungia mawasiliano hayo linaendelea na vyenyewe vinatarajiwa kukamilika ifikapo Mwezi Novemba. Itakapofika Mwezi Desemba mwaka huu mawasiliano yatakuwa yamefungwa katika hayo maeneo uliyoyataja kwenye swali la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili la mawasiliano katika maeneo ya barabara uliyoyataja. Hili ninakuomba Mheshimiwa, kama itakupendeza, ulilete kama swali la msingi, ili tuweze kukupa majibu yanayostahili, lakini Wizara yetu ya Mawasiliano ina mkakati wa miaka mitano wa kujenga na kufikia maeneo yote yenye changamoto ya mawasiliano hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya tathmini kama Wizara, kuna upungufu wa minara takribani 3,000. Zoezi linaloendelea ni kutafuta fedha, kwa ajili ya kutekeleza mradi huo na ifikapo mwaka 2030 nchi hii yote tutakuwa tumeifikia na changamoto ya mawasiliano itakuwa imekwisha. Ninakushukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Restituta pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kama haujaridhika utapeleka swali la msingi kwa hilo swali la pili.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Morris Makoi, swali la nyongeza.

MHE. MORRIS J. MAKOI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Katika Jimbo la Moshi Vijijini, katika Kata ya Uru Mashariki, Uru Kaskazini, Uru Shimbwe, Kibosho Magharibi na Kata ya Kindi, kumekuwa na changamoto kubwa sana ya mawasiliano ya

simu. Nimeandika barua rasmi nikaipeleka ofisini kwa Mheshimiwa Waziri. Je, Serikali ina mpango gani katika bajeti ya mwaka huu kuhakikisha tatizo hilo linatatuliwa katika maeneo hayo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua changamoto ya mawasiliano, hususan katika maeneo ya mjini, kwa sababu ya ukuaji wa miji na ongezeko la watu katika maeneo ya mjini ni kubwa. Wakati mwingine minara yetu inapungukiwa nguvu kutokana na ongezeko la watu na watumiaji wa mitandao ya simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwelekeza Mkurugenzi Mkuu wa *UCSAF,* kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, aende katika Jimbo la Moshi Mjini kufanya tathmini, ili tufahamu nini kinahitaji kufanyika, kama ni kuiongezea nguvu minara iliyopo au kujenga minara mipya. Kwa hiyo, baada ya tathmini hiyo ndio tutajua nini cha kutekeleza, ili kutatua tatizo la mawasiliano katika Jimbo la Moshi Mjini. Ninakushukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri ni Jimbo la Moshi Vijijini.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Naibu Spika, sawa, ni Moshi Vijijini.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Haran Sanga, swali la nyongeza.

MHE. HARAN N. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kuniona. Serikali imekuwa ikitoa ahadi za kuweka huduma ya *internet* katika usafiri wetu wa *SGR,* lakini ninataka niombe. Je, ni lini sasa huduma hiyo itakuwa inapatikana? Kwa sababu, kumekuwa na shida sana ukiwa unasafiri kupata huduma ya *internet*. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua changamoto ya mawasiliano, kama Wizara, kwenye treni za *SGR* na tunalifanyia kazi katika mradi ambao upo kwenye hatua ya manunuzi hivisasa, Mradi Na.11. Maeneo ambayo tutayapa uzito mkubwa katika utekelezaji wa Mradi huo ni maeneo ya *SGR*, reli ya *MGR*, reli ya *TAZARA,* Hifadhi za Taifa na maeneo ya mipakani. Kwa hiyo, tutakapotekeleza Mradi wa 11 wa Ujenzi wa Minara 280, ambao upo katika hatua ya manunuzi hivi sasa, eneo hili la *SGR* litafanyiwa kazi na ninaamini changamoto ya mawasiliano tutaimaliza. Ninakushukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa *Engineer* Amosy Maganga, swali la nyongeza.

MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninakushukuru sana kunipa hii nafasi. Awali ya yote, ninaanza kwa kutoa shukurani kwa Serikali, kupitia Wizara hii ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Tulipata changamoto katika Kata yetu ya Kitunda kwamba, tulikuwa hatuna mawasiliano kwa takribani wiki mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwasiliana na Mheshimiwa Naibu Waziri na ndani ya wiki tatizo liliisha, lakini kubwa zaidi ni pamoja na kutoa mrejesho kwangu kwa maandishi. Kwa kweli, huu ni utawala ulio bora kabisa na ninaipongeza sana Serikali kwa hatua inazofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, kati ya Kata ya Ipole kwenda mpaka huko Kitunda, umbali wa takribani kilometa 150, kupitia Hifandi ya Wanyapori ya Pembampanzi, hakuna mawasiliano kabisa. Je, ni lini Serikali sasa itatuwekea mawasiliano katika eneo hilo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimekuwa nikieleza katika Bunge hili kwamba, Wizara yetu ina mpango mkakati wa miaka mitano wa kufikisha mawasiliano katika wilaya zote za nchi hii na majimbo yote ya nchi hii. Namhakikishia Mheshimiwa *Engineer* Maganga kwamba, katika maeneo aliyoyataja tutayafikia katika mkakati wetu wa miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, namwelekeza Mkurugenzi Mkuu wa *UCSAF* kufika katika maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge, kufanya tathmini na kujua mahitaji yanayohitajika, ili kumaliza tatizo hilo la changamoto ya mawasiliano.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi.

Ninamwita Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 63

Ujenzi wa Meli Ukanda wa Pwani

MHE. AGNES E. HOKORORO aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa meli ukanda wa pwani, ili iweze kuunganisha nchi yetu na nchi jirani?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa David Kihenzile, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Kampuni ya Meli Tanzania *(TASHICO)* imekamilisha utafiti wa masoko katika mwambao wa Bahari ya Hindi, ili kujua mahitaji ya meli inayotakiwa kujengwa, kwa ajili ya kusafirisha mizigo kati ya Tanzania na nchi jirani. Aidha, katika mwaka huu wa fedha 2026/2027, Serikali imetenga kiasi cha fedha shilingi bilioni 10, ili kuanza taratibu za ujenzi wa meli mpya itakayofanya safari zake kati ya Tanzania na nchi jirani kupitia Bahari ya Hindi. Kwa sasa *TASHICO* inaendelea na taratibu za manunuzi, kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa kujenga meli hiyo. Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, swali la nyongeza.

MHE. AGNES E. HOKORORO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, lakini ninaomba nitumie fursa hii kuipongeza sana Wizara na Serikali kwa namna ilivyofanya haraka kuhakikisha hili zoezi linakamilika na hasa lile la kufanya utafiti. Sasa nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza. Kwa kuwa, hii meli tumeambiwa kwamba, shilingi bilioni 10 zimetengwa kwa mwaka huu wa fedha. Swali hapa ni kwamba, je, lini ujenzi utaanza na utakamilika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa, hii meli ni, kwa ajili ya mizigo katika mwambao wa pwani, ili kutuunganisha na nchi za jirani, lakini huko nyuma sisi wakati tunakua tulikuwa tunasafiri kwa kutumia usafiri wa meli na kwa sasa bidhaa nyingine katika Mkoa wa Mtwara zimeendelea kupanda kwa sababu ya kusafirishwa kwa mabasi; hapa ninazungumzia ile mizigo midogo ama tunasema *loose cargo,* ambayo ingeweza kusafirishwa kwa meli nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga meli ya abiria, ili kurahisisha usafiri katika mwambao wa pwani katika Mkoa wa Mtwara na mikoa mingine nchini kwetu? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Agnes Hokororo, Mbunge wa Viti Maalam, Mkoa wa Mtwara, ambaye pia, ni Katibu wetu wa Wabunge wa CCM hapa Bungeni kwa kazi kubwa anayofanya ya kuturatibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ninampongeza kwa namna anavyofuatilia kwa karibu usafiri na usafirishaji katika Bahari ya Hindi, hususan kwenye ukanda wa bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ameuliza maswali mawili na kabla hajauliza, ametoa pongezi. Ninamhakikishia pongezi hizi zitafika Serikalini, ambapo kimsingi Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ndiyo imeamua na ameipongeza jinsi ilivyoharakisha kuhakikisha kwamba, inaanza kuboresha usafiri huo na tunapata meli kwenye Bahari yetu ya Hindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, ameuliza lini ujenzi utaanza; kwa sasa tupo kwenye manunuzi. Tunakusudia kukamilisha taratibu za kimanunuzi ifikapo Disemba mwaka 2026 na mara baada ya kumaliza taratibu za kumpata mkandarasi tunategemea akianza kazi atatumia miaka miwili na hatimaye meli hiyo ya mizigo itakuwa imekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ameuliza, lakini pia, ametoa ushauri kwamba, je, Serikali haioni umuhimu katika kuboresha upande wa meli za abiria; tumefanya tathmini ya kina na ikaonekana kwamba, soko linahitaji zaidi meli upande wa mizigo. Tutakapotoka hapo tutakwenda hatua ya pili ya kutazama fursa nyingine zilizopo, ikiwa ni sambamba na ushauri ambao Mheshimiwa Mbunge ameutoa kuhakikisha kwamba, tunapata meli za abiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatumia fursa hii pia, kuwaomba sekta binafsi, kama ambavyo tumezungumza, sekta ya uchumi wa buluu inazidi kushamiri, mizigo inazidi kuongezeka na watumiaji

wanazidi kuongezeka. Ni vyema sasa tukachangamkia fursa kujenga meli katika Bahari ya Hindi na kwenye maziwa makuu, Serikali peke yake haina uwezo wa kupata meli hizo zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeboresha miundombinu, inajenga Bandari ya Mtwara, Kisiwa Mgao, kwa shilingi bilioni 435. Tayari imejenga Bandari ya Mtwara kwa shilingi bilioni 157, imeboresha Bandari ya Tanga, Bandari ya Dar es Salaam na tunakwenda Bagamoyo. Miundombinu hii yote inahitaji vitendea kazi vya kutosha, hivyo, ni vyema sekta binafsi ikachangamkia fursa hii kuona namna inavyoweza kushiriki katika ujenzi wa uchumi wa taifa letu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Regina Malima, swali la nyongeza.

MHE. DKT. REGINA C. MALIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi, ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali katika kuhakikisha Watanzania wanapata usafiri ambao ni wenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninauliza tu, katika Kisiwa cha Ukerewe au Jimbo la Ukerewe, kwa 100% tunategemea maji, ili kuweza kupata *connection* kwenda Mwanza na maeneo ya visiwa vingine. Tumekuwa na meli mbili za Serikali, *Mv Clarius,* ambayo ni mbovu na haifanyi kazi kabisa na pia, *Mv Butiama*, ambayo ilifanyiwa matengenezo na kufanya kazi kwa wiki mbili tu na mpaka sasa imesimama haifanyi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nini kauli ya Serikali kuhakikisha kisiwa hiki cha pekee ambacho kina visiwa 38 kinapata usafiri wa uhakika wa meli? Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ameuliza kuhusiana na meli zetu mbili; *Mv*

Clarius pamoja na *Mv Butima*. Ni kweli kabisa Serikali inatambua kwamba, Kisiwa cha Ukerewe kinategemea sana meli hizi, ili kurahisisha usafiri na usafirishaji katika Ziwa Victoria. Tumeanza taratibu, ikiwa ni pamoja na kutenga fedha, kwa ajili ya kuanza maboresho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli meli hizi zilisimama baada ya kujiridhisha kwamba, pamoja na kwamba tulifikia hatua nzuri, usalama wake siyo wa uhakika. Hivyo, tukaona ni bora zisimame, tujiridhishe, tuziboreshe vizuri zaidi, ili zikianza zikianza ziweze kufanya kazi vizuri kwa sababu, kipaumbele cha kwanza kwenye vyombo vya majini, kama ilivyo angani, ni usalama wa abiria wanaotumia vifaa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tumepokea hoja yake. Tutaongeza msukumo, ili tuweze kukamilisha hatimaye ziweze kurudi majini na kuboresha usafirishaji, kwa ajili ya wananchi wetu wa Ukerewe.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 64

Kubadilisha Mkataba wa Kusambaza Umeme, Mufindi

MHE. EXAUD S. KIGAHE aliuliza:-

Je, lini mkataba wa kusambaza umeme kutoka *Mwenga Power* kwenda *TANESCO* utabadilishwa, ili *Mwenga Power* wabaki kuwa wazalishaji tu?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Salome Makamba, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, usambazaji wa umeme katika Wilaya ya Mufindi unafanywa na Kampuni ya *RVE* Tanzania, kupitia kampuni zake tanzu za *Mwenga Power Services Limited,* kupitia leseni ya usambazaji umeme na *Mwenga Hydro Limited* inayohusika na uzalishaji wa umeme kiasi cha MW 4 kutoka Mto Mwenga, pamoja na MW 2.4 zinazotokana na upepo katika eneo la Usokami lililopo wilayani humo. Utoaji na usimamizi wa leseni za uzalishaji na usambazaji wa umeme nchini ni jukumu la kisheria la Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji *(EWURA),* kwa mujibu wa Sheria ya Umeme ya mwaka 2008 na taratibu husika za utoaji leseni. Hivyo, uamuzi wowote wa kubadili muundo wa leseni ya usambazaji umeme katika eneo hilo unapaswa kuzingatia matakwa ya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kwa kutambua kuwa, kumekuwa na malalamiko ya ubora wa huduma inayotolewa na *Mwenga Power* tayari Serikali, kupitia taasisi zake za *EWURA, TANESCO* na *REA,* imeanza tathmini ya kina, ili kuona uwezekano wa kufanya mabadiliko hayo pasipo kuathiri uwekezaji uliofanyika katika maeneo husika kwa lengo la kutafuta suluhisho la kudumu litakalowawezesha wananchi wa Mufindi Kaskazini na maeneo mengine kupata huduma bora na ya uhakika ya umeme, kama ilivyo kwa maeneo mengine nchini. Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Exaud Kigahe, swali la nyongeza.

MHE. EXAUD S. KIGAHE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Kwanza nachukua nafasi hii kuishukuru sana

Serikali ya Awamu ya Sita kwa kusikiliza na kutambua changamoto tulizonazo katika Jimbo la Mufindi Kaskazini kwenye sekta ya nishati. Pia, ninampongeza sana Naibu Waziri kwa kazi nzuri na usikivu wake kwetu sisi Wabunge wenzake wakati tunampelekea changamoto ya maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo maswali mawili. Kwanza hawa *Mwenga Hydro Power* kwa kweli, wamekuwa changamoto kubwa sana kwa muda mrefu. Kuna wakati inatokea wanakata umeme zaidi ya siku tatu bila taarifa. Juzi nilikuwa jimboni, wamekata umeme tangu saa mbili mpaka saa nane mchana bila taarifa, hata jana wameendelea na ninadhani hata leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa sababu changamoto hii imekuwa kubwa na Serikali imetambua. Ninaomba watuhakikishie, Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini watatuma timu yao ya wataalamu wa *TANESCO, EWURA* na *REA,* ili wakafanye tathmini ya kina waone changamoto hii kubwa, ambayo tunayo katika Jimbo la Mufindi Kaskazini?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili. Kwa usikivu wao mkubwa, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mbunge mwenzangu, amewahi kunisikiliza. Je, yuko tayari kuandamana na mimi baada ya Bunge hili, ili akasikie changamoto hizi kutoka kwa wananchi wenyewe wa Jimbo la Mufindi Kaskazini, ambavyo wanapata tabu kwa sababu ya kukosa umeme unaosambazwa na hawa *Mwenga Hydro? (Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninampongeza kaka yangu, Mheshimiwa Kigahe, kwa kufuatilia changamoto za umeme zinazowapata wananchi wake. Kwa faida ya wananchi wa Mufindi Kaskazini nasema, Mheshimiwa Kigahe amekuwa anashiriki kuhakikisha pale ambapo miundombinu ya umeme inachelewa kufika anashiriki na wananchi wake na anachangia kuhakikisha kwamba, nguzo zinafika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu namba moja la Wizara ya Nishati ni kuhakikisha wananchi wanapata umeme wa uhakika pamoja na taarifa pale ambapo panatokea changamoto. Sasa Mheshimiwa Mbunge unafahamu, tumekuwa na vikao ofisini katika kufanya tathmini, tumekushirikisha na timu ya wataalamu inaendelea kufanya uchambuzi. Kubwa ambalo Mheshimiwa Mbunge nakuahidi ni kwamba, tathmini hii itafanyika kwa haraka, ili wananchi hawa waweze kunufaika na umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili. Hili wala siyo ombi, kazi yangu kubwa mimi, kama Naibu Waziri, ni kusikiliza changamoto wanazopata Waheshimiwa Wabunge. Nakuahidi Mheshimiwa Mbunge, tukatapomaliza Bunge hili niko tayari kuongozana na wewe, kwa ajili ya kwenda kuzungumza na wana-Mufindi na kuona changamoto wanayopata. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, maswali ya nyongeza mafupi. Mheshimiwa Issa Mchungahela.

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru. Nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi njema anayoifanya. Jimboni kwangu kuna changamoto ya umeme katika vitongoji kadhaa na sababu kubwa inasemwa kwamba, ni umbali wa kilometa tatu na zaidi. Ni lini Serikali itaona ina uwezo wa kutatua changamoto ya umeme katika maeneo haya na kuepuka hili jambo la umbali? Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika Dira ya Maendeleo ya mwaka 2050. Moja kati ya jukumu kubwa ambalo tumepewa Wizara ya Nishati ni kuhakikisha tunapunguza umbali wa nyaya kati ya wilaya na wilaya kwa kujenga *substation,* hilo ndilo lengo letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge amesema, bado sijafahamu changamoto kubwa inasababishwa na umbali wa nyaya au uchakavu wa miundombinu. Ninaomba nikuahidi Mheshimiwa Mbunge, nitaifanyia kazi changamoto yako, tutakuja kuzungumza, lakini tutakwenda kuangalia maeneo hayo, ili tuweze kutatua changamoto hiyo kulingana na lile ambalo liko katika eneo lako Mheshimiwa Mbunge. Ninakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Masache Kasaka, swali la nyongeza.

MHE. MASACHE N. KASAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Wilaya ya Chunya ina changamoto kubwa sana ya umeme, hali inayosababisha umeme kukatika mara kwa mara. Tunaishukuru Serikali kwa kuanza kujenga *line* mpya ya umeme, lakini pamoja na ujengaji huo umeme unakatika mara kwa mara bila taarifa yoyote, hali inayosabaisha wananchi wengi kuunguziwa vifaa vyao, hasa mitambo maeneo ya uchimbaji. Je, ipi kauli ya Serikali juu ya wananchi hawa ambao mitambo na vifaa vyao vinaungua, namna gani ambavyo wataweza kulipwa fidia?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa swali zuri. Pia, umekuwa unafuatilia kwa karibu sana na kama unakumbuka, imesabaisha mpaka aliyekuwa Waziri wetu wa Nishati kuja kufanya ziara, ili kuweza kujua changamoto hii tunaitatua vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa ni kwamba, *line* ya umeme iliyokuwa inapeleka umeme kule ilikuwa inapeleka umeme mdogo sana. Wewe unafahamu Mheshimiwa Mbunge, sasahivi tunaendelea na ujenzi wa *line* ya *TAZA,* ambayo inakwenda mpaka Zambia na tunatarajia mpaka Disemba mwaka huu, *line* ile itakuwa imekamilika maana mkandarasi yuko *site* na amelipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna hakika tukiwasha katika *line* hii ya *TAZA* changamoto ya kukatika kwa umeme katika jimbo lako itapungua sana. Kama hiyo haitoshi, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, mmetutengea zaidi ya shilingi bilioni 25, kwa ajili ya kwenda kuimarisha na kujenga *line* za umeme katika maeneo ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamuahidi Mheshimiwa Mbunge, kwa maeneo ya wachimbaji wadogo wa kwako, tunaweza tusikamilishe pote, lakini wengi watapata faida ya kupelekewa *line* na transfoma za uhakika, ili waweze kufanya shughuli za kiuchumi. Ninakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwita Waitara, swali la nyongeza.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Salome Makamba, alifanya kazi nzuri sana katika mkutano wa Sirari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Tarime ina majimbo mawili, Tarime Mjini na Tarime Vijijini, lakini uso wa Tarime ni Tarime Mjini. Ni aibu sana, yaani umeme unakatika kwa kiwango ambacho si cha kawaida pale mjini. Ninaomba Mheshimiwa Naibu Waziri awasaidie wafanyabiashara wa Tarime, vifaa vya umeme vimeungua, *tv,* kwenye hoteli wamepoteza wateja sana na unajua sisi tupo mpakani, ni eneo la kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nipate majibu ya Serikali. Ni lini changamoto hiyo ya kukatika umeme Tarime Mjini itapata tiba ya kudumu? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza pia, Mheshimiwa Mwita Waitara, kaka yangu, kwa kazi kubwa anayoifanya. Mheshimiwa Waitara utakumbuka

tumefanya mkutano wa hadhara pale kwako Tarime na katika mkutano ule niliwaahidi wana-Tarime kwamba, tunaendelea na kazi kubwa ya kujenga *line* ya umeme kutoka Chalinze kuja Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatumia fursa hii kuwaambia Watanzania kwamba, sasa tumewasha *line* ile, ambayo inatoa umeme katika Bwawa la Mwalimu Nyerere kuja Dodoma. Watu wanaoishi Dodoma watakubaliana na mimi changamoto ya kukatika kwa umeme imepungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *line* ile hivisasa tunafanya *extension* kuelekea Singida – Shinyanga. Pale Shinyanga tumejenga *substation* ya uhakika, maana yake ni kwamba, *line* inayotoka Shinyanga kwenda Mwanza mpaka Musoma sasahivi itakuwa ni *line* ya uhakika. Mheshimiwa Waitara pamoja na Wabunge wote, ninamuona dada yangu Mheshimiwa Ester Bulaya, pia tuna *substation* pale kwako tumejenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawahakikishia wananchi wote wa Kanda ya Ziwa, tutakapokamilisha ujenzi wa *line* hii umeme utakuwa wa uhakika na utakuwa, kwa ajili ya uzalishaji na siyo kuwasha taa peke yake. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge, tunakushukuru sana. Tunaendelea, Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Ushetu, sasa aulize swali lake.

Na. 65

Serikali Kushughulikia Bei ya Pembejeo

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI aliuliza:-

Je, upi mkakati wa kushughulikia bei ya pembejeo, ambayo ipo juu tofauti na gharama za uzalishaji ikizingatiwa kuwa, bei ya tumbaku imeshuka?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, karibu kwa majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo ninaomba sasa nijibu swali namba 65 la Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani:-

Mheshimiwa Naibu Spika, bei za pembejeo za kilimo, ikiwemo za tumbaku, zimeongezeka katika Soko la Dunia kutokana na mgogoro ambao unaendelea Mashariki ya Kati. Katika kushughulikia changamoto hiyo, Serikali imeziomba taasisi za fedha zinazowezesha wakulima wa tumbaku kupunguza riba ya mikopo ya pembejeo, ili kumpa nafuu mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki za *NBC* na *CRDB* zimekubali kupunguza riba kutoka 10% hadi 9%. Benki za *NMB* na Benki ya Ushirika Tanzania zinaendelea kufanya mapitio ya masharti ya malipo ya mikopo hiyo, ili kumpatia mkulima wa tumbaku unafuu wa kulipa mkopo wa pembejeo. Vilevile, *TCJE* inaendelea kuhakikisha kuwa, wanapatikana wasambazaji wa mbolea wa bei nafuu. Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, swali la nyongeza.

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza, ninatoa shukrani kubwa kwa Kampuni ya *Mkwawa Leaf Tobacco* kwa jinsi ilivyonunua zaidi ya kilo 64,214,000 za tumbaku, ni kiwango kikubwa sana. Pia, ninampongeza Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Tumbaku kwa usimamizi mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sheria Ndogo ya Bodi ya Tumbaku na *Tanzania Tobacco Council* tumekubaliana bei ya tumbaku isiwe chini ya bei elekezi. Ukizingatia bei ya pembejeo imepanda sana juu na wakulima wameuza chini ya wastani wa bei elekezi, Dola za Kimarekani 1.60, na wamekula hasara. Ninataka kujua kauli ya Serikali juu ya hasara ambayo wakulima wameipata?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Wakulima wengi wameuza tumbaku zao zote na wengi wameshindwa kumaliza madeni…

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tuongee kwa sauti ya chini na Mheshimiwa Mbunge pia ongeza sauti kidogo.

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya bei kuwa chini. Ninataka kujua mkakati wa Serikali ulivyo kwa sasa, ni namna gani mnaweza kuwasaidia wakulima hawa, ili waweze kupunguziwa au kusogezewa kulipa madeni yao taratibu, warudi tena shambani msimu ujao kwa sababu, wamekula hasara kulingana bei kuwa chini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nijue sasa *commitment* kubwa ya Serikali ili wakulima hawa waweze tena kurudi shambani badala ya kukimbizana, kukamatwa na benki wakati hasara haikuwa upande wao.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Cherehani amekuwa ni mwanaushirika wa kweli na pia amekuwa mpambanaji mkubwa wa vyama vya ushirika, pia wakulima kupata bei ambayo inalingana na jasho na *investment* ambayo unaiweka katika mnyororo mzima wa thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kwanza kukiri kwamba ni kweli kwamba bei ya tumbaku katika soko la dunia

imeporomoka na kwa muktadha huo, Serikali imechukua hatua kadhaa kutengeneza mazingira nafuu kwa wakulima wa tumbaku, kuliokoa zao la tumbaku na kuwapa nafuu wakulima wa tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya hatua hizo kama nilivyotangulia kujibu kwenye jibu la msingi kwamba, Serikali kwa kushirikiana na taasisi za fedha, kwa kuwa wateja wa tumbaku ni moja ya wateja wakubwa wa taasisi zetu za fedha, kuona kwamba wanawekewa mazingira nafuu ya urejeshaji wa fedha lakini pia kupunguza riba. Kama nilivyotangulia kusema, benki ya *NMB* na *CRDB* zimekubali kupunguza riba kutoka asilimia 10 hadi asilimia tisa pia kuona namna bora ya kuweka mazingira rafiki ya urejeshaji wa mikopo kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuporomoka kwa bei ya tumbaku kumetuathiri pia sisi na vilevile vita ambayo inaendelea kule Mashariki ya Kati imeongeza gharama ya usafirishaji wa pembejeo na hivyo kuathiri bei ya pembejeo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua nyingine ambayo Serikali imechukua ni kuanzisha bima ya mazao ili huko mbele tunakoelekea bei ya mazao kama tumbaku inapodondoka *then* hii bima ya mazao ita-*chip in* kwa ajili ya kuokoa wakulima wa tumbaku ambao wanaenda kupata athari za moja kwa moja kutokana na kuanguka kwa bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na wakulima kuuza tumbaku yao yote lakini malipo yao kuwa bado, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Cherehani kwamba, Serikali iko makini, tutazifuatilia kampuni zote ambazo zina madeni kwa wakulima na kuona namna ambavyo wanaenda kulipa madeni yote ya wakulima ili mkulima arudi shambani kwa ajili ya msimu ujao, ili kukidhi malengo ya Serikali kuongeza zao la tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, unaohusiana na kulipa kidogo kidogo wakulima ili kumaliza

deni hilo kwa wakati. Serikali inalichukulia kwa uzito na tunaenda kuifanyia kazi kuona utekelezaji wake. Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Edwin Swalle, swali la nyongeza swali fupi.

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mwezi uliopita nilikwenda kufanya ziara Jimbo la Lupembe na nilipita Kata zote. Wananchi wana kilio kikubwa cha bei ya pembejeo kuwa juu wakati bei ya mahindi ikiwa chini.

Je, Serikali ina mpango upi wa kushusha bei ya pembejeo na kuongeza bei ya mahindi nchini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwa swali la nyongeza la Wakili Msomi Ndugu yangu Edwin Swalle.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakiri ni kweli kwamba, bei ya pembejeo iko juu, lakini si kwa Tanzania tu dunia nzima bei ya pembejeo imeenda juu kutokana na wazalishaji wakubwa wa mbolea, hasa kule Ulaya ya Mashariki, kwa maana ya Urusi na Ukraine lakini pia huku Mashariki ya Kati kwa maana ya kile ambacho kinaendelea Iran na vile vitu ambavyo vinaendelea, vimesabisha Mfereji wa Hormuz kufungwa na hivyo meli chache ambazo zinapita ambazo zinabeba pembejeo hasa za kilimo zimekuwa zikigombewa kwa bei, kwa hiyo imepelekea mfumko wa bei ya pembejeo dunia nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Serikali imejipanga vipi? Dira yetu ya 2020 - 2050 inaelezea kuhusiana na kuongeza thamani ya bidhaa zetu na hiyo ikiwemo gesi pamoja na magadi soda na bidhaa nyingine ambazo tunaweza tukazalisha mbolea kupitia hizo. Pia, tumekuwa katika jitihada za kuvutia wawekezaji na tumeweka vivutio vingi ili tuone kwamba wawekezaji wengi wanakuja

wanajikita katika eneo la kuzalisha mbolea ili tukidhi soko la ndani na ikiwezekana tuanze kusafirisha nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imejipanga katika utekezaji wa Dira 2020 - 2050 Tanzania inaenda kujitegemea katika pembejeo hasa mbolea. Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Asha Salum Motto Mbunge wa Viti Maalum, sasa uulize swali lake.

Na. 66

Ahadi Ya Kusambaza Trekta Elfu Kumi Katika Vijiji – Nchini

MHE. ASHA S. MOTTO aliuliza:-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kusambaza trekta Elfu Kumi katika Vijiji vyote nchini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO: alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijibu swali Namba 66 kutoka kwa Mheshimiwa Asha Salum Motto, Mbunge wa Viti Maalum Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo inaendelea kutekeleza ahadi yake ya kusambaza trekta 10,000, ambapo hadi sasa vituo 79 vya kutoa huduma ya zana za kilimo kwa wakulima vimeanzishwa. Trekta kubwa 555, trekta za mkono 800 pamoja na zana zake zimenunuliwa na kusambazwa katika vituo hivyo kwa ajili ya kusogeza huduma karibu na wakulima nchini ikiwemo vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, vyama vya ushirika vitakuwa vituo vya ukodishaji wa matrekta haya na Serikali itaendelea kuviwezesha vyama hivi viweze pia kununua trekta kwa ajili ya ukodishaji. Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Asha Salum Motto swali la nyongeza.

MHE. ASHA S. MOTTO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri. Aidha, ninaipongeza sana Serikali chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uzalendo mkubwa na kuwatumikia kwa dhati kabisa wananchi, hususan wakulima, kwa kuwapatia zana za kilimo. Pamoja na juhudi kubwa za Serikali za kusambaza matrekta nchini lakini bado kasi ni ndogo sana ya usambazaji wa matrekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na uzalishaji mkubwa wa zao la korosho nchini lakini wananchi wa Mkoa wa Mtwara tayari wamedhihirisha kwa vitendo kufanya mbadala wa uzalishaji wa mazao kwa wingi, hasa Choroko, Mbaazi na Ufuta. Changamoto kubwa ni ukosefu wa zana za kilimo, ikiwemo trekta.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapa kipaumbele wananchi wa Mkoa wa Mtwara hususan kuweza kuwapatia trekta za kutosha ili kuongeza tija kwa uzalishaji kwa wakulima na taifa kwa ujumla?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Asha Salum Motto Mbunge wa Viti Maalum kwa namna ambavyo anapambana kuhakikisha kwamba Mkoa wa Mtwara unakuwa kitovu cha uchumi hasa kwenye sekta ya kilimo, na kuona kwamba utekelezaji wa Ilani yetu kupitia usambazaji wa zana za kilimo hasa trekta Mtwara inaenda kukumbukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyofahamu kwamba, tumemaliza juzi kupitisha bajeti ya Serikali ya 2026/2027 na hivi sasa

ni miezi mitatu tu ya utekelezaji wa bajeti hiyo. Ndani ya hii miezi mitatu, kama nilivyotangulia kujibu kwa jibu la msingi zaidi ya trekta kubwa 555 na trekta za mkono 800 na vituo 79 vya kutoa huduma ya zana za kilimo vimeanzishwa. Kwa hiyo *speed* ambayo tunaenda nayo ni nzuri, na nina uhakika tutafikia malengo ndani ya muda ambao umepangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Serikali ina mpango wa kuzindua mkakati wa taifa kuhusiana na zana za kilimo kwa awamu ya pili 2026 – 2035 ambayo unaenda kujumuisha vituo jumuishi vya zana za kilimo zaidi ya 1000 nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tuna dira ya maendeleo ya 2020 - 2050 inaelekeza wazi ushiriki wa sekta binafsi kwa 70%. Hii pia ni fursa kwa sekta binafsi kwa kuwa tumetoa vivutio kwa sekta binafsi. Naomba Mheshimiwa Mbunge kupitia Halmashauri ambayo yeye pia ni diwani kuona kwamba wanaunga mkono katika utekelezaji wa dira yetu wa kushiriki kikamilifu katika ununuzi wa zana za kilimo na kuwasambazia kupitia vyama vya ushirika. Pia wadau binafsi tumewawekea vivutio kupitia *TISEZA* kwa ajili ya kuja kuanzisha viwanda vya kuunganisha pamoja na kuzalisha na kusambaza zana za kilimo ili tufikie malengo. Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Asia Halamga swali la nyongeza.

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Serikali iliweka mkakati katika Wilaya ya Hanang' ya kupelekewa zana za kilimo na kuanzishwa kwa vituo vinne. Kwa kuwa tunaelekea msimu wa mvua na mpango huu bado haujaja kutekelezwa. Je, Serikali haioni haja ya kuleta zana hizi badala ya vituo vinne ikaanza na kituo kimoja ili kukimbizana na msimu wa mvua?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa ahadi hii ya

Serikali kama nilivyotangulia kusema kwamba tunaenda kujenga vituo jumuishi zaidi ya 1,000 kwa ajili ya usambazaji wa zana za kilimo na maeneo mengi kupitia vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge wa Hanang' kwamba Mkoa wa Manyara ni moja ya Mkoa wa kipaumbele. Wilaya ya Hanang' hususan kuna malengo ambayo tumeyaweka, napokea ushauri wake kwamba walau tuanze na kituo kimoja cha usambazaji wa zana za kilimo na hilo ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa tunaenda kuanza nalo. Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Edifonsi Joackim Kanoni, Mbunge wa Kalambo, sasa ulize swali lake.

Na. 67

Utafiti katika wingi wa Samaki
Ziwa Tanganyika

MHE. EDIFONSI J. KANONI aliuliza:-

Je, lini Serikali itafanya utafiti katika Ziwa Tanganyika ili kujua wingi wa Samaki?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi ninaomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Edifonsi Joackim Kanoni, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ina utaratibu wa kufanya utafiti wa kubaini wingi na mtawanyiko wa samaki wa tabaka la juu katika Ziwa Tanganyika kwa kupitia Taasisi yake ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania *(TAFIRI)*. Utafiti huo hufanyika kwa kushirikiana na nchi ya Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo *(DRC)* na Zambia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Tanzania, utafiti wa aina hiyo umefanyika mwaka 1998, 2022 na 2024. Kwa mwaka 2025 na 2026, utafiti ulifanyika kwa kushirikiana na nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokasia ya Kongo *(DRC)* na Zambia. Matokeo ya utafiti huo yanaonesha kuwa, kiasi cha samaki katika Ziwa Tanganyika kimepungua kutoka tani 304,500 mwaka 1998 hadi takribani tani 116,000 mwaka 2026, sawa na upungufu wa asilimia 62.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii inaonesha mwenendo wa kupungua kwa rasilimali za samaki, hususan dagaa na migebuka. Hivyo, Serikali inaendelea kuimarisha mifumo ya ulinzi wa mazalia ya samaki na udhibiti wa uvuvi usiozingatia sheria ili kuwezesha samaki kuzaliana na kuongezeka katika Ziwa pamoja na kuendeleza teknolojia ya ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa wito kwa umma kuhakikisha wanashiriki katika utekelezaji wa mipango ya ulinzi wa rasilimali, mazalia ya samaki pamoja na kuzingatia uvuvi unaofuata sheria. Aidha, Serikali inakamilisha mchakato wa kuunda Mamlaka ya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi ili kuimarisha zaidi mifumo ya usimamizi na udhibiti wa rasilimali za uvuvi. Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Edifonsi Joackim Kanoni swali la nyongeza.

MHE. EDIFONSI J. KANONI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana Serikali kwa majibu mazuri. Niipongeze sana Wizara pamoja na Waziri Mheshimiwa Bashiru Ally na Mheshimiwa Naibu

Waziri kwa jinsi ambavyo wanahangaika na kutatua changamoto za wavuvi na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kunusuru wananchi na wavuvi katika Ziwa Tanganyika, Jimbo la Kalambo, Mkoa wa Rukwa, Mkoa wa Katavi, Kigoma na kuwa na uvuvi endelevu. Je, ni lini sasa Serikali itaunda mamlaka ya udhibiti uvuvi usiozingatia sheria?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Wananchi na wavuvi wa Jimbo la Kalambo, Tarafa ya Kasanga Kata ya Kasanga wameendelea kusubiri kwa hamu ukamilishaji wa soko la samaki ambalo litawanufaisha katika kuongeza thamani ya mazao yao. Je, lini sasa Serikali itakamilisha soko hilo ambalo limesimama kwa zaidi ya miaka miwili sasa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Ninaomba kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge Kanoni kwa sababu ni mara nyingi sana amekuja Wizarani na pia amefuatilia hata kwa njia ya simu maendeleo ya Soko hili la Kasanga na pia rasilimali za uvuvi katika Ziwa Tanganyika hasa kwa wananchi wa Jimboni kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza swali lake juu ya lini hasa tutakamilisha uundwaji wa mamlaka hii ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uundwaji wa mamlaka hii ni maelekezo ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya uchaguzi wa mwaka 2025 - 2030 lakini pia ni maelekezo ya Ilani ya mwaka 2025 na pia ni maelekezo ya Kamati ya Bunge ya kudumu inayosimamia Wizara yetu. Hivyo nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote wanaotusikiliza ambao ni wanufaika wa rasilimali za Ziwa Tanganyika, kwamba tayari tuko katika hatua nzuri na hatua za mwishoni za kukamilisha undoaji wa mamlaka hii. Pindi tutakapokamilisha hatua zetu za ndani basi tutaleta sheria hii ndani

ya Bunge hili Tukufu. Tutaomba sana ushirikiano wa Wabunge wote ili tuweze kupitisha sheria hii na kuanza rasmi mamlaka hii ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi ili kuweza kulinda na kusimamia rasilimali katika maziwa yetu makuu na maziwa madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, katika Soko hili la Kasanga ni kweli mkataba ulisainiwa mwaka 2023 na na mradi huu wa ujenzi wa soko hili ulikuwa na thamani ya takriban bilioni 1.4. Hadi sasa mkandarasi amekwishalipwa bilioni 1.312 na ujenzi wa soko hili umefikia asilimia 92. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba, sasa hivi mwenendo wa Wizara yetu kwanza ni kukamilisha miradi yote iliyokwishaanza na iliyokwama kwa sababu moja au nyingine kabla hatujaanza miradi mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo moja ya vipaumbele vyetu ni Soko hili la Kasanga kwa kukamilisha malipo haya ya fedha hizi zilizobaki ili basi tumalizie hizi asilimia nane na wananchi waanze kunufaika na soko hili. Ninakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Tinnar Chenge, swali la nyongeza.

MHE. TINNAR A. CHENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona na nashukuru majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri inaonekana kwamba kuna upungufu mkubwa sana wa samaki kwenye Ziwa Tanganyika. Siyo Ziwa Tanganyika tu, bali ni hata katika Ziwa Victoria. Pamoja na jitihada nyingi ambazo mmezieleza hapo. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza Samaki, kwa maana ya *restocking,* kwenye maziwa haya ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa samaki kwenye maziwa yetu haya makuu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Ni kweli upungufu huu wa samaki tunaoupata kwenye Ziwa Tanganyika si kwa Ziwa Tanganyika pekee yake, hii inakwenda mpaka kwa Ziwa Victoria na hivyo inaathiri pia wananchi walioko katika Mikoa inayozunguka maziwa haya na hasa wale ambao wanategemea shughuli za uvuvi kama shughuli kuu za upatikanaji wa uchumi katika familia na jamii zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Wizara tunatambua changamoto tuliyonayo na tunatambua uzito wa changamoto hii hasa katika utekelezaji au kufikia malengo yetu ya Dira ya maendeleo ya mwaka 2050.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekwishaanza kuchukua hatua mbalimbali, mojawapo ikiwa ni kuendeleza nguvu na kuongeza nguvu katika kupambana na uvuvi usiozingatia sheria kwa sababu ndiyo sababu kuu ambayo imetufikisha katika upungufu huu wa rasilimali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni kuendelea kuimarisha ushiriki wa wananchi katika harakati hizi kupitia *BMU* na kwa kuwaona moja kwa moja TAMISEMI ambao nao wameendelea kutupa ushirikiano mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mwaka jana tuliongeza *stocking* ya vifaranga zaidi ya 10,000 katika Ziwa Tanganyika ikiwa ni mbinu mojawapo ya kuongeza wingi wa samaki katika ziwa hilo na tunaendeleza pia jitihada mbalimbali za kuwezesha wananchi hasa vijana kuingia katika uvuvi wa samaki kwa vizimba ili pia kuendelea kupunguza upungufu wa samaki kwa wananchi wetu na kuongeza uchumi kupitia sekta yetu ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea na hatua hizi, lakini tunaendelea kuomba na kuwasihi wananchi kwa sababu wao haswa ndiyo ambao wako katika rasilimali zetu waendelee kutupa ushirikiano sisi kama Wizara lakini pia Serikali kupitia TAMISEMI katika maeneo yetu katika kupambana na uvuvi huu usiozingatia sheria.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Mwantumu Mzamilu Zodo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa ulize swali lake.

Na. 68

Kuboresha Miundombinu ya Maji Maeneo ya Malisho ya Mifugo – Handeni

MHE. MWANTUMU M. ZODO aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha miundombinu ya maji katika maeneo ya malisho ya mifugo – Handeni.

NAIBU SPIKA: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Mzamilu Zodo Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Tanga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuboresha miundombinu ya maji kwa ajili ya mifugo katika maeneo ya malisho hapa nchini. Hivyo, ili kuhakikisha kuwa miundombinu iliyopo inakuwa endelevu Serikali imeandaa Mwongozo wa Upatikanaji, Usimamizi na Uendelezaji wa Maeneo ya Malisho wa mwaka 2021, ambao umeainisha majukumu ya wadau mbalimbali wakiwemo wataalam katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo huu pia umeelekeza kuundwa kwa kamati za usimamizi wa miundombinu ya maji iliyopo. Aidha, Wizara inaendelea kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Wizara ya Maji ili kuhakikisha kuwa katika miradi yote ya maji inayotekelezwa inazingatia upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo

kwa kuweka makaro ya maji yatakayotumiwa na mifugo. Mipango hii inahusisha pia maeneo ya malisho yaliyopo katika Wilaya ya Handeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea kutoa rai kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwaelimisha wafugaji kutumia fursa ya uwepo wa mitambo ya ujenzi wa mabwawa na uchimbaji wa visima iliyonunuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita kuimarisha huduma ya upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo yote katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwantumu Zodo, swali la nyongeza.

MHE. MWANTUMU M. ZODO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini ninaomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kijiji cha Lengusero, Kata ya Mkindi, Jimbo la Kilindi hakuna miundombinu ya maji kabisa kwa ajili ya mifugo mpaka inapelekea mifugo kufa.

Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kuhakikisha inapeleka miundombinu ya maji maeneo yale kwa ajili ya mifugo? *(Makofi)*

Swali langu la pili, Katika Mkoa wetu wa Tanga, maeneo yenye mifugo mingi ni katika Jimbo la Handeni na Kilindi ambapo hakuna kabisa malisho ya mifugo, hali inayopelekea migogoro ya wafugaji na wakulima.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wanawawezesha wafugaji malisho bora kwa ajili ya kupunguza migogoro katika maeneo haya?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa maswali hayo ya nyongeza.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Katika swali la kwanza Mbunge amehitaji kujua ni hatua gani ambazo tunazichukua kuhakikisha tunakuwa na miundombinu ya maji katika Kijiji cha Lengusero kilichopo Kilindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie hadhara hii kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba tunalo bwawa katika Kijiji cha Kangikwambe ambalo tayari lina maji na linatumika kwa ajili ya kunyweshea mifugo. Kwa vile Kijiji hiki cha Lengusero na cha Kangikwambe viko karibu basi kwa hatua za awali wanaweza wakaendelea kutumia bwawa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, tunaendelea kutoa rai kwa wafugaji wetu kutumia vifaa ambavyo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amevileta katika maeneo yetu ambayo ni mitambo ya ujenzi wa mabwawa na uchimbaji wa visima ambapo ipo katika Mikoa yote nchi nzima kuendelea kutatua changamoto hii kwa utatuzi wa muda mfupi (kuchimba mabwawa na visima). Sisi kama Serikali kadri ya upatikanaji wa fedha, tutaendelea kuchimba mabwawa na kuendeleza vyanzo vya maji kwa ajili ya wafugaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika swali la pili, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara tulitenga fedha takribani shilingi milioni 700 kuanzisha mashamba karibu 100 katika Wilaya 44 na Mikoa 18 nchi nzima. Katika Mkoa wa Tanga, Wilaya ya Handeni na Wilaya ya Kilindi ilipata mashamba haya. Wilaya ya Handeni ilipata mashamba manne yenye ekari 10 kila shamba na Wilaya ya Kilindi ilipata mashamba matatu yenye ekari tano kila shamba ambayo yalikuwa ni mashamba ya malisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwamba baada ya kumalizika kwa mashamba haya, tumeweza kuacha mbegu kwa wazalishaji binafsi ambao wameendeleza kilimo hiki. Sasa, rai yangu ni kwamba wafugaji wetu katika maeneo haya kwanza, waweze kununua mbegu kutoka kwa wazalishaji hawa binafsi ambao wengi

wako tayari kuziuza mbegu hizo na kuzisambaza kwa wafugaji wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili; Wizara tumeendeleza juhudi mbalimbali ambapo Maafisa Ugani wetu wanapoona kwamba kuna mkulima au mfugaji ambaye yuko *serious* na ana eneo, ameli-*clear* ameliandaa kwa ajili ya malisho, basi wanafanya mawasiliano na sisi. Sisi tutaleta mbegu *either* kwa kulingana na mahitaji ya mfugaji husika lakini na utaalamu ili kumsaidia mfugaji kuweza kuzalisha mbegu zake na kuweza kuzitunza kwa ajili ya matumizi ya muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo tu na sisi tunaendelea kadri ya upatikanaji wa fedha, kutenga fedha shilingi 230,000,000 ambazo tumesema tutaanzisha mashamba darasa katika Halmashauri zote nchi nzima kwa ajili ya malisho kuhakikisha kwamba, kila mfugaji anayehitaji mbegu za malisho aweze kuzipata kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Paschal Chinyele, swali la nyongeza.

MHE. PASCHAL I. CHINYELE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia ongezeko kubwa la watu katika Jiji la Dodoma, wafugaji wa Kata za pembezoni zikiwemo za Mbabala, Mpunguzi, Matumbulu, Chigongwe, Ipala, na Kikombo wamejikuta wakikosa maeneo ya malisho kutokana na ongezeko hilo.

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuwapatia miundombinu ya maji pamoja na malisho ili waweze kuendeleza shughuli za ufugaji na kukidhi mahitaji yao ya kila siku?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Pia ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge wa Dodoma Mjini ambaye na yeye kwa nyakati mbalimbali amekuwa akipambana sana kuhakikisha wanachi wake walioko pembezoni wanaweza kupata huduma sahihi za malisho na vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende tu kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba, moja, kama tulivyosema wananchi wake awape elimu. Wale ambao wana uwezo wa kuandaa mashamba waweze kuyaandaa ili waweze kufanya mawasiliano na sisi na tulete utaalamu na mbegu katika mashamba yao ili waweze kuanza kulima moja kwa moja malisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili; kuna hawa ambao tayari ni wazalishaji binafsi, wanazalisha mbegu na wao tayari tuna mawasiliano nao na wako tayari kuwauzia wananchi wetu muda wowote ule, sisi kama Serikali tumetoa ruzuku ya mbegu hizi. Kuna baadhi ya mbegu ambazo zilikuwa zinauzwa shilingi 4,000 kwa kilo, sasa tunatoa kwa shilingi 1,000. Baadhi zilikuwa zinauzwa shilingi 40,000 sasa hivi tunatoa kwa shilingi 20,000. Maana yake tayari tunatengeneza mazingira rafiki ili kila mfugaji anayetaka kuzalisha malisho, aweze kuyazalisha kwa mazingira rafiki lakini kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge, wananchi wake watakapoandaa mashamba, wakiwa tayari awasiliane na sisi ili sisi tutume maafisa wetu waweze kuwaletea elimu, utaalamu na mbegu katika maeneo yao kwa ajili ya kuanza kuzalisha malisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Fadhili Fabian Ngajilo, Mbunge wa Iringa Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 69

Kuhamisha Gereza Kuu – Iringa

MHE. FADHILI F. NGAJILO aliuliza:-

Je, lini Gereza Kuu la Iringa litahamishiwa eneo la Mlolo Kata ya Isakalilo ili kupisha upanuzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Ayoub Mohammed Mahmoud, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Fadhili, kwa ruhusa yako ninaomba nitumie fursa hii kwa vile ni mara ya kwanza kusimama mahali hapa baada ya mabadiliko ya uongozi ndani ya Serikali yetu. Nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kutoa uongozi ndani ya Taifa letu na kuhakikisha kwamba anafanya mabadiliko sahihi katika nyakati sahihi, kwa mahitaji sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, nitumie fursa hii kipekee kabisa kumpongeza Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani na heshima kubwa aliyopewa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kumsaidia katika kazi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi

ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Fadhili Fabian Ngajilo, Mbunge wa Iringa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Jeshi la Magereza inaendelea na hatua mbalimbali za utekelezaji wa mpango wa uhamishaji wa Gereza la Iringa katika eneo la Mlolo, Kata ya Isakalilo. Utekelezaji wa mpango huo umezingatia umuhimu wa huduma zinazotolewa na Hospitali ya Mkoa ya Iringa kwa wananchi, licha ya eneo hilo kuwa karibu sana na gereza, hadi kupelekea wakati mwingine barabara kufungwa kwa sababu za kiusalama na hivyo kuathiri matumizi ya barabara kwa wananchi na hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali ilitenga kiasi cha shilingi 183,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mawili na kufanya jumla ya mabweni kufikia manne. Mabweni hayo yameshajengwa na hivi sasa yapo katika hatua za umaliziaji, sambamba na nyumba 20 zilizojengwa na kukamilika kwa ajili ya Maafisa na Askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutumia fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu, kumuomba Mheshimiwa Mbunge kuwa na subira wakati Serikali ikiendelea na hatua mbalimbali za utafutaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa uhamishaji wa Gereza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ngajilo, swali la nyongeza.

MHE. FADHILI F. NGAJILO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini bado ninapata mashaka na majibu kwa sababu suala hili limeshazungumzwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu miaka ya 1980 tunazungumzia suala la kuhamisha Gereza Kuu la Iringa pale mjini liondolewe liende eneo la Mlolo ambapo Magereza wameshapewa eneo wahamie huko. Sasa, hili Gereza limekuwa ni kero kwenye lile eneo na sisi

tunataka huduma za Hospitali ya Rufaa ziweze kuongezwa na kupanuliwa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, mimi kama Mbunge nikishirikiana pamoja na uongozi wa hospitali, tumeshapata shilingi 600,000,000 kutoka Shirika la Maendeleo Italia la *ASVET Vicenza*. Wametupatia hizo fedha tujenge jengo kubwa la *physiotherapy* kwa ajili ya mazoezi ya viungo, sasa, hatuna eneo la kujenga na Magereza bado wako palepale kwenye lile eneo. *TARURA* wameshaondoka, *TBA* wameondoka, wamebakia Magereza. Sasa, nikuombe Mheshimiwa Waziri uweke sasa tarehe, ni lini wataondoka Magereza pale Iringa Mjini? *(Makofi)*

Swali la pili, ni kuhusu kule Mlolo ambako gereza linahamia. Kule Mlolo kulikuwa na mgogoro wa nyumba 75 kwamba ziko ndani ya eneo la Magereza, lakini mgogoro ule ulishasuluhishwa kilichobakia ni kuhamisha mipaka. Niwaombe sasa Magereza wafanye haraka kuhamisha mipaka ili wananchi wale waweze kupata sasa uhuru wa kuchukua hati zao ili wafurahie maisha yao pale na kupata tabasamu lile la Mheshimiwa Dkt. Samia alilolielezea, waweze kumiliki maeneo yao kwa uhalali. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Fadhili Fabian Ngajilo kwa jinsi ambavyo anawatetea wanachi wake wa Iringa Mjini, hasa kwenye upanuzi wa huduma za afya, vilevile, hamu na shauku aliyonayo ya kuhakikisha kwamba gereza letu hili la pale Iringa Mjini linahama na kwenda pale mahali ambapo limepangwa kuhamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza la lini, nimelijibu kwenye swali mama ingawa sikusema lini. Sikusema lini kwa sababu nilisema tunatafuta fedha ili kusudi tukamilishe ujenzi wa gereza lile ili tuweze kuhamia huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nimkumbushe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunafahamu kwamba hali ya uhitaji wa magereza nchini ni kubwa na hali ya kuhama na umuhimu na haraka tunaiona. Vilevile, hali ya bajeti ndiyo msingi mzima wa kuona lini tutaweza kuhama. Ninatoa mfano tu, kwa sasa bajeti yetu ya maendeleo kwa Jeshi la Magereza ni shilingi 21,000,000,000. Kati ya hizo, shilingi 10,000,000,000 zimeongezwa mwaka huu kwa ajili ya kilimo. Shilingi 11,000,000,000 ndiyo zipo kama maendeleo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna magereza matano tunamalizia hivi sasa katika Mikoa mbalimbali lakini pia tunapaswa kumaliza na gereza hili. Kwa hiyo, nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwenye hili tutajitahidi tuwezavyo na tuko tayari kushirikiana na wao ili kusudi tufanye haraka kuhamisha gereza hili kwa sababu tumeongeza mabweni. Mabweni yanayohitajika ni tisa, tumeshajenga manne, tunaendelea kukamilisha ili tufikie mabweni tisa ili wanafunzi wale waweze kuhamia kule na nyumba zile waweze kuhamia Askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo tutatakiwa tujenge na majengo ya utawala kwenye eneo lile. Kwa hiyo, tunazingatia uhitaji walionao wa sekta ya afya kwenye eneo lile, lakini kadhalika hali ya upatikanaji wa fedha kwa upande wa kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa changamoto ameeleza vizuri, kweli changamoto za eneo lile zimeshapatiwa ufumbuzi tunashukuru sana, lakini na sisi tutaendelea kuongeza bidii ya kukamilisha kazi hiyo kwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Josephine Kapoma, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, Gereza la Kihonda ambalo lipo Manispaa ya Morogoro Mjini ni Gereza ambalo liko katikati ya Mji ambalo limepakana na *SGR* na sasa hivi tuna stendi mpya lakini tuna makazi ya watu.

Je, ni mkakati upi wa Serikali wa kulihamisha Gereza hili ili kuweza kuruhusu mji wa Manispaa ya Morogoro kutanuka? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge wa Morogoro kwa hoja yake ya kuhamisha gereza katika eneo la mji pale Kihonda – Morogoro. Ninataka nimwambie kwamba tayari tumefanya mazungumzo ya awali kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro na tuko kwenye mazungumzo kati ya Magereza na Manispaa ili kuona ni eneo gani linaweza likawa ni mbadala wa kuhamishia gereza hilo na utaratibu ukikamilika tutaweza kukamilisha uhamishaji huo.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Nassoro Rashid Nassoro, Mbunge wa Konde, sasa aulize swali lake.

Na. 70

Maboresho ya Kambi ya JWTZ

MHE. NASSORO RASHID NASSORO aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha Kambi ya JWTZ iliyopo Konde Kiperani yenye miaka zaidi ya 30 bila maboresho yoyote?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ninaomba kumjibu Mheshimiwa Nassoro Rashid Nassoro, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Konde Kiperani ni Kiteule cha 14 Kikosi cha Jeshi, kilichopo Kisiwa cha Pemba. Kiteule hiki kipo Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba. Eneo hili lilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za maafisa na askari waliokuwa wanafanyia kazi 15 Kikosi cha Jeshi kilichokuwa eneo la Makuwe, Wilaya ya Micheweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya ujenzi wa nyumba hizo kuanza katika eneo la Konde, Jeshi lilifanya maamuzi ya kupunguza baadhi ya vikosi kama vile 15 Kikosi cha Jeshi kilikuwa ni moja ya vikosi vilivyopunguzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya 15 Kikosi cha Jeshi kupunguzwa mpango wa ujenzi wa makazi katika eneo hilo ulisitishwa. Kwa sasa wapo askari wachache wanaolinda maeneo hayo dhidi ya uvamizi. Vilevile, eneo hilo linatumika kwa ajili ya mafunzo na mazoezi ya medani kwa 14 Kikosi cha Jeshi. JWTZ inao mpango wa kuyaendeleza maeneo hayo kwani yalitwaliwa kutokana na mkao wake wa kimkakati kwa ulinzi wa kisiwa cha Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nassoro Rashid Nassoro, swali la nyongeza.

MHE. NASSORO RASHID NASSORO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, wakati inaanzishwa kambi hii ilikuwa iko mbali na makazi ya watu lakini leo kambi hii tayari imeshazungukwa na

makazi ya watu, na kwa kuwa wao wamesema wako pale kwa ajili ya kuangalia eneo hili dhidi ya wavamizi.

Je, eneo hili lini watazungushia uzio ili wasije kuingia kwenye migogoro baina yao na wananchi?

Swali la pili, wakati eneo hili linachukuliwa walisema walilichukua kwa ajili ya ulinzi wa Kisiwa cha Pemba na eneo hili liko mpakani na wao bado wanalitumia ka shughuli zao za ulinzi. Je, wakiwa wao ndiyo walinzi wa mipaka, lini wataongeza askari katika eneo hili, hasa wa kikosi cha maji ili kuulinda mpaka huu? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nimshukuru sana Mheshimiwa Nassoro kwa maswali yake mawili ya nyongeza, ambayo kwa kweli nimshukuru na kumpongeza sana kwa jinsi ambavyo anajali usalama wa Taifa letu lakini pia na usalama wa wananchi wake wa Jimbo la Konde, hasa katika eneo lile la Kiperani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu eneo kulizungushia uzio na kuepusha migogoro na wananchi, ninapenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwanza eneo hilo la Jeshi limepimwa na limetolewa hati kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, askari waliopo ni wachache moja ya jukumu lao ni kuhakikisha eneo hilo liko salama na wananchi hawatalivamia kuepusha migogoro baina ya wananchi na Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hilo kuhusu lini tutajenga uzio, Serikali inalichukua jambo hilo na tutajenga uzio kwa kadri ya hali ya upatikanaji wa fedha, eneo litajengwa uzio kuzungushiwa, ikiwa ni sehemu ya pili ya udhibiti wa eneo hilo baada ya ile ya kupata hati na kupimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili la kuongeza askari. Ni kweli, moja ya jukumu la Jeshi la Wananchi wa Tanzania ni ulinzi wa mipaka ya nchi yetu lakini mipaka hii ya nchi yetu iko ya aina tatu, ipo mipaka ya ardhini, iko mipaka ya kwenye maji na iko mipaka ya angani na mipaka yote hiyo katika nyakati zote inalindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nchi yetu ipo salama. Ipo salama na Jeshi la Wananchi wa Tanzania linaendelea kutimiza wajibu wake wa kuhakikisha kwamba Taifa letu liko salama. Kwa upande wa kuimarisha ulinzi kwenye eneo husika, tukiri kwamba tuna zaidi ya vipenyo 1,900 nchi nzima ambavyo baadhi ya raia wa kigeni wanavitumia kuingia nchini kinyume na utaratibu, jambo ambalo linaweza kuleta changamoto ya kiusalama ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kwa kuwa jukumu la Jeshi la Wananchi wa Tanzania ni kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama kuhakikisha kuwa Taifa letu liko salama, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kabla ya kuongeza askari katika eneo hilo, Serikali itahakikisha kwamba Jeshi la Wananchi wa Tanzania linashirikiana na KMKM kwa upande wa Zanzibar, ambao wanafanya kazi katika eneo la maji ya Zanzibar kwa maana ya *territorial water* ili kuhakikisha usalama kwenye eneo hilo unaimarishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, tupo katika hatua za mwisho kwa kushirikiana na Jeshi la Wananchi wa Tanzania na wenzetu wa Uhamiaji kuhakikisha kwamba vipenyo vilivyopo kwenye maeneo hayo vinazidi kuwekewa ofisi na watendaji kwa kufanya doria ili kusudi kuhakikisha kwamba eneo lake la Konde nalo linakuwa kati ya maeneo salama zaidi ndani ya Jamhuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Mheshimiwa Mbunge. Tunaendelea Wizara ya

Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Sasa ni swali la Mheshimiwa Fatma Ally Rembo, Mbunge wa Viti Maalum, litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Mwanahamisi Munkunda.

Na. 71

Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa Wanawake Nchini

MHE. MWANAHAMISI A. MUNKUNDA K.n.y. MHE. FATMA A. REMBO aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia Wanawake Mafunzo ya Kimkakati ya Ufundi Stadi ili kuwawezesha kuibua fursa za kibiashara?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji mbalimbali wa kisekta unaendelea ili kuwapatia wanawake mafunzo ya ufundi stadi na kuwawezesha kuibua fursa za kibiashara na hii ni pamoja na:-

(i) Mradi wa uwezeshaji kupitia ujuzi unaotekelezwa na Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa wasichana wenye umri wa miaka 18 hadi 35 ambapo, hadi Juni 2026, jumla ya wasichana 1,051 wamefikiwa na mradi huo;

(ii) Kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi *(VETA)*, Serikali inaendelea kutoa mafunzo ya vitendo kwa wanawake katika fani mbalimbali, zikiwemo ushonaji, utengenezaji wa bidhaa na matumizi ya teknolojia;

(iii) Utekelezaji wa Programu ya Utambuzi na Urasimishaji Ujuzi ikiwemo Programu ya Mama Samia, inayolenga kutambua na kurasimisha ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa elimu

ambapo, hadi Juni 2026, jumla ya vijana 14,400, sawa na 18% ya lengo, kutoka mikoa 11 walikuwa wamesajiliwa na lengo ni kuwafikia vijana 80,000 ifikapo Juni 2027; na

(iv) Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Ufundi vya Mabughai na Misungwi, vinaendelea kutoa mafunzo katika fani za uhandisi wa ujenzi na maendeleo ya jamii ambapo, katika mwaka wa fedha 2025/2026, jumla ya wanachuo 100,087 walihitimu, wasichana wakiwa 400,096, sawa na 46%.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuongeza fursa za mafunzo haya hasa vijijini ili kuhakikisha walengwa wanawezeshwa kujiajiri, kuanzisha na kukuza biashara, kuongeza kipato na kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na maendeleo ya Taifa. Ninashukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwanahamisi Munkunda, swali la nyongeza.

MHE. MWANAHAMISI A. MUNKUNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na jitihada kubwa ambayo Serikali imefanya, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Fatma Rembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wengi wa vijijini wanashindwa kuyafikia mafunzo haya kutokana na umbali na gharama kubwa ambayo ipo kuyapata mafunzo haya maeneo ya mijini. Kwa mfano, kwa Halmashauri kama ya Ushetu, hakuna Chuo cha Ufundi Stadi wala Chuo cha *VETA*. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha mafunzo maalum ya stadi kwenye maeneo kama hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Pamoja na kazi nzuri tunafahamu kwamba wanawake ndiyo nyenzo muhimu na ndiyo nguzo kubwa ya kuchochea maendeleo kwenye familia. Je, Serikali haioni haja sasa ya kupanga mafunzo maalum kulingana na

mahitaji ya kila Mkoa, kuangalia zile *economic potentials* kwenye kila Mkoa na kuwapatia wanawake ili waweze kujiongezea kipato?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kwa Mkoa wa Iringa, tunategemea kungekuwa na mafunzo maalum ya wanawake kwa kuwajengea uwezo kwenye maeneo ya misitu lakini pia na *Agro-processing*. Kwa upande wa Mkoa wa Shinyanga, tunategemea kuwe kuna mafunzo maalum ambayo yatawajengea uwezo wanawake kwa upande wa uchakataji wa pamba, lakini pia na *processing* ya *mining*. Ninaomba nipate majibu ya Serikali.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninapenda kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Fatma Rembo kwa namna ambavyo anaendelea kuwapigania wanawake wa Mkoa wa Iringa, lakini akisemea kwa mapana zaidi wanawake wa Tanzania. Ninampongeza pia mwakilishi wake, Mheshimiwa Mwanahamisi, kwa namna ambavyo ameweza kuyafikisha maswali vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia swali lake la kwanza wale wanawake walioko vijijini na maeneo ya mbali na mitandao Serikali ina mpango gani? Tayari Serikali inashirikiana na taasisi binafsi, sekta binafsi ambazo zinaweka makongamano mbalimbali na kuwafikia wanawake katika maeneo mbalimbali. Kwa mfano, juzi nilikuwa Arusha na wanawake 100,000, lakini wanawake 100,000 hao wanazunguka Mikoa mbalimbali kulingana na mahitaji kama ambavyo umeuliza kwenye swali lako namba mbili, kila Mkoa kulingana na shughuli za kiuchumi zinazoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali tutaendelea kushirikiana na taasisi za sekta binafsi kuona kwamba tunafika kule kwenye Kata lakini vilevile shughuli mbalimbali zinazowezekana kama utengenezaji wa batiki, lakini ufinyanzi, ususi wa vikapu vizuri ambavyo mwisho wa siku tunaweza tukavipeleka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari tunashirikiana *na Tanzania Women Chamber of Commerce*, hawa wanagusa wanawake wale wa chini. Kwa mfano, kwa pale Mkoa wa Mbeya, tuna timu inayoongozwa na Dada anaitwa Linah na anajiita "Linah Batiki". Yeye tayari amefanikiwa, anakusanya wale wadogo wadogo anawawezesha. Tumeona Mheshimiwa Waziri Dorothy Gwajima, akisisitiza matumizi ya batiki ya watengenezaji wa ndani kwenye sherehe zote za wanawake ule mwezi wa tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tutaendelea kuwafikia kule vijijini kwa kuwashirikisha shughuli zinazowezekana kwenye maeneo yao, wana matete kule wakisuka mikeka mizuri ya kisasa yenye *quality* nzuri, tukawasaidia kuwapelekea wawezeshaji wa *packaging*, *branding*, kuwafanyia *barcodes*. Kwa hiyo, watapata uwezeshaji zaidi wa kuona zile bidhaa zao zinaweza kuingia hata kwenye *supermarkets*, kwenye maduka makubwa na kupelekwa nje ya nchi. Kwa mfano, huyu Linah Batiki, wao sasa hivi wanaelekea Malawi wiki ijayo, kwa hiyo, unaweza ukaona ni wanawake wa chini kabisa lakini pia wanashirikishwa hata kwenye masoko ya nchi na nchi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Maryam Mwinyi, swali la nyongeza.

MHE. MARYAM AZAN MWINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wengi wanashindwa kumudu katika biashara kutokana na uelewa mdogo wa masuala ya kifedha na usimamizi wa biashara. Je, Serikali ina mkakati gani wa kushirikiana na taasisi za kifedha katika kuhakikisha wanawake wanapatiwa elimu ya kifedha na usimamizi wa biashara hasa kule vijijini? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu

swali la nyongeza la Mheshimiwa Maryam Mwinyi. Kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Maryam Mwinyi amekuwa mstari wa mbele sana kufuatilia masuala mazima ya wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara tunafanya kazi kwa karibu sana na taasisi za kifedha ikiwemo mabenki, tayari tuko karibu na benki ya *NMB* ambayo Mheshimiwa Rais ameshaweka fedha zaidi ya shilingi bilioni 18, hizi fedha tunaendelea kukopesha wanawake na kuwasaidia bidhaa zao ziweze kuongezewa thamani, kuwaongezea uwezo, vilevile biashara ziwe na uendelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile wenzetu wa *Azania Bank* wanafanya kazi nzuri sana kwa wanawake, wameweka madirisha ambayo wanawake wanakopeshwa kwa riba ndogo ili kuhakikisha kwamba wanakuwa na biashara zenye uendelevu, yeyote anayekopeshwa, hapewi fedha bila kupatiwa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza elimu ya fedha, elimu ya usimamizi wa fedha, kisha anapatiwa mkopo, anakuwa ameshafanyiwa utafiti wa kutosha na uhakika kwamba ile fedha haiendi kuwa mbegu, inakwenda kuwa endelevu. Kwa hiyo, tutaendelea kushirikiana na wenzetu wa taasisi za fedha kuhakikisha wajasiriamali wadogo wadogo wanawake hasa walioko pembezoni mwa miji wanaweza kufikiwa na huduma hizi muhimu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Joseph Enock Tama, Mbunge wa Kaliua, sasa aulize swali lake.

Na. 72

Maji ya Ziwa Victoria – Kaliua

MHE. JOSEPH E. TAMA aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha mradi wa kutoa maji ya Ziwa Victoria kupeleka Jimbo la Kaliua ili wananchi wanufaike na mradi huo?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Eng*. Kundo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Enock Tama, Mbunge wa Jimbo la Kaliua, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji wa miji 28 kwa kutumia maji ya Ziwa Victoria kutoka Tabora kwenda katika Wilaya za Sikonge, Urambo, na Kaliua, Mkoani Tabora kwa gharama ya zaidi ya shilingi bilioni 143. Miongoni mwa kazi zinazotekelezwa kupitia mradi huo ni pamoja na ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 290.2 sambamba na ujenzi wa matanki matano yenye jumla ya ujazo wa lita milioni nane likiwemo tanki la lita 2,000,000 lililojengwa eneo la Kalemela kwa lengo la kuhudumia wananchi wa Wilaya ya Kaliua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa mradi huo umefikia wastani wa 79% za utekelezaji na tayari umeanza kutoa huduma ya maji katika Mji wa Sikonge wakati ujenzi ukiendelea. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2026 na kunufaisha zaidi ya wananchi 490,926 waishio kwenye Miji ya Sikonge, Urambo na Kaliua, sambamba na Vijiji 63 vya Wilaya hizo tatu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joseph Tama, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH E. TAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nianze kuipongeza Serikali kwa majibu mazuri na hakika, sisi wanakaliua tunaliona tumaini na tabasamu ambalo Wizara hii inaenda kuwatua ndoo wananchi kichwani wa Jimbo la Kaliua. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza. Ni lini sasa wananchi wa Kaliua watapata maji haya kutoka Ziwa Victoria?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa mradi huu unakwenda kuhudumia Kata Nane kati ya 13 na hivyo kuziacha Kata Tano kukosa maji ya Ziwa Victoria. Ni nini mkakati sasa wa Serikali wa kuhakikisha wananchi wote wa Jimbo la Kaliua kutoka kwenye Kata zote 13 wanakwenda kupata maji ya Ziwa Victoria? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge mahiri kabisa kutoka Jimbo la Kaliua, Mheshimiwa Joseph Enock Tama, kwa kazi kubwa ambayo ameianza kwa kasi kubwa sana kuwatetea na kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata maji kutoka Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la msingi, Mheshimiwa Tama, alivyoapishwa tu Bungeni, *message* yake ya kwanza ilikuwa ni kuhusu zile Kata Tano ambazo hazijafikiwa na huu mradi wa Ziwa Victoria, baada ya hapo tulizungumza na kueleweshana lakini kasi yake imeendelea kuonyesha namna gani anapenda wananchi wake wapate maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa msimamo wa Serikali na utaratibu wa Serikali ni kwamba sasa tunaanza kuhakikisha kwamba maeneo ambayo mabomba tayari yameshalazwa wananchi waanze kupata maji. Kwa mfano, tumeanza na Sikonge, tumekamilisha sasa tumeenda Urambo tayari wameshaanza kupata maji katika maeneo mbalimbali, sasa tumeongeza kasi katika eneo la kwenda Kaliua, tuna uhakika kwamba inapofika mwezi Desemba, 2026, wananchi wa Kaliua kwa kauli ya Serikali wataanza kupata maji ya kutoka Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la msingi, ni suala la hizi Kata. Ni kweli kabisa kwamba tuna Kata 13 katika Jimbo la Kaliua kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema, lakini katika mradi huu ambavyo ulikuwa ume-*designed* ni Kata Nane ambazo zinaguswa lakini hamu ya wananchi wa Kaliua katika hizi Kata Tano, kwa sababu kuna miradi midogo midogo ya visima ambayo Mheshimiwa Rais aliwekeza zaidi ya shilingi bilioni saba na kuna mingine inaendelea ya shilingi bilioni 1.2, lakini bado hamu yao ni kutumia maji ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu miradi hiyo haina uhakika sana kwa sababu visima mara nyingine vinakauka, nikutoe hofu kwa Wizara hii inayoongozwa na Mheshimiwa Jumaa Aweso na kwa maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, vijiji hivi ambavyo vitakuwa vimebaki tutafanya usanifu na kuwapelekea maji ya Ziwa Victoria ili na wao wapate huduma ya maji safi na salama. Ninakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joshua Nassari, swali la nyongeza.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kuniona. Ninafikiri hata kabla sijauliza hili swali Mheshimiwa Naibu Waziri na Kaka yangu Mhandisi hapo Mheshimiwa Jumaa Aweso anajua nitauliza swali gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa Meru au Wilaya ya Arumeru, maji sehemu kubwa yanayotumika kwenye Mkoa mzima wa Arusha yanatoka kwenye Wilaya yetu. Kuna maeneo ya ndani ya Jimbo letu ambayo bado watu hawana maji. Ule mradi wa maji wa Kikatiti – Samaria, Mheshimiwa Waziri anajua kwa maana hata wiki iliyopita nimetoka kumsumbua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini ahadi ya Serikali, Mheshimiwa Naibu Waziri, kuhakikisha kwamba ule mradi wa shilingi bilioni nne unakamilika ili wale watu wa Kikatiti mpaka kule Samaria waweze kupata maji safi ya kunywa, wafurahie kuwa pale kwenye ardhi ya

Meru ambayo maji yote yanatoka pale yanakwenda mpaka Monduli na sehemu nyingine. Nini ahadi ya Serikali?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Kaka yangu Mheshimiwa Joshua Nassari, katika mambo ambayo ukipewa kum-*describe* Mheshimiwa Joshua Nassari ni mtu mfuatiliaji sana kwa niaba ya wananchi wake wa Meru. Nikutoe hofu, kazi kubwa tayari imeshaanza kufanywa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba tunayo miradi mingi na ndipo ambapo Mheshimiwa Waziri wakati anasoma bajeti yetu tuliweka mkakati na mkakati wetu siyo kuanzisha miradi mipya, ni kwenda kulipa madeni ya wakandarasi ili kuhakikisha kwamba miradi inayoendelea iweze kukamilika na kutoa matokeo ili sasa wananchi waweze kuona maji yanatoka bombani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimtoe hofu na Serikali tayari tunawashukuru sana Wizara ya Fedha wameanza kutekeleza maelekezo ya Bunge ya kuhakikisha kwamba mgawanyo wa fedha kutoka tozo ya mafuta unakuja moja kwa moja na tayari awamu ya kwanza tumeshapokea na tumeshaanza kuwalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatarajia kwamba katika awamu ijayo tunaenda kuwapatia eneo lako kipaumbele kwa kuhakikisha kwamba wanalipwa na kuhakikisha mradi unaweza kuendelea kwa haraka sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, ninawaona na muda wetu umekwenda sana na kuna hoja za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Waziri, ninakushukuru sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaenda Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa *Eng*. Ramadhani Hamza Singano, Mbunge wa Bumbuli, sasa aulize swali lake.

Na. 73

Kiwanda cha Mponde Kuongezewa Uwezo

MHE. RAMADHANI H. SINGANO aliuliza:-

Je, lini Serikali itaongeza uwezo wa Kiwanda cha Mponde ambacho ni tegemeo katika kukuza uchumi na pato la Halmashauri ya Bumbuli?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dennis Londo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, ninaomba kujibu swali kutoka kwa Mheshimiwa Ramadhani Hamza Singano, Mbunge wa Jimbo la Bumbuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda cha Mponde kinamilikiwa kwa ubia na taasisi mbili za Serikali ambazo ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma *(PSSSF)* na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi *(WCF)*. Kwa sasa kiwanda kinazalisha takribani kilo 7,000 za chai kwa siku na Serikali kupitia wanahisa imeidhinisha mpango mkakati na mpango biashara ambao unalenga kuongeza uzalishaji hadi kufikia kilo 10,000 kwa siku. Utekelezaji wa mpango huo unatarajiwa kufanyika na utagharimu takribani shilingi bilioni 11 ambapo 60% ya fedha hizo zinatarajiwa kutoka kwa wanahisa na 40% kupitia masoko ya mitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii itaongeza uwezo wa uchakataji wa chai, kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza soko la majani ya chai kwa wakulima, kuongeza ajira na kipato kwa wananchi na mchango wa sekta ya chai katika uchumi wa Bumbuli na Mkoa wa Tanga kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Singano, swali la nyongeza.

MHE. RAMADHANI H. SINGANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali ambayo yanawatia moyo wananchi wa Mponde, Bumbuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kukisaidia Kiwanda cha Mponde ambacho kimekutana na changamoto za madeni baada ya kusitishwa miaka tisa, ikiwemo madeni ya wafanyakazi, wakulima na madeni ya umeme?

Swali la pili; Je, ni lini Serikali sasa itarejesha msitu wa Sakale ambao ulikuwa ukitumika kama chanzo cha nishati kwa maana ya miti, kwa kuwa baadaye msitu huu ulitwaliwa au ulichukuliwa na *TR* kwa maana ya Hazina ili kuwezesha kupata nishati kwa bei nafuu? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge atakuwa shahidi kwamba, Serikali inakichukulia kwa umakini sana na kwa uzito kiwanda hiki, ndiyo maana Serikali baada ya kukibinafsisha kiwanda hiki tangu mwaka 2016 kwa maksudi iliamua kukirejesha kwa Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilielekeza taasisi hizi mbili za Serikali *PSSSF* na *WCF* kuwekeza kwenye kiwanda hiki ambapo zaidi ya shilingi bilioni nne taasisi hizi mbili ziliwekeza katika kufufua kiwanda hiki. Hivi tunavyozungumza kiwanda hiki kinaendelea na uzalishaji vizuri, zaidi ya kilo 7,000 zinazalishwa kwa siku na malengo ni kufikia tani 10,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarehe 23 Julai, 2026, mwezi uliopita, katika kikao cha wanahisa, wamekubaliana kwa pamoja mkakati wa miaka mitano ya uzalishaji wa kiwanda hiki, katika makubaliano ambayo wameweka, ambayo kama nilivyotangulia kusema, mpango mkakati na mpango biashara ambao unalenga katika

kuongeza uzalishaji wa kiwanda hiki, wamepitisha zaidi ya shilingi bilioni 11 kwa ajili ya kufufua kiwanda hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, 60% ya fedha hizi zitatoka kwa wanahisa hawa wawili *PSSSF* na *WCF*, na 40% tutapata kupitia masoko ya mitaji. Rai yangu kwa Mheshimiwa Mbunge ambaye pia ni Diwani wa Halmashauri ya Bumbuli, Halmashauri na yenyewe kupitia masoko ya mitaji iwekeze fedha ili iwe mmiliki wa kiwanda hiki, kwa maana wao wakiwekeza maana yake wamiliki pia watakuwa wananchi wa Halmashauri ya Bumbuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutilia umakini sekta ya chai, tunao mkakati wa kufufua kiwanda pale Korogwe cha chai, hivi tunavyozungumza neno la faraja kwa Bunge lako ni kwamba, mitambo imeshawasili, mitambo hii ina uwezo wa kuzalisha kilo 5,000 kwa siku sawa na tani tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji kwenye kiwanda hiki cha chai pale Korogwe utapunguza mzigo wa chai kwenye kiwanda cha Mponde na hivyo kuongeza tija kwa wakulima, lakini pia itapunguza gharama za uzalishaji na hivyo kuongeza tija kwa wakulima wa Korogwe, Bumbuli na Mkoa wa Tanga kwa ujumla. Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa maswali kutoka kwetu na majibu kutoka kwa upande wa Serikali. Naomba nilete matangazo tuliyonayo mezani.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la kwanza ni la wageni walioko Bungeni asubuhi hii. Kwanza kuna mgeni wa Mheshimiwa Naibu Spika, Ndugu Ibrahim Tango ambaye ni Mjasiriamali kutoka Jimbo la Babati Vijijini, Mkoani Manyara. Ahsante, karibu sana rafiki yangu. *(Makofi)*

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika, tunao wageni watano wa Bunge kutoka Bunge la Uganda kama ifuatavyo:-

Tunaye Mheshimiwa Dennis Namara, Mbunge wa Buyaga *West Constituency* ambaye pia ni *Chairperson Committee on East African Community Affairs and former Member of East African Legislative Assembly* ni *leader of delegation,* karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye *Honorable Ngopek Linos, MP*, Kibanda *South County and Vice Chairperson Committee on Défense and Internal Affairs;* Mheshimiwa *Opolot-Okwalinga Simon Peter,* ambaye ni *MP, Kanyum Constituency;* Ms. Adrine Natuku da, ambaye ni *Assistant Director, Department of Legislative Services; na* Mr. John Tamale Mirundi, *Principal Legislative Counsel, Department of Legislative Services.*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni sita wa Mheshimiwa Balozi Khamis Mussa Omar, Waziri wa Fedha ambao ni Wakuu wa Taasisi kutoka Wizarani kama ifuatavyo:-

Tunaye Profesa Eliamani Sedokyeka, Mkuu wa Chuo cha Uhasibu Arusha; Ndugu Charles Malyato, Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria, Chuo cha Uhasibu Arusha; Ndugu Pius P. Hillary, Mwanasheria Mwandamizi, Taasisi ya Kudhibiti Fedha Haramu; na Profesa Hozen Mayaya, Mkuu wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni Prof. Canute Hyandye, Makamu Mkuu wa Chuo, Mipango, Fedha na Utawala; na Wakili Aisha Mjegere, Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini. Karibuni sana hapa Bungeni. *(Makofi)*

Pia wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge nao ni wageni watatu wa Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, ambao ni Ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, ambaye ni mpiga kura wake kutoka Nanyamba, Ndugu Ismaily Liuye, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau, rafiki yake kutoka Kinondoni Jijini Dar es Salaam, Ndugu Hellen Mlay, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Fagason Aron Nkingwa, Ndugu Suzan Zabron ambaye ni mdogo wake kutoka Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Madiwani kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo Mkoani Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima, ambaye ni familia yake kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni Sita wa Mheshimiwa Asha Salum Motto, vijana kutoka Hazina Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 17 wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, ambao ni wanamaombi wa Jijini Dodoma, karibuni sana wanamaombi. *(Makofi)*

Pia wapo wageni 19 wa Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, familia yake kutoka Mkoa wa Ruvuma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tunaye Ndugu Oifrasia Damian Mbuligwe, Mwalimu wa Mstaafu kutoka Wilaya ya Chalinze, Mkoani Pwani, karibu sana. *(Makofi)*

Vile vile wapo wanafunzi 54 na walimu wanne wa Shule ya Sekondari Marangu kutoka Mkoani Kilimanjaro, karibuni sana walimu na wanafunzi wetu hapa Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 97 na walimu nane wa Shule ya Msingi Ritaliza kutoka Holili Mkoani Kilimanjaro, karibuni sana wanafunzi na walimu kwa ajili ya mafunzo. *(Makofi)*

Pia tunao viongozi na washiriki 20 wa Taasisi ya *Anti-Corruption Voices* kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge anawatangazia kuwa kesho, siku ya Jumatano Tarehe 2 Septemba, 2026 kutakuwa na semina itakayoendeshwa na *Kingdom Leadership Network* Tanzania, *World Vision* Tanzania and The Tanzanian *Parliamentary Fellowship* kuhusu *ethical leadership and servant governance, strengthening integrity and accountability in public service*. Semina hiyo itafanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa kuanzia Saa Saba Mchana mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu.

Tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawakumbusha kuwa siku ya Jumanne Tarehe Mosi Septemba, 2026, kutakuwa na semina itakayoendeshwa na Soko la Hisa la Dar es Salaam *(DSE),* kuhusu uwekezaji wa masoko ya mitaji ya umma na huduma zinazotolewa na *DSE*. Semina hiyo itafanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa kuanzia Saa Saba Mchana mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge, Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026, [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill,* 2026]

(Kusomwa Mara ya Pili)

NAIBU SPIKA: Sasa namwita Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Johari Hamza, karibu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano wa Nne wa Bunge na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026, *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill,* 2026).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa umahiri, mafanikio makubwa pamoja na uzalendo. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wenzangu kuendelea kumwombea Mheshimiwa Rais wetu kwa Mwenyezi Mungu amjalie kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia niungane na Wabunge na Watanzania wote kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Deogratius John Louis Pankras Mtemi Ndejembi kwa kuteuliwa, kuthibitishwa na kuapishwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninamtakia kheri katika majukumu yake ya kumsaidia Mheshimiwa Rais kuliongoza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninatoa pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwatumikia wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, ninaishukuru sana Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mwenyekiti Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge, na Makamu wake, Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, pamoja na wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa ushirikiano waliouonesha kwa Serikali wakati wa kuchambua Muswada huu. Kutokana na michango na maoni mazuri yaliyotolewa na Kamati, Serikali imeyazingatia na imeleta jedwali la marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo maoni hayo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Fedha, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Afya, Wizara ya Uchukuzi, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Maliasili na Utalii, na wadau wengine wote kwa ushirikiano walioutoa kwa ofisi yangu katika mchakato mzima wa kushughulikia Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutumia fursa hii kuwapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wakiongozwa na Ndugu Samwel Maneno kwa kujituma na kutekeleza majukumu yao kwa umahiri na weledi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninawashukuru kwa namna ya pekee watumishi wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria chini ya uongozi wa Ndugu Onorius John Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa ushirikiano na msaada mkubwa walionipatia katika hatua mbalimbali za kushughulikia Muswada huu na hivyo kuniwezesha kutekeleza jukumu hili kwa ufanisi na kwa kiwango kinachostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajielekeza katika maudhui ya muswada, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba, marekebisho ya sheria ni miongoni mwa hatua muhimu za Serikali katika kuweka mazingira wezeshi ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Dira hiyo pamoja na mambo mengine inalenga kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani unaoenda sambamba na kuwa na taasisi zenye ufanisi, mazingira bora ya biashara na uwekezaji, uwazi na uwajibikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia azma hiyo, ni muhimu mfumo wetu wa sheria uendelee kuhuishwa ili kuendana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kiteknolojia na kimataifa, kuondoa vikwazo vya utekelezaji na kuimarisha mifumo ya usimamizi na hivyo kuhakikisha kwamba, tunaoanisha sheria hizi na Dira ya Maendeleo 2050.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliowahi kuwa Marais wa Marekani, Woodrow Wilson na Thomas Jefferson waliwahi kusema yafuatayo na ninanukuu, kwa tafsiri isiyo rasmi. Woodrow Wilson alisema: "Sheria inayostawi ni ile inayobadilika kulingana na mabadiliko ya maisha ya jamii yenyewe." Naye Thomas Jefferson aliwahi kusema: "Sheria na taasisi ni lazima ziende mkono kwa mkono na maendeleo ya akili ya mwanadamu. Kadri akili inavyoelimika na kugundua mambo mapya, ndivyo taasisi nazo pamoja na sheria lazima zibadilike ili kwenda na wakati. Hatuwezi kutarajia mtu mzima avae nguo iliyomtosha akiwa mtoto". *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, maboresho yanayopendekezwa na Serikali katika nyakati tofauti yanaendelea kuweka misingi ya kisheria ya kufanikisha mageuzi ya kiuchumi na kitaasisi ambayo pia yanakusudiwa katika Dira yetu ya 2050.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026, *The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill,* 2026 ambao uko mbele ya Bunge lako Tukufu, unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria 21 zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu, Sura ya 423; Sheria ya Nguvu za Atomu, Sura ya 188; Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197; Sheria ya Majina ya Biashara, Sura ya 213; Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80; Sheria ya Kampuni, Sura ya 212; Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20; Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95; Sheria ya Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, Sura ya 174; Sheria ya Chuo cha Uhasibu Arusha, Sura ya 240; Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1; Sheria ya Usimamizi wa Mahakama, Sura ya 237; Sheria ya Baraza la Vijana, Sura ya 441; Sheria ya Usajili wa Hataza, Sura ya 217.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Sheria ya Magereza, Sura ya 58; Sheria ya Usimamizi wa Maabara ya Binafsi za Afya, Sura ya 136; Sheria ya Huduma za Maktaba Tanzania, Sura ya 102; Sheria ya Bodi ya Utalii, Sura ya 364; Sheria ya Utalii, Sura ya 65; Sheria ya Alama za Biashara na Huduma, Sura ya 326 na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, baada ya mashauriano baina ya Kamati na Serikali, ninapendekeza kupitia jedwali la marekebisho kuondolewa kwa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197 na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 kwa kuwa yalishawasilishwa na kushughulikiwa kupitia Muswada wa Fedha wa Mwaka 2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kupitia jedwali la marekebisho, ninapendekeza pia kuondoa marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mahakama, Sura ya 237 na Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa, Sura ya 441 kutokana na uhitaji uliobainika kwa mapendekezo husika kufanyiwa kazi zaidi na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu 22 ambapo Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la Muswada na namna

ambavyo sheria zinazopendekezwa kurekebishwa zimebainishwa katika sehemu zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada, inapendekeza kurekebisha Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu, yaani Sura ya 423 ambapo Kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza fasili za misamiati *Foreign Politically Exposed Persons,* na *Domestic Politically Exposed Persons.*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa ujumla, kwa kuboresha fasili ya misamiati hiyo kwa kadri inavyotumika katika masharti mbalimbali ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza wigo wa fasili ya misamiati hiyo ili kubainisha mazingira ya utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa usambazaji wa silaha za maangamizi yanayohusisha mtu wa ndani ya nchi mwenye wadhifa maalum *(domestic politically exposed person)* na raia wa kigeni mwenye wadhifa maalum *(foreign politically exposed person)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mapendekezo ya marekebisho yanalenga kutoa ufafanuzi sahihi wa misamiati hiyo kama ilivyotumika katika masharti mbalimbali ya sheria. Baada ya mashauriano yaliyofanyika kati ya Serikali na Kamati, ninapendekeza kujumuisha fasili ya misamiati "*higher Risk business relationship", "important political party official*" na "*suspicious transactions*" katika Muswada kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 15 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza muda unaohitajika kuhuisha tathmini ya vihatarishi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwezesha uzingatiaji wa viwango vya Kimataifa kuhusu uhuishaji wa tathmini ya vihatarishi kama inavyotakiwa na Kikosi Kazi cha Kimataifa Dhidi ya Utakatishaji Fedha Haramu *(FATF)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, marekebisho haya yanalenga ushughulikiaji wa wakati wa changamoto zinazojitokeza katika kupambana na utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa usambazaji wa silaha za maangamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 16 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kutofautiana namna ya kufanya uchunguzi wa kina kwa wateja ambao ni watu wa kigeni na wa ndani wenye wadhifa maalumu. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwawezesha watoa taarifa kufanya uchunguzi wa kina kwa wateja kwa ufanisi kulingana na matakwa ya kisheria yaliyoainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 18(a) kinapendekezwa kuongezwa ili kuainisha mazingira ambayo wataalamu walioteuliwa wa biashara isiyo ya kifedha wanapaswa kutoa taarifa ya miamala shuku. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufanisi katika utoaji taarifa wa miamala shuku kwa lengo la kushughulikia changamoto katika kupambana na utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa usambazaji wa silaha za maangamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Serikali kushauriana na Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, ninapendekeza wajibu wa watoa taarifa usihusishe miamala shuku inayohusiana na kesi iliyopo Mahakamani au taarifa inayoweza kuathiri haki ya kutunza siri kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Nguvu za Atomu, Sura ya 188 ambapo aya ya kwanza ya jedwali inapendekezwa kurekebishwa kwa kupunguza idadi ya Wajumbe wa Bodi na aya ya pili inapendekezwa kurekebishwa ili kuweka utaratibu wa kumchagua Makamu Mwenyekiti wa Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kupunguza gharama zinazohusiana na

uendeshaji wa shughuli za bodi, kuimarisha usimamizi wa bodi na kuhakikisha usawa katika uwakilishi wa pande zote za Muungano katika ujumbe wa bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197. Hata hivyo, kama nilivyoeleza awali, ninapendekeza mapendekezo yaliyopo katika sehemu hii yaondolewe kwa kuwa yalikuwa yameshawasilishwa na kushughulikiwa kupitia Muswada wa Fedha wa Mwaka 2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Majina ya Biashara, Sura ya 213. Kifungu cha pili kinapendekeza kurekebishwa kwa kuweka fasili ya msamiati "*designated non-financial business professional*." Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza uelewa wa maana iliyokusudiwa katika masharti mbalimbali ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha Sita kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwajumuisha wataalamu wa biashara wasio wa kifedha kwenye watu wanaotakiwa kutoa taarifa za wamiliki manufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza wigo wa masuala yanayoweza kufanyiwa ufuatiliaji katika kupambana na utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa usambazaji wa silaha za maangamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 21 kinapendekezwa kurekebishwa ili kutoa fursa kwa watoa taarifa kupata taarifa za umiliki manufaa baada ya kuwasilisha maombi kwa msajili. Lengo la marekebisho haya ni kuwawezesha watoa taarifa kuwa na taarifa kamili za umiliki manufaa kwa madhumuni ya kuzuia vitendo vya utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa usambazaji wa silaha za maangamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80. Kifungu cha Pili kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza fasili ya msamiati *"Chief Investigator," "Investigation," "Investigator"* na *"serious incident."* Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kutoa ufafanuzi wa matumizi ya misamiati mbalimbali ambayo imetumika katika sheria ili kuendana na mabadiliko ya sekta ya usafiri wa anga na viwango vya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Serikali kushauriana na Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, ninapendekeza kujumuisha kupitia jedwali la marekebisho fasili ya misamiati *"state level safety reporting system"* na *"voluntary stake level safety reporting system"* ili kuweka ufasaha wa misamiati hiyo iliyotumika katika masharti ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vifungu vya tano na 15 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha maudhui yake kwa dhumuni la kuongeza wigo wa maeneo yanayoweza kutengenezewa kanuni pamoja na kufanya maboresho madogo ya kiuandishi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha utekelezaji wa masharti ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu 15 (a) kinapendekezwa kuongezwa ili kuainisha masharti kuhusu uchunguzi wa ajali za ndege na matukio hatarishi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kubainisha mawanda ya uchunguzi wa ajali za ndege na matukio hatarishi yanayotokea ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 15 (b) kinapendekezwa kuongezwa ili kutambua uwepo wa Kitengo cha Uchunguzi wa Ajali za Ndege kinachojitegemea chini ya Wizara yenye dhamana na masuala ya usafiri wa anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuendana na viwango vya Kimataifa vya

usimamizi wa usafiri wa anga na kukiwezesha kitengo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi katika uchunguzi wa matukio na ajali katika usafiri wa anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 15(c) kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti kuhusu uhuru wa uchunguzi na upatikanaji wa taarifa muhimu zinazohusiana na ajali na matukio katika usafiri wa anga. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufanisi katika uchunguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 15(d) kinapendekezwa kuongezwa kwa lengo la kuzuia utoaji wa taarifa zilizopatikana wakati wa uchunguzi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kulinda taarifa nyeti kuhusu usalama wa usafiri wa anga na kuhamasisha ushirikiano thabiti kwa watu waliohusika katika uchunguzi wa ajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 15(e) kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti yanayohusiana na mgongano wa masilahi kwa wajumbe wa kitengo cha uchunguzi wa ajali na hatua zitakazochukuliwa pale panapotokea ukiukwaji. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kutoruhusu upendeleo, kuimarisha imani ya umma na kuhakikisha kwamba uamuzi haufanyiki kutokana na ushawishi au masilahi binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 33(a) kinapendekezwa kuongezwa kwa kuweka masharti kuhusu utaratibu wa kuzuia ndege ya abiria ikiwa katika anga la Jamhuri ya Muungano. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kulinda usalama wa ndege za abiria zinapokuwa angani na kukidhi mapendekezo ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 37 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuongeza mawanda ya ushirikiano wa Wizara na taasisi nyingine za Serikali kuhusu masuala ya usalama wa usafiri wa anga kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya sheria. Aidha, baada ya Serikali kushauriana na Kamati, ninapendekeza

maboresho katika Kifungu cha 37 kwa kuboresha majukumu ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 38 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka sifa za uteuzi wa Wajumbe wa Bodi wasio watendaji. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha usimamizi wa mamlaka na kuongeza uwajibikaji na uwazi katika uteuzi wa Wajumbe wa Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 45 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kumpa mamlaka Mheshimiwa Rais kumteua Mkurugenzi Mkuu na kuainisha muda wa Mkurugenzi Mkuu kushika madaraka. Kwa sasa sheria haijabainisha muda ambao Mkurugenzi Mkuu anapaswa kushika madaraka. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha utawala bora na kuongeza uwajibikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kifungu cha 73 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha adhabu dhidi ya ukiukwaji wa masharti ya Sheria. Lengo la mapendekezo ya marekebisho ni kuhakikisha kwamba masharti ya sheria yanazingatiwa na kuongeza udhibiti wa utendaji wa makosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Kampuni Sura ya 212 ambapo Sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza fasili za misamiati mipya katika Kifungu cha Pili kwa lengo la kutoa ufafanuzi wa misamiati kama ilivyotumika katika Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa kuanzisha rejesta ya Mkurugenzi Mteule na mwanahisa mteule. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuzingatia matakwa ya *FATF* kuhusu ushughulikiaji wa changamoto katika kupambana na utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa usambazaji wa silaha za maangamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha Nane kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuanzisha sharti la kampuni kubainisha malengo mahsusi ya kampuni katika Katiba ya Kampuni *(MEMARTs)*. Hata hivyo, baada ya Serikali kushauriana na Kamati, ninapendekeza kuondoa mapendekezo ya marekebisho ya kifungu hiki kupitia jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la kuondoa mapendekezo haya ni kuendelea kuruhusu kampuni iliyosajiliwa kufanya biashara yoyote kwa kuzingatia sheria za nchi kutokana na kuwa na utu wa kisheria *(legal personalities)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 15 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuanzisha hitaji la kuzitaka kampuni kuweka wazi taarifa za Mkurugenzi Mteule au Mwanahisa Mteule, kama yupo kwenye kampuni. Lengo la marekebisho haya ni kukuza uwazi kwa kuhakikisha kuwa taarifa zote muhimu kuhusu kampuni zinawasilishwa kwa msajili wakati wa usajili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 33 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kumpa msajili wa kampuni mamlaka, baada ya kuisha kwa muda wa notisi, kufuta kampuni yoyote kwenye rejesta ikiwa kampuni hiyo itashindwa kubadilisha jina ambalo ni sawa na jina la kampuni iliyotangulia kusajiliwa. Hata hivyo, baada ya Serikali kushauriana na Kamati, ninapendekeza kuondoa mapendekezo ya marekebisho ya kifungu hiki kupitia jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo haya yameondolewa kwa kuwa msingi wake umejumuishwa katika marekebisho ya Kifungu cha 404 kupitia jedwali la marekebisho. Lengo ni kuwezesha utaratibu unaotumika chini ya Kifungu cha 404 kutumika iwapo mtu atakaidi amri ya msajili ya kubadili jina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 118 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti yanayoitaka kampuni kuandaa na kutunza daftari la wanahisa wateule. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha uwazi katika kampuni na kuhakikisha kuwa kampuni

zinazingatia masharti yanayowekwa kwa mujibu wa viwango vya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 133 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka masharti yanayozitaka kampuni kuainisha katika taarifa ya kila mwaka idadi ya hisa zilizolipiwa na zisizolipiwa za kila daraja zinazoshikiliwa na kila mwanahisa wa kampuni kwa lengo ambalo taarifa imeandaliwa. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuepuka udanganyifu kuhusu hadhi ya hisa, udanganyifu katika ulipaji wa kodi na kulinda masilahi ya wanahisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 213 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti yanayozitaka kampuni kuweka na kutunza rejesta ya Mkurugenzi Mteule katika ofisi zao za usajili. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha uwazi kwa kuzitaka kampuni kuweka kumbukumbu za Wakurugenzi Wateule na kuhakikisha kuwa zinazingatia masharti yanayowekwa kwa mujibu wa viwango vya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu kipya cha 220(a) kinapendekezwa kuongezwa ili kumpa msajili mamlaka ya kufanya ukaguzi wa kumbukumbu za kampuni, hesabu, na nyaraka nyingine muhimu katika Ofisi ya Usajili ya Kampuni, au mahali pengine ambapo kumbukumbu za kampuni zinahifadhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, baada ya Serikali kushauriana na Kamati, ninapendekeza kurekebisha Kifungu hicho cha 220 kupitia jedwali la marekebisho ili kuongeza sharti la kuruhusu utekelezaji wa kifungu hicho ufanyike kupitia kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia jedwali la marekebisho ninapendekeza kuongeza marekebisho ya Kifungu cha 404 cha Sheria ili kumpa msajili mamlaka ya kufuta kampuni ambayo haijazingatia matakwa ya Kifungu cha 33 kinachotaka kampuni kubadili jina iwapo jina hilo linafanana na kampuni nyingine na imepewa notisi ya kubadili jina na msajili na haijafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 438 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka hitaji kwa kampuni za kigeni kuwasilisha kwa msajili orodha ya wanahisa na taarifa za umiliki manufaa kama ilivyo kwa kampuni za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuzuia kampuni kujihusisha na vitendo vya utakatishaji fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na shughuli haramu za dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 440 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka masharti yanayozitaka kampuni za kigeni kujumuisha katika taarifa ya mwaka mabadiliko yoyote yaliyotokea kwa wanahisa wakati wa kuwasilisha taarifa hiyo kwa msajili. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kumwezesha Msajili kuhuisha rejesta na kuwa na taarifa sahihi wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu kipya cha 456 (a) kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti yanayomtaka msajili kutunza daftari la Wakurugenzi na wanahisa wateule. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha uwazi kwa kuzitaka kampuni kufichua taarifa za Wakurugenzi na wanahisa wateule.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 457 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwawezesha watoa taarifa kupata taarifa za umiliki manufaa baada ya kuwasilisha maombi kwa msajili. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwawezesha watoa taarifa kuwa na taarifa kamili za umiliki manufaa kwa madhumuni ya kudhibiti vitendo vya utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa usambazaji wa silaha za maangamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu kipya cha 468 (a) kinapendekezwa kuongezwa ili kumpa msajili mamlaka ya kutoa maelekezo na miongozo kwa ajili ya utekelezaji bora wa sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha utekelezaji wa masharti ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nane ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura ya 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha Nne kinapendekeza kurekebishwa kwa kuondoa masharti yanayoweka ulazima wa shauri lenye sura ya jinai, madai au utawala chini ya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366 na Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 kushughulikiwa kwanza katika utaratibu wa madai au wa kiutawala kabla ya kuanza taratibu za jinai. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuhakikisha kuwa makosa ya jinai yanayotokana na masuala ya ajira yanashughulikiwa kwa wakati, hivyo kuwezesha upatikanaji wa haki jinai kwa wakati na kuondoa ucheleweshaji na ukosefu wa haki jinai kwa waathirika wa uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tisa ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95 ambapo Kifungu cha Pili kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza wigo wa fasili ya bangi ili kujumuisha majani na mbegu. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kutambua majani na mbegu kuwa bangi, ili kuwezesha utekelezaji wa sheria hususan wakati wa ukamataji, upimaji na uchunguzi wa sampuli au vidhibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 11 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kubainisha kosa la kukutwa na mbegu za mmea wowote uliokatazwa pasipo kujali dhumuni la matumizi ya mbegu husika ikijumuisha uzalishaji wa madawa ya kulevya. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kupanua wigo wa kosa la kumiliki na kusambaza mbegu za mimea iliyokatazwa na sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 12 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kubainisha uwezo wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, kutengeneza kanuni na kutofautisha kanuni zinazoweza kutengenezwa na Waziri. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuondoa mwingiliano wa

utekelezaji wa mamlaka ya kutengeneza kanuni chini ya sheria husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifungu vya 15 na 16 vinapendekezwa kurekebishwa kwa kujumuisha hali za yabisi na kimiminika kwa dawa za kulevya. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kutambua ujazo wa dawa za kulevya katika hali ya kimiminika ambazo awali zilikuwa hazitambuliki katika sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 18 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka bayana kosa la kumiliki dawa za kulevya kinyume na masharti ya kibali. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kutofautisha makosa yanayofanyika chini ya sheria na kosa la umiliki wa dawa za kulevya kinyume na masharti ya kibali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 25 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kukiboresha kimantiki kwa kujumuisha vitendo vilivyokusudiwa kuwa kosa. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuweka bayana vitendo ambavyo vinawezesha kutendeka kwa kosa la kula njama ya kutenda kosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 30 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kujumuisha hali zote za yabisi na kimiminika kwa dawa za kilevi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kutambua ujazo wa dawa za kulevya katika hali ya kimiminika ambazo awali zilikuwa hazitambuliki katika sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 34 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kutanua wigo wa maafisa wanaoweza kutoa amri ya upekuzi kwa kujumuisha afisa mwidhiniwa wa mamlaka. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kurahisisha utekelezaji nyakati ambazo matukio yanayotokea katika maeneo ambayo haiwezekani kumpata Kamishna Jenerali au Mkuu Wa Kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 38 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka sharti la kuainisha nchi ya asili ya dawa za kulevya katika hati ya orodha ya mali wakati wa ukamataji iwapo nchi hiyo inafahamika. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, jedwali la tatu linapendekezwa kurekebishwa kwa kurekebisha vichwa vya habari vya fomu. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kubainisha matumizi sahihi ya fomu husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, Sura ya 174 ambapo sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa ujumla ili kuweka cheo stahiki cha mkuu wa chuo kulingana na matakwa ya *NACTVET*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aya ya kwanza ya jedwali inapendekezwa kurekebishwa ili kupunguza idadi ya Wajumbe wa Baraza. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufanisi wa watendaji na utendaji wa baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi na Moja ya Muswada inapendekezwa kurekebisha Sheria ya Chuo cha Uhasibu Arusha, Sura ya 240 ambapo Sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa ujumla kwa kuweka jina stahiki la baraza la uongozi na mkuu wa taasisi ili kuendana na matakwa ya *NACTVET*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha Nne kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza wigo wa kazi za taasisi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuweka misingi ya kisheria kwa kozi zote zinazotolewa na taasisi na kuongeza ufanisi wa utendaji wa taasisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha Kumi kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kumfanya mkuu wa taasisi kuwa Katibu

wa Baraza la Uongozi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Uongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jedwali la kwanza linapendekezwa kurekebishwa kwa kupunguza idadi na kuweka ukomo wa muda wa uteuzi wa Wajumbe wa Baraza la Uongozi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha usimamizi bora wa Baraza la Uongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi na Mbili ya Muswada inapendekezwa kurekebisha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya Kwanza. Kifungu cha 85 cha Sheria kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza masharti ya kuruhusu sheria ndogo kutengenezwa kwa lugha ya utunzi wa sheria kuu husika. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuoanisha lugha ya sheria ndogo na lugha ya utunzi wa sheria kuu ili kuepuka mkinzano wa maneno au misamiati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi na Tatu ya Muswada inapendekezwa kurekebisha Sheria ya Usimamizi wa Mahakama, Sura ya 237. Hata hivyo, kama nilivyoeleza awali, ninapendekeza kuondolewa kwa mapendekezo ya marekebisho ya sheria hii katika Muswada. Mapendekezo haya yanaondolewa kutokana na kuonekana kwa uhitaji wa kufanyiwa kazi zaidi na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi na Nne ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Baraza la Vijana, Sura ya 441. Hata hivyo, kama nilivyoeleza awali, ninapendekeza kuondolewa kwa mapendekezo ya marekebisho wa sheria hii katika Muswada ili kutoa fursa kwa mapendekezo husika kufanyiwa kazi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi na Tano ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Usajili wa Hataza, Sura ya 217. Kifungu cha pili kinapendekezwa kurekebishwa kwa

kuboresha fasili ya msamiati '*ARIPO office'*. Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi wa fasili hiyo kama ilivyotumika katika sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 13 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumpa Waziri mamlaka ya kuziondoa kwa muda baadhi ya vumbuzi zinazoweza kusajiliwa kama hataza ambazo zinahusu bidhaa na mchakato wa uzalishaji wa bidhaa kutoka kwenye ulinzi wa sheria hii. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza wigo wa mamlaka ya Waziri kwa kuzingatia makubaliano ya Shirika la Biashara Ulimwenguni kuhusu masuala yanayohusiana na biashara ya haki za miliki za ubunifu *(TRIPS Agreement)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Serikali kushauriana na Kamati ninapendekeza kuondoa pendekezo la marekebisho ya kifungu hiki kupitia jedwali la marekebisho. Lengo la kuondoa mapendekezo hayo ni kuendelea kutambua utaratibu uliopo wa kisheria wa kuondolea baadhi ya vumbuzi uwezo wa kusajiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 39 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka muda wa ukomo wa ulinzi wa hataza. Lengo la marekebisho yanayopendekeza ni kuendana na makubaliano ya *TRIPS* ambayo hutoa kiwango cha chini zaidi cha muda wa ulinzi wa hataza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 73 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwianisha na mapendekezo wa marekebisho katika masharti yaliyopo chini ya Sehemu ya Kumi na Saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 74 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza muda wa ulinzi wa hataza ndogo. Lengo la marekebisho haya ni kuchochea uvumbuzi na ubunifu. Aidha, Kifungu cha 76 kinapendekezwa kurekebishwa ili kutoa ulinzi kwa maumbo bunifu yaliyosajiliwa kupitia Sheria za Kikanda na Kimataifa ambapo Tanzania ni mwanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi na Sita ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Magereza, Sura ya 58 ambapo sheria inapendekeza kufanya marekebisho ya jumla kwa kubadilisha majina ya vyeo "*Principal Commissioner*" na "*Commissioner*" na kutumia jina la cheo cha "*Commissioner General*." Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuoanisha sheria na mfumo wa kisheria unaosimamia vyeo ndani ya Jeshi la Magereza Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifungu vya pili na 51 vinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa matumizi ya msamiati '*young prisoner.*' Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuendana na masharti ya Sheria ya Mtoto, Sura ya 13 na kuimarisha ulinzi wa watoto wanaotumikia adhabu ya kifungo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 3A kinapendekezwa kuongezwa kwa madhumuni ya kubainisha majukumu na misingi ya utekelezaji wa majukumu ya Utumishi wa Magereza. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Magereza Tanzania chini ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha Tano kinapendekezwa kurekebishwa kwa kubainisha mamlaka ya Kamishna Jenerali ya uteuzi, upandishaji vyeo, uhamisho na ushushaji vyeo kwa Maafisa wa Magereza. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kubainisha mamlaka hayo ya Mkuu wa Magereza na kuwianisha na mamlaka yaliyopo chini ya sheria nyingine kuhusu utumishi wa Magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 7A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka mfumo wa usimamizi wa Magereza katika ngazi ya mikoa na wilaya. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha uongozi, udhibiti na usimamizi wa Magereza kwa kuzingatia muundo wa kiutawala uliothibitishwa na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mashauriano ya Serikali na Kamati, ninapendekeza marekebisho ya kifungu hiki kupitia jedwali la marekebisho ili kuweka sharti la kumpa Kamishna Mkuu wa Magereza mamlaka ya kuwateua wakuu wa magereza wa wilaya ambao watakuwa chini ya kamandi ya wakuu wao wa Magereza wa mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifungu vya 43, 82, 84, 85, 86, 87, 88, 89, 90, 91, 92, 93 na 94 vinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuhuisha faini na adhabu ili ziendane na masharti ya sheria. Lengo la mapendekezo ya marekebisho ni kuendana na thamani ya fedha za sasa na kuzuia kutendeka kwa makosa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu Kipya cha 62A kinapendekezwa kuongezwa ili kulipa Jeshi la Magereza Tanzania mamlaka ya kuanzisha programu za urekebishaji wa wafungwa ikiwemo elimu, mafunzo ya ufundi, huduma za kiroho, kiutamaduni, shughuli za kimwili na huduma za msaada wa kisaikolojia. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha urekebishaji bora wa wafungwa na kuwawezesha kurejea katika jamii yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 81A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti ya msaada kwa wafungwa baada ya kuachiwa huru ikiwemo usafiri kwenda sehemu zao za makazi pamoja na uunganishaji na taasisi za Serikali na huduma za kijamii. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwezesha urejeaji salama wa wafungwa waliomaliza vifungo vyao katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 105 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kumwezesha Waziri kutengeneza kanuni kuhusiana na urekebishaji bora wa wafungwa na kuwawezesha kurejea katika jamii yao kwa lengo la kuweka utekelezaji bora wa masharti ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi na Saba ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Usimamizi wa Maabara Binafsi za Afya, Sura ya 133, Toleo la 2023 ambapo sheria

inapendekezwa kurekebishwa kwa ujumla kwa kufuta neno "*technologist*" na badala yake kuweka neno "*practitioner.*" Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwianisha sheria hii na Sheria ya Watoa Huduma za Afya, Sura ya 48 ambayo inatumia neno la jumla "*practitioner*" kujumuisha mwanasayansi wa maabara ya afya, Mteknolojia wa Maabara ya Afya na Msaidizi wa Maabara za Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha Tatu kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha fasili ya msamiati '*private health laboratory'* kwa kujumuisha aina mpya za maabara na maeneo ya upimaji. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza wigo wa maabara binafsi ambazo zinaweza kusajiliwa na bodi kwa kuzingatia maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kifungu hicho kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha msamiati '*private health laboratory services'* kwa lengo la kuondoa huduma ambazo kwa sasa zinasimamiwa na Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania zinazohusiana na vifaa vya uchunguzi wa maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kifungu hicho kinapendekezwa kurekebishwa ili kujumuisha tafsiri ya misamiati mipya iliyotumika katika sheria. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kutoa tafsiri iliyokusudiwa ya misamiati hiyo iliyotumika katika sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha Kumi na Mbili kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka rejea sahihi ya sheria inayosimamia wataalam wa maabara ya afya. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kutoa ufafanuzi kuhusiana na sheria husika inayosimamia usajili wa wataalamu wa maabara ya afya. Aidha, kifungu hicho kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza adhabu kwa watu wanaokiuka masharti ya sheria. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuhakikisha adhabu inaendana na ukubwa wa kosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 12A kinapendekezwa kuongezwa kwa kuweka wajibu kwa mtu aliyeidhinishwa kuendesha maabara binafsi kuwa na wajibu wa kusimamia shughuli za kila siku za maabara binafsi ya afya. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuhakikisha uwazi na uwajibikaji wa watu walioidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 13 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza wigo wa utambuzi wa maabara binafsi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwezesha umma kutambua aina mpya za maabara binafsi za afya zilizoongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 14 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka ukomo wa juu na wa chini wa adhabu kwa watu wanaoendesha maabara binafsi bila kusajiliwa au ambao usajili wao umesitishwa. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha adhabu zinazowekwa na sheria zinaendana na uzito wa makosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu Kipya cha 17A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka adhabu ya jumla kwa makosa ambayo adhabu yake haijatajwa katika sheria. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kutoa mwongozo wa adhabu ambayo inaweza kutolewa kwa makosa yaliyotendwa chini ya sheria hiyo pale ambapo sheria haijabainisha adhabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu Kipya cha 17B kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka sharti la kinga kwa Wajumbe wa Bodi, Msajili au wafanyakazi kutowajibishwa binafsi kisheria kwa makosa wanayoyafanya kwa nia njema wakati wa utekelezaji wa majukumu yao. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kumlinda Msajili, Wajumbe wa Bodi na watumishi ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao bila hofu ya kushitakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 18 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kutoa mamlaka kwa Waziri ya kuainisha katika

kanuni majukumu mahsusi na taratibu zinazopaswa kuzingatiwa na watu walioidhinishwa kuendesha maabara binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 21 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kutoa fursa ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa bodi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kutoa haki ya kikatiba ya kukata rufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jedwali linapendekeza kurekebishwa katika aya ya kwanza kwa kupitia upya mfumo wa bodi ili kujumuisha uwakilishi wa kitaalamu wa sekta hiyo na kuwezesha utekelezaji bora wa shughuli za bodi. Vilevile, aya ya 1A inapendekezwa kuongezwa ili kuainisha ukomo wa Wajumbe wa Bodi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha uwajibikaji na utendaji bora wa Wajumbe wa Bodi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, aya ya tisa inapendekezwa kuongezwa ili kuipa bodi mamlaka ya kuanzisha kamati zitakazosaidia katika utekelezaji wa majukumu yake. Aya ya 10 inapendekezwa kuongezwa ili kujumuisha masharti kuhusu mgongano wa kimasilahi kwa Wajumbe. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwezesha uendeshaji bora wa mikutano na kuimarisha ufanisi wa bodi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi na Nane ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Huduma za Maktaba Tanzania, Sura ya 102 ambapo sheria inapendekezwa kufanyiwa marekebisho ya jumla kwa kufuta msamiati "*director*" na badala yake kuweka neno "*Director General*." Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwianisha sheria na muundo wa huduma za maktaba Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha Pili kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha fasili ya msamiati '*book*' na kuongeza misamiati mipya. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kutoa fasili mahsusi ya misamiati kama ilivyotumika katika sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha Nne kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza wigo wa kazi za bodi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza wigo wa kazi za bodi kwa nia ya kuimarisha usimamizi na udhibiti wa huduma za maktaba.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Serikali kushauriana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, ninapendekeza marekebisho ya kifungu hiki kupitia jedwali la marekebisho ili kuipa bodi mamlaka ya kuhakikisha kuwa vitabu na machapisho yanayotunzwa katika maktaba ni yale yanayokuza maadili ya Kitaifa, mila na desturi na yasiyokuwa na maudhui yanayokiuka maadili hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha Tano kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha adhabu kwa ukiukwaji wa kifungu hiki. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwianisha adhabu na hali halisi ya sasa ya kiuchumi. Aidha, marekebisho yanakusudia kuzuia ukiukwaji wa masharti ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 13 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kujumuisha vyanzo vingine vya mapato ya bodi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza wigo wa vyanzo vya mapato ya bodi kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 14 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza kiwango cha fedha kinachoweza kuhamishwa kutoka kwenye bajeti iliyotengwa kutoka shilingi 50,000 hadi shilingi milioni 50. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuendana na mabadiliko ya thamani ya fedha ili kuhakikisha utekelezaji wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, jedwali linapendekezwa kurekebishwa kwa kubainisha Wajumbe wa Bodi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufanisi wa bodi katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya 19 ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania, Sura ya 364 ambapo sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa ujumla kwa kuweka cheo stahiki cha Mtendaji Mkuu wa Bodi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwianisha cheo hicho na muundo wa sasa wa Bodi ya Utalii Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha Pili kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza fasili ya misamiati mipya kwa lengo la kutoa fasili ya misamiati hiyo kama ilivyokusudiwa kutumika katika sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha Tano cha sheria kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza majukumu ya bodi yanayohusiana na vifaa na shughuli za utalii. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufanisi katika kusimamia shughuli za utalii. Jedwali linapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha muundo wa bodi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufanisi wa bodi katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Serikali kushauriana na Kamati, ninapendekeza marekebisho ya aya (g) ya jedwali la sheria kupitia jedwali la marekebisho ili kuongeza wawakilishi kutoka Shirikisho la Utalii Tanzania kuwa sehemu ya Wajumbe wa Bodi ya Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Ishirini ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Utalii, Sura ya 65 ambapo sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta rejea ya "*director*" katika vifungu mbalimbali na badala yake kuweka rejea ya "*Director General*" ili kuhamisha majukumu ya kiutendaji ya kusimamia shughuli za utalii kutoka kwa Mkurugenzi wa Utalii kwenda Bodi ya Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha ufanisi katika kusimamia shughuli za utalii kwa kuwa majukumu hayo ya kiutendaji yatatekelezwa na

Bodi ya Utalii na Wizara itabaki na jukumu la usimamizi wa ujumla na majukumu ya kisera.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha Pili kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa kuongeza fasili ya msamiati "Director *General*" ili kuweka ufafanuzi wa msamiati huo kama ulivyotumika katika masharti mbalimbali ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha Nne kinapendekezwa kurekebishwa ili kufafanua mamlaka ya kamati ya kitaalamu ya ushauri. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kubainisha jukumu la ushauri la kamati katika masuala mbalimbali yaliyo chini ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha Sita kinapendekezwa kurekebishwa kwa madhumuni ya kuhamisha majukumu yote ya kiutendaji yanayohusiana na usimamizi wa shughuli za utalii kutoka kwa Mkurugenzi wa Utalii. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha ufanisi katika kusimamia shughuli za utalii kwa kuwa majukumu hayo ya kiutendaji yatatekelezwa na Bodi ya Utalii, na Wizara itabaki na jukumu la usimamizi wa jumla wa majukumu ya kisera.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 13 na 34 vinapendekezwa kurekebishwa kwa kutoa sharti la kuchapisha katika Gazeti la Serikali orodha ya vivutio vilivyosajiliwa au vilivyopangiwa madaraja, shughuli za utalii na waendeshaji wa utalii. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kurahisisha utaratibu wa kuchapisha taarifa zinazohusiana na vituo vya utalii, shughuli za waendeshaji wa utalii na kurahisisha upatikanaji wa taarifa za utalii kwa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 14 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa sharti la kulipa ada za upangaji wa madaraja zinazolipwa na waendeshaji wa vituo vya utalii. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwahimiza waendeshaji wa

utalii kupandisha madaraja vituo vyao vya utalii na kuboresha huduma za utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 16 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa jukumu la Waziri katika kufuta usajili wa vituo vya utalii au shughuli za utalii. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwezesha utekelezaji bora wa majukumu ya kiutendaji ya Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 17 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kumpa Mkurugenzi Mkuu wajibu wa kupendekeza vituo au shughuli kwa ajili ya kutangazwa na Waziri kama vituo au shughuli za utalii. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kutambua mamlaka ya kiutendaji yaliyowekwa kwa Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 36 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kubainisha muda halali wa leseni kuwa miezi 12 kuanzia tarehe ya kutolewa kwake. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuondoa utata na kuweka bayana usahihi wa kisheria, hivyo kurahisisha usimamizi wa shughuli za kitalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 42 kinapendekezwa kurekebishwa, na Kifungu cha 43 kinapendekezwa kufutwa kwa kuondoa masharti ya vigezo na taratibu za usajili wa waongoza utalii. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuboresha usimamizi wa waongoza utalii ili kukuza sekta ya utalii na ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vifungu vya 50 na 53 vinapendekezwa kurekebishwa kwa kujumuisha Mkurugenzi Mkuu katika masharti ya vifungu hivyo. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha masharti hayo na mapendekezo ya kumpa Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Utalii majukumu ya kiutendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jedwali la kwanza la Sheria linapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha muundo wa kamati

ya ushauri wa wataalam na kupunguza idadi ya mikutano ya lazima ya kamati kutoka minne hadi miwili kwa mwaka. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa kazi za kamati na kupunguza gharama za uendeshaji wa kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mashauriano na kamati, ninapendekeza marekebisho ya muundo wa kamati ya ushauri ya wataalam kupitia jedwali la marekebisho ili kuongeza wawakilishi kutoka sekta binafsi kuwa miongoni mwa Wajumbe wa Kamati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya 21 ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Alama za Biashara na Huduma Sura 326, ambapo Kifungu cha Pili kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha fasili ya misamiati iliyotumika katika sheria na kuweka fasili mpya ya misamiati iliyotumika kwenye sheria. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kutoa ufafanuzi wa masharti katika sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vifungu vipya vya 16(A) na 16(B) vinapendekezwa kuongezwa kwa ajili ya kutoa ulinzi wa alama za pamoja na usajili wa alama za uthibitisho. Lengo la marekebisho haya ni kuweka ulinzi wa alama za pamoja kwa njia ya usajili na kushughulikia usajili wa alama za uthibitisho ambazo baada ya usajili zitaweza kulindwa chini ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 19(A) kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti kuhusu ulinzi wa alama ya biashara inayojulikana kwa mujibu wa mikataba ya kikanda au Kimataifa iliyoridhiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lengo la marekebisho haya ni kuweka ulinzi wa alama hizo za biashara chini ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 26 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumpa msajili mamlaka ya kutangaza maombi ya usajili wa alama kabla ya kuyakubali. Lengo la marekebisho haya ni kutoa fursa kwa umma kutoa maoni yao kuhusiana na maombi

yaliyowasilishwa pale ambapo msajili anaona kuwa kuna mazingira ya kipekee ya kufanya hivyo kabla ya kukubali maombi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 28(A) kinapendekezwa kuongezwa ili kutambua alama za biashara na huduma zilizosajiliwa na Shirika la Miliki Bunifu Kanda ya Afrika, ikibainisha Tanzania kama nchi teule kabla ya kuanza kutumika kwa Itifaki ya *Banjul* katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania *(Banjul Protocol)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha ulinzi wa alama za biashara na huduma zinazotambuliwa chini ya Itifaki ya *Banjul* ambayo nchi yetu imetia saini na kuridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya 22 ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura 148. Hata hivyo, kama nilivyoeleza awali, ninapendekeza kuondolewa kwa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria hii katika Muswada kwa kuwa marekebisho husika yaliwasilishwa na kushughulikiwa katika Muswada wa Fedha wa Mwaka 2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa utawala wa sheria katika maendeleo ya Taifa ulielezwa vyema na hayati Askofu Desmond Tutu aliposema kwamba, *"Strengthening the rule of law is an essential ingredient to enhance justice, peace and economic and social progress."* Yaani, kuimarisha utawala wa sheria ni nguzo muhimu katika kuendeleza haki, amani pamoja na maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli hii inatukumbusha kwamba, utawala wa sheria ni msingi muhimu wa kujenga jamii yenye haki, taasisi zinazowajibika na mazingira yenye utulivu yanayowezesha shughuli za kijamii na kiuchumi kustawi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kauli hii inaendana na mwelekeo wa Dira yetu ya Taifa ya Maendeleo 2050 ambayo utekelezaji wake unahitaji uwepo wa taasisi madhubuti, uwajibikaji

na mazingira ya kisheria yanayowezesha shughuli za kijamii na kiuchumi kufanyika kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, kuendelea kuimarisha utawala wa sheria ni sehemu muhimu au ni nguzo muhimu ya kuweka misingi ya kufikia malengo ya maendeleo yaliyowekwa katika Dira ya 2050.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo marefu, na kwa mara nyingine tena, ninaomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026, *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill 2026]* na kuupitisha pamoja na marekebisho yake katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na Mara ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima, ninaomba kutoa hoja.

MAELEZO YA MHESHIMIWA HAMZA S. JOHARI (MB), MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AKIWASILISHA MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI WA MWAKA 2026 (THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) BILL, 2026) KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema; na kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano wa Nne wa Bunge, na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2026).

Mheshimiwa Spika, Naomba kutumia fursa hii kumpongeza kwa dhati **Mhe. *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano**

wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza Nchi yetu kwa umahiri, mafanikio makubwa na uzalendo. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wenzangu kuendelea kumuombea Rais wetu kwa Mwenyezi Mungu amjalie kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Napenda pia niungane na Wabunge na Watanzania wote kutoa pongezi kwa Mhe. Deogratius John Ndejembi, kwa kuteuliwa, kuthibitishwa na kuapishwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninamtakia heri katika majukumu yake ya kumsaidia Mhe. Rais kuliongoza Taifa letu. Aidha, ninatoa pongezi kwa Mhe. *Dkt.* Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwatumikia wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Nitumie fursa hii pia kukupongeza wewe mwenyewe, kumpongeza Mhe. Naibu Spika na kuwapongeza Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha vikao na mijadala ndani ya Bunge kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria, ikiwa ni pamoja na kuboresha na Sheria zilizopo ili kuendana na mahitaji na mwelekeo wa Nchi.

Mheshimiwa Spika, Kwa namna ya pekee niishukuru sana Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mwenyekiti, **Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro** (Mb.) na Makamu wake **Mhe. Edwin Enosy Swalle (Mb.)** pamoja na Wajumbe wa Kamati hiyo kwa ushirikiano walioonesha kwa Serikali wakati wa kuchambua Muswada huu.

Kutokana na michango na maoni mazuri yaliyotolewa na Kamati, Serikali imeyazingatia na imeleta Jedwali la Marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo maoni hayo muhimu.

Mheshimiwa Spika, Ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Fedha, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Afya, Wizara ya Uchukuzi, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Maliasili na Utalii na wadau wengine wote kwa ushirikiano waliotoa kwa Ofisi yangu katika mchakato mzima wa kushughulikia Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wakiongozwa na Ndg. Samwel Maneno, kwa kujituma na kutekeleza majukumu yao kwa umahiri na weledi. Aidha, ninawashukuru kwa namna ya pekee watumishi wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria, chini ya uongozi wa Ndg. Onorius John Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria, kwa ushirikiano na msaada mkubwa walionipatia katika hatua mbalimbali za kushughulikia Muswada huu, na hivyo kuniwezesha kutekeleza jukumu hili kwa ufanisi na kwa kiwango kinachostahili.

Mheshimiwa Spika, kabla sijajielekeza katika maudhui ya Muswada, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba marekebisho ya sheria ni miongoni mwa hatua muhimu za Serikali katika kuweka mazingira wezeshi ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Dira hiyo inalenga, pamoja na mambo mengine, kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani unaoenda sambamba na kuwa na taasisi zenye ufanisi, mazingira bora ya biashara na uwekezaji, uwazi na uwajibikaji. Ili kufikia azma hiyo, ni muhimu mfumo wa sheria uendelee kuhuishwa ili kuendana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kiteknolojia na kimataifa, kuondoa vikwazo vya utekelezaji na kuimarisha mifumo ya usimamizi.

Mheshimiwa Spika, waliowahi kuwa Marais wa Marekani, Woodrow Wilson na Thomas Jefferson waliwahi kusema yafuatayo, ninanukuu kwa tafsiri isiyo rasmi:
Woodrow Wilson; *'Sheria inayostawi ni ile inayobadilika kulingana na mabadiliko ya maisha ya jamii yenyewe'*
Thomas Jefferson; *'Sheria na taasisi ni lazima ziende mkono kwa mkono na maendeleo ya akili ya mwanadamu. Kadri akili*

inavyoelimika na kugundua mambo mapya, ndivyo taasisi nazo lazima zibadilike ili kwenda na wakati. Hatuwezi kutarajia mtu mzima avae nguo iliyomtosha akiwa mtoto'.

Hivyo, maboresho yanayopendekezwa na Serikali katika nyakati tofauti yanaendelea kuweka msingi wa kisheria wa kufanikisha mageuzi ya kiuchumi na kitaasisi ambayo pia yanakusudiwa katika Dira 2050.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2026) ambao uko mbele ya Bunge lako Tukufu, unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Ishirini na Moja zifuatazo:

(a) Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu, Sura ya 423;
(b) Sheria ya Nguvu za Atomu, Sura ya 188;
(c) Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197;
(d) Sheria ya Majina ya Biashara, Sura ya 213;
(e) Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80;
(f) Sheria ya Kampuni, Sura ya 212;
(g) Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20;
(h) Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95;
(i) Sheria ya Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, Sura ya 174;
(j) Sheria ya Chuo cha Uhasibu Arusha, Sura ya 240;
(k) Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1;
(l) Sheria ya Usimamizi wa Mahakama, Sura ya 237;
(m) Sheria ya Baraza la Vijana, Sura ya 441;
(n) Sheria ya Usajili wa Hataza, Sura ya 217;
(o) Sheria ya Magereza, Sura ya 58;
(p) Sheria ya Usimamizi wa Maabara Binafsi za Afya, Sura ya 136;
(q) Sheria ya Huduma za Maktaba Tanzania, Sura ya 102;
(r) Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania, Sura ya 364;

(s) Sheria ya Utalii, Sura ya 65;
(t) Sheria ya Alama za Biashara na Huduma, Sura ya 326; na
(u) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba baada ya mashauriano baina ya Kamati na Serikali, napendekeza kupitia Jedwali la Marekebisho kuondolewa kwa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197 na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 kwa kuwa yaliwasilishwa na kushughulikiwa kupitia Muswada wa Fedha wa mwaka 2026. Vile vile kupitia Jedwali la Marekebisho, ninapendekeza pia kuondoa marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mahakama, Sura ya 237 na Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa, Sura ya 441 kutokana na uhitaji uliobainika wa mapendekezo husika kufanyiwa kazi zaidi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Ishirini na Mbili ambapo Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi ambayo yanajumuisha jina la Muswada na namna ambavyo Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa zimebainishwa katika Sehemu zake.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu, Sura ya 423 ambapo kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza fasili za misamiati "foreign politically exposed persons" na "domestic politically exposed persons". Aidha, Sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa ujumla kwa kuboresha fasili ya misamiati hiyo kwa kadiri inavyotumika katika masharti mbalimbali ya Sheria. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza wigo wa fasili ya misamiati hiyo ili kubainisha mazingira ya utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa usambazaji wa silaha za maangamizi yanayohusisha mtu wa ndani ya nchi mwenye wadhifa maalumu (domestic politically exposed person) na raia wa kigeni mwenye wadhifa maalumu (foreign politically exposed person). Aidha, mapendekezo ya marekebisho

yanalenga kutoa ufafanuzi sahihi wa misamiati hiyo kama ilivyotumika katika masharti mbalimbali ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, baada ya mashauriano yaliyofanyika kati ya Serikali na Kamati, napendekeza kujumuisha fasili ya misamiati "*higher risk business relationship*", "important political party official", na "suscipious transactions" katika Muswada kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 15 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza muda unaohitajika kuhuisha tathmini ya vihatarishi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwezesha uzingatiaji wa viwango vya kimataifa kuhusu uhuishaji wa tathmini ya vihatarishi kama inavyotakiwa na Kikosi Kazi cha Kimatifa Dhidi ya Utakatishaji Fedha Haramu (FATF). Aidha marekebisho haya yanalenga kuwezesha ushughulikiaji wa wakati wa changamoto zinazojitokeza katika kupambana na utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa usambazaji wa silaha za maangamizi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 16 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kutofautisha namna ya kufanya uchunguzi wa kina kwa wateja ambao ni watu wa kigeni na wa ndani wenye wadhifa maalumu. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwawezesha watoa taarifa kufanya uchunguzi wa kina kwa wateja kwa ufanisi kulingana na matakwa ya kisheria yaliyoainishwa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 18A kinapendekezwa kuongezwa ili kuainisha mazingira ambayo wataalamu walioteuliwa wa biashara isiyo ya kifedha wanapaswa kutoa taarifa kuhusu miamala shuku. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufanisi katika utoaji taarifa kuhusu miamala shuku lengo la kushughulikia changamoto zilizobainika katika kupambana na utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa usambazaji wa silaha za maangamizi.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kushauriana na Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, napendekeza wajibu wa watoa taarifa

usihusishe miamala shuku inayohusiana na kesi iliyopo mahakamani au taarifa inayoweza kuathiri haki ya kutunza siri kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Nguvu za Atomu, Sura ya 188. Ambapo aya ya 1 ya Jedwali inapendekezwa kurekebishwa kwa kupunguza idadi ya wajumbe wa Bodi na aya ya 2 inapendekezwa kurekebishwa ili kuweka utaratibu wa kumchagua Makamu Mwenyekiti wa Bodi.

Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kupunguza gharama zinazohusiana na uendeshaji wa shughuli za Bodi, kuimarisha usimamizi wa Bodi na kuhakikisha usawa katika uwakilishi wa pande zote za Muungano katika ujumbe wa Bodi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197. Hata hivyo, kama nilivyoeleza awali, napendekeza mapendekezo yaliyopo katika Sehemu hii yaondolewe kwa kuwa yalikuwa yamekwishawasilishwa na kushughulikiwa kupitia Muswada wa Fedha wa mwaka 2026.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Majina ya Biashara, Sura ya 213. Kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka fasili ya msamiati "designated non-financial business professional". Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza uelewa wa maana iliyokusudiwa katika masharti mbalimbali ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 6 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwajumuisha wataalamu wasio katika biashara ya kifedha miongoni mwa watu wanaopaswa kutoa taarifa za wamiliki manufaa. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza wigo wa masuala yanayoweza kufanyiwa ufuatiliaji katika kupambana na utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa usambazaji wa silaha za maangamizi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 21 kinapendekezwa kurekebishwa ili kutoa fursa kwa watoa taarifa kupata taarifa za umiliki manufaa baada ya kuwasilisha maombi kwa Msajili. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwawezesha watoa taarifa kuwa na taarifa kamili za umiliki manufaa kwa madhumuni ya kuzuia vitendo vya utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa usambazaji wa silaha za maangamizi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80. Kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza fasili ya misamiati "*Chief Investigator*", "*investigation*", "*investigator*" *na* "*serious incident*". Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kutoa ufafanuzi wa matumizi ya misamiati mbalimbali ambayo imetumika katika Sheria ili kuendana na mabadiliko ya sekta ya usafiri wa anga na viwango vya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kushauriana na Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, napendekeza kujumuisha, kupitia Jedwali la Marekebisho, fasili ya misamiati "State-level safety reporting system" na "voluntary State-level safety reporting system" ili kuweka ufasaha wa misamiati hiyo iliyotumika katika masharti ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, Vifungu vya 5 na 15 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha maudhui yake kwa dhumuni la kuongeza wigo wa maeneo yanayoweza kutengenezewa Kanuni pamoja na kufanya maboresho madogo ya kiuandishi. Lengo la marekebisho yaliyopendekezwa ni kuimarisha utekelezaji wa masharti ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 15A kinapendekezwa kuongezwa ili kuainisha masharti kuhusu uchunguzi wa ajali za ndege na matukio hatarishi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kubainisha mawanda ya uchunguzi wa ajali za ndege na matukio hatarishi yanayotokea ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 15B kinapendekezwa kuongezwa ili kutambua uwepo wa Kitengo cha Uchunguzi wa Ajali za Ndege

kinachojitegemea chini ya Wizara yenye dhamana na masuala ya usafiri wa anga.

Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuendana na viwango vya kimataifa vya usimamizi wa usafiri wa anga na kukiwezesha Kitengo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi katika uchunguzi wa matukio na ajali katika usafiri wa anga.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 15C kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti kuhusu uhuru wa uchunguzi na upatikanaji wa taarifa muhimu zinazohusu ajali na matukio katika usafiri wa anga. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufanisi katika kufanya uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 15D kinapendekezwa kuongezwa kwa lengo la kuzuia utoaji wa taarifa zilizopatikana wakati wa uchunguzi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kulinda taarifa nyeti kuhusu usalama wa usafiri wa anga na kuhamasisha ushirikiano thabiti kwa watu waliohusika katika uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 15E kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti yanayohusiana na mgongano wa maslahi kwa wajumbe wa Kitengo cha Uchunguzi wa Ajali na hatua zitakazochukuliwa pale panapotokea ukiukwaji. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kutoruhusu upendeleo, kuimarisha imani ya umma na kuhakikisha kwamba uamuzi haufanyiki kutokana na ushawishi wa maslahi binafsi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 33A kinapendekezwa kuongezwa kwa kuweka masharti kuhusu utaratibu wa kuzuia ndege ya abiria ikiwa katika anga la Jamhuri ya Muungano. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kulinda usalama wa ndege za abiria zinapokuwa angani na kukidhi mapendekezo ya kimataifa. Kifungu cha 37 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuongeza mawanda ya ushirikiano na wizara na taasisi nyingine za Serikali kuhusu masuala ya usalama wa usafiri wa anga kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya Sheria. Aidha, baada ya Serikali

kushauriana na Kamati, napendekeza maboresho katika kifungu cha 37 kwa kuboresha majukumu ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 38 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka sifa za uteuzi wa wajumbe wa Bodi wasio watendaji. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha usimamizi wa Mamlaka na kuongeza uwajibikaji na uwazi katika uteuzi wa wajumbe wa Bodi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 45 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kumpa mamlaka Rais kumteua Mkurugenzi Mkuu na kuainisha muda wa Mkurugenzi Mkuu kushika madaraka. Kwa sasa Sheria haijabainisha muda ambao Mkurugenzi Mkuu anapaswa kushika madaraka. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha utawala bora na kuongeza uwajibikaji.

Aidha, kifungu cha 73 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha adhabu dhidi ya ukiukwaji wa masharti ya Sheria. Lengo la mapendekezo ya marekebisho ni kuhakikisha kwamba masharti ya Sheria yanazingatiwa na kuongeza udhibiti wa utendekaji wa makosa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Kampuni, Sura ya 212 ambapo Sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza fasili za misamiati mipya katika kifungu cha 2 kwa lengo la kutoa ufafanuzi wa misamiati kama ilivyotumika katika Sheria. Vilevile, Sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa kuanzisha rejesta ya mkurugenzi mteule na mwanahisa mteule. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuzingatia matakwa ya FATF kuhusu ushughulikiaji wa changamoto katika kupambana na utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa usambazaji wa silaha za maangamizi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 8 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuanzisha sharti la kampuni kubainisha malengo mahsusi ya kampuni katika katiba ya kampuni (MEMARTs). Hata hivyo, baada

ya Serikali kushauriana na Kamati, napendekeza kuondoa mapendekezo ya marekebisho ya kifungu hiki kupitia Jedwali la Marekebisho. Lengo la kuondoa mapendekezo haya ni kuendelea kuruhusu kampuni iliyosajiliwa kufanya biashara yoyote kwa kuzingatia sheria za nchi kutokana na kuwa na utu wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 15 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuanzisha hitaji la kuzitaka kampuni kuweka wazi taarifa za mkurugenzi mteule au mwanahisa mteule, kama yupo kwenye kampuni. Lengo la marekebisho haya ni kukuza uwazi kwa kuhakikisha kuwa taarifa zote muhimu kuhusu kampuni zinawasilishwa kwa Msajili wakati wa usajili.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 33 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kumpa Msajili wa Kampuni mamlaka, baada ya kuisha kwa muda wa notisi, kufuta kampuni yoyote kwenye rejesta ikiwa kampuni hiyo itashindwa kubadilisha jina ambalo ni sawa na jina la kampuni iliyotangulia kusajiliwa. Hata hivyo, baada ya Serikali kushauriana na Kamati, napendekeza kuondoa mapendekezo ya marekebisho ya kifungu hiki kupitia Jedwali la Marekebisho. Mapendekezo haya yameondolewa kwa kuwa msingi wake umejumuishwa katika marekebisho ya kifungu cha 404 kupitia Jedwali la Marekebisho. Lengo ni kuwezesha utaratibu unaotumika chini ya kifungu cha 404 kutumika iwapo mtu atakaidi amri ya Msajili ya kubadili jina.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 118 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti yanayoitaka kampuni kuandaa na kutunza daftari la wanahisa wateule. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha uwazi katika kampuni na kuhakikisha kuwa kampuni zinazingatia masharti yanayowekwa kwa mujibu wa viwango vya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 133 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka masharti yanayozitaka kampuni kuainisha katika taarifa ya kila mwaka idadi ya hisa zilizolipiwa na zisizolipiwa za kila daraja zinazoshikiliwa na kila mwanahisa wa kampuni kwa tarehe ambayo

taarifa imeandaliwa. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuepuka udanganyifu kuhusu hadhi ya hisa, udanganyifu katika ulipaji wa kodi na kulinda maslahi ya wanahisa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 213 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti yanayozitaka kampuni kuweka na kutunza rejesta ya mkurugenzi mteule katika ofisi zao za usajili. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha uwazi kwa kuzitaka kampuni kuweka kumbukumbu za wakurugenzi wateule na kuhakikisha kuwa zinazingatia masharti yanayowekwa kwa mujibu wa viwango vya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu kipya cha 220A kinapendekezwa kuongezwa ili kumpa Msajili mamlaka ya kufanya ukaguzi wa kumbukumbu za kampuni, hesabu, na nyaraka nyingine muhimu katika ofisi ya usajili ya kampuni, au mahali pengine ambapo kumbukumbu za kampuni zinahifadhiwa. Aidha, baada ya Serikali kushauriana na Kamati, napendekeza kurekebisha kifungu hicho cha 220A kupitia Jedwali la Marekebisho ili kuongeza sharti la kuruhusu utekelezaji wa kifungu hicho ufanyike kupitia kanuni.

Mheshimiwa Spika, kupitia Jedwali la Marekebisho napendekeza kuongeza marekebisho ya kifungu cha 404 cha Sheria, ili kumpa Msajili mamlaka ya kufuta kampuni ambayo haijazingatia matakwa ya kifungu cha 33 kinachotaka kampuni kubadili jina iwapo jina hilo linafanana na kampuni nyingine na imepewa notisi ya kubadili jina na Msajili na haijafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 438 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka hitaji kwa kampuni za kigeni kuwasilisha kwa Msajili orodha ya wanahisa na taarifa za umiliki manufaa kama ilivyo kwa kampuni za ndani. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuzuia kampuni kujihusisha na vitendo vya utakatishaji fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na shughuli haramu za dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 440 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka masharti yanayozitaka kampuni za kigeni kujumuisha

katika taarifa ya mwaka mabadiliko yoyote yaliyotokea kwa wanahisa wakati wa kuwasilisha taarifa hiyo kwa Msajili. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kumwezesha Msajili kuhuisha rejesta na kuwa na taarifa sahihi wakati wote.

Mheshimiwa Spika, Kifungu kipya cha 456A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti yanayomtaka Msajili kutunza daftari la wakurugenzi na wanahisa wateule. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha uwazi kwa kuzitaka kampuni kufichua taarifa za wakurugenzi na wanahisa wateule.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 457 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwawezesha watoa taarifa kupata taarifa za umiliki manufaa baada ya kuwasilisha maombi kwa Msajili. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwawezesha watoa taarifa kuwa na taarifa kamili za umiliki manufaa kwa madhumuni ya kudhibiti vitendo vya utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa usambazaji wa silaha za maangamizi. Kifungu kipya cha 468A kinapendekezwa kuongezwa ili kumpa Msajili mamlaka ya kutoa maelekezo na miongozo kwa ajili ya utekelezaji bora wa Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha utekelezaji wa masharti ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nane ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura ya 20.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 4 kinapendekeza kurekebishwa kwa kuondoa masharti yanayoweka ulazima wa shauri lenye sura ya jinai, madai au utawala chini ya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366 na Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 kushughulikiwa kwanza katika utaratibu wa madai au wa kiutawala kabla ya kuanza taratibu za jinai.

Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuhakikisha kuwa makosa ya jinai yanayotokana na masuala ya ajira yanashughulikiwa kwa wakati hivyo kuwezesha upatikanaji wa haki

jinai kwa wakati na kuondoa ucheleweshaji na ukosefu wa haki jinai kwa waathirika wa uhalifu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tisa ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95 ambapo kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza wigo wa fasili ya bangi ili kujumuisha majani na mbegu. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kutambua majani na mbegu kuwa bangi ili kuwezesha utekelezaji wa sheria hususani wakati wa ukamataji, upimaji na uchunguzi wa sampuli au vidhibiti.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 11 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kubainisha kosa la kukutwa na mbegu za mmea wowote uliokatazwa pasipo kujali dhumuni la matumizi ya mbegu husika ikijumuisha uzalishaji wa madawa ya kulevya. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kupanua wigo wa kosa la kumiliki na kusambaza mbegu za mimea iliyokatazwa na Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 12 kinapendekezwa kurebishwa kwa kubainisha uwezo wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kutengeneza kanuni na kutofautisha na kanuni zinazoweza kutengenezwa na Waziri. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuondoa muingiliano wa utekelezaji wa mamlaka ya kutengeneza kanuni chini ya Sheria husika.

Mheshimiwa Spika, Vifungu vya 15 na 16 vinapendekezwa kurekebishwa kwa kujumuisha hali za yabisi na kimiminika kwa dawa za kulevya. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kutambua ujazo wa dawa za kulevya katika hali ya kimiminika ambazo awali zilikuwa hazitambuliki katika sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 18 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka bayana kosa la kumiliki dawa za kulevya kinyume na masharti ya kibali. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kutofautisha makosa yanayofanyika chini ya sheria na kosa la umiliki wa dawa za kulevya kinyume na masharti ya kibali.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 25 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kukiboresha kimantiki kwa kujumuisha vitendo vilivyokusudiwa kuwa kosa. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuweka bayana vitendo ambavyo vinawezesha kutendeka kwa kosa la kula njama ya kutenda kosa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 30 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kujumuisha hali zote za yabisi na kimiminika kwa dawa za kulevya. Lengo la marekebisho yanayopendezwa ni kutambua ujazo wa dawa za kulevya katika hali ya kimiminika ambazo awali zilikuwa hazitambuliki katika Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 34 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kutanua wigo wa maofisa wanaoweza kutoa amri ya upekuzi kwa kujumuisha afisa mwidhiniwa wa Mamlaka. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kurahisisha utekelezaji nyakati ambazo matukio yanatokea katika maeneo ambayo haiwezekani kumpata Kamishna Jenerali au Mkuu wa Kituo cha Polisi**.**

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 38 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka sharti la kuainisha nchi ya asili ya dawa za kulevya katika hati ya orodha ya mali wakati wa ukamataji, iwapo nchi hiyo inafahamika. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya sheria.

Mheshimiwa Spika, Jedwali la Tatu linapendekezwa kurekebishwa kwa kurekebisha vichwa vya habari vya Fomu Na. DCEA 001. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kubainisha matumizi sahihi ya Fomu husika.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, Sura ya 174 ambapo Sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa ujumla ili kuweka cheo stahiki cha Mkuu wa Chuo kulingana na matakwa ya NACTVET.

Mheshimiwa Spika, aya ya 1 ya Jedwali inapendekezwa kurekebishwa ili kupunguza idadi ya wajumbe wa Baraza. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufanisi wa utendaji wa Baraza.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Moja ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Chuo cha Uhasibu Arusha, Sura ya 240 ambapo, Sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa ujumla kwa kuweka jina stahiki la Baraza la Uongozi na Mkuu wa Taasisi ili kuendana na matakwa ya NACTVET.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 4 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza wigo wa kazi za Taasisi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuweka misingi ya kisheria kwa kozi zote zinazotolewa na Taasisi na kuongeza ufanisi wa utendaji wa Taasisi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 10 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kumfanya Mkuu wa Taasisi kuwa Katibu wa Baraza la Uongozi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Uongozi.

Mheshimiwa Spika, Jedwali la Kwanza linapendekezwa kurekebishwa kwa kupunguza idadi na kuweka ukomo wa muda wa uteuzi wa wajumbe wa Baraza la Uongozi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha usimamizi bora wa Baraza la Uongozi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Mbili ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1. Kifungu cha 85 cha Sheria kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza masharti ya kuruhusu sheria ndogo kutengenezwa kwa lugha ya utunzi wa sheria kuu husika. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuoanisha lugha ya sheria ndogo na lugha ya utunzi wa sheria kuu ili kuepuka mkinzano wa maneno au misamiati.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Tatu ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Usimamizi wa Mahakama, Sura ya 237. Hata hivyo, kama nilivyoeleza awali, napendekeza kuondolewa kwa mapendekezo ya marekebisho ya sheria hii katika Muswada. Mapendekezo haya yanaondolewa kutokana na kuonekana kwa uhitaji wa kufanyiwa kazi zaidi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Nne ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Baraza la Vijana, Sura ya 441. Hata hivyo, kama nilivyoeleza awali, napendekeza kuondolewa kwa mapendekezo ya marekebisho ya sheria hii katika Muswada ili kutoa fursa kwa mapendekezo husika kufanyiwa kazi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Tano ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria Usajili wa Hataza, Sura ya 217. Kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha fasili ya msamiati "ARIPO office". Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi wa fasili hiyo kama ilivyotumika katika Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 13 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumpa Waziri mamlaka ya kuziondoa kwa muda baadhi ya vumbuzi zinazoweza kusajiliwa kama hataza ambazo zinahusu bidhaa au mchakato wa uzalishaji wa bidhaa kutoka kwenye ulinzi wa Sheria hii. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza wigo wa mamlaka ya Waziri kwa kuzingatia Makubaliano ya Shirika la Biashara Ulimwenguni kuhusu masuala yanayohusiana na biashara ya haki za Miliki Ubunifu (TRIPS Agreement).

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kushauriana na Kamati, napendekeza kuondoa pendekezo la marekebisho ya kifungu hiki kupitia Jedwali la Marekebisho. Lengo la kuondoa mapendekezo hayo ni kuendelea kutambua utaratibu uliopo wa kisheria wa kuondolea baadhi ya uvumbuzi uwezo wa kusajiliwa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 39 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka muda wa ukomo wa ulinzi wa hataza. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuendana na Makubaliano ya

TRIPS ambayo hutoa kiwango cha chini zaidi cha muda wa ulinzi wa hataza.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 73 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwianisha na mapendekezo ya marekebisho katika masharti yaliyopo chini ya Sehemu ya Kumi na Saba.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 74 kinapendekeza kurekebishwa ili kuongeza muda wa ulinzi wa hataza ndogo. Lengo la marekebisho haya ni kuchochea uvumbuzi na ubunifu. Aidha, Kifungu cha 76 kinapendekezwa kurekebiswa ili kutoa ulinzi kwa maumbo bunifu yaliyosajiliwa kupitia sheria za kikanda na kimataifa ambapo Tanzania ni mwanachama.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Sita ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Magereza, Sura ya 58 ambapo Sheria inapendekeza kufanya marekebisho ya jumla kwa kubadilisha majina ya vyeo vya "Principal Commissioner" na "Commissioner" na kutumia jina la cheo la "Commissioner General". Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuoanisha Sheria na mfumo wa kisheria unaosimamia vyeo ndani ya Jeshi la Magereza Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Vifungu vya 2 na 51 vinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa matumizi ya msamiati "young prisoner". Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuendana na masharti ya Sheria ya Mtoto, Sura ya 13 na kuimarisha ulinzi wa watoto wanaotumikia adhabu ya kifungo.

Mheshimiwa Spika, Kifungu kipya cha 3A kinapendekezwa kuongezwa kwa madhumuni ya kubainisha majukumu na misingi ya utekelezaji wa majukumu ya Utumishi wa Magereza. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Magereza Tanzania chini ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kubainisha mamlaka ya Kamishna Jenerali ya uteuzi,

upandishaji vyeo, uhamisho au ushushaji vyeo kwa maafisa wa magereza. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kubainisha mamlaka hayo ya Mkuu wa Magereza na kuwianisha na mamlaka yaliyopo chini ya Sheria nyingine kuhusu Utumishi wa Magereza.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 7A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka mfumo wa usimamizi wa magereza katika ngazi za mikoa na wilaya. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha uongozi, udhibiti na usimamizi wa magereza kwa kuzingatia muundo wa kiutawala uliothibitishwa na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, baada ya mashauriano kati ya Serikali na Kamati, napendekeza marekebisho ya kifungu hiki kupitia Jedwali la Marekebisho ili kuweka sharti la kumpa Kamishna Mkuu wa Magereza mamlaka ya kuwateua Wakuu wa Magereza wa Wilaya ambao watakuwa chini ya kamandi ya Wakuu wao wa Magereza wa Mkoa.

Mheshimiwa Spika, Vifungu vya 43, 82, 84, 85, 86, 87, 88, 89, 90, 91, 92, 93 na 94 vinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuhuisha faini na adhabu ili ziendane na masharti ya sheria. Lengo la mapendekezo ya marekebisho ni kuendana na thamani ya fedha ya sasa na kuzuia kutendeka kwa makosa hayo.

Mheshimiwa Spika, Kifungu kipya cha 62A kinapendekezwa kuongezwa ili kulipa Jeshi la Magereza Tanzania mamlaka ya kuanzisha programu za urekebishaji wa wafungwa, ikiwemo elimu, mafunzo ya ufundi, huduma za kiroho, kitamaduni, shughuli za kimwili na huduma za msaada wa kisaikolojia. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha urekebishaji bora wa wafungwa na kuwawezesha kurejea katika jamii yao.

Mheshimiwa Spika, Kifungu kipya cha 81A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti ya msaada kwa wafungwa baada ya kuachiwa huru ikiwemo usafiri kwenda sehemu zao makazi pamoja na uunganishaji na taasisi za Serikali na huduma za kijamii.

Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwezesha urejeaji salama wa wafungwa waliomaliza vifungo vyao katika jamii.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 105 kinapendekeza kurekebishwa kwa kumuwezesha Waziri kutengeneza kanuni kuhusiana na urekebishaji bora wa wafungwa na kuwawezesha kurejea katika jamii yao kwa lengo la kuweka utekelezaji bora wa masharti ya sheria.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Saba ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Usimamizi wa Maabara Binafsi za Afya, Sura ya 136 Toleo la 2023 ambapo Sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa ujumla kwa kufuta neno "*technologist*" na badala yake, kuweka neno "*practitioner*". Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuiwianisha Sheria hii na Sheria ya Watoa Huduma ya Afya, Sura ya 48 ambayo inatumia neno la jumla "*practitioner*" kujumuisha mwanasayansi wa maabara ya afya, mteknolojia wa maabara ya afya na msaidizi wa maabara za afya.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha fasili ya msamiati "*private health laboratory*" kwa kujumuisha aina mpya za maabara na maeneo ya upimaji. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza wigo wa maabara binafsi ambazo zinaweza kusajiliwa na Bodi, kwa kuzingatia maendeleo ya sayansi na teknolojia. Aidha, kifungu hicho kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha msamiati "*private health laboratory services*" kwa lengo la kuondoa huduma ambazo kwa sasa zinasimamiwa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania zinazohusiana na vifaa vya uchunguzi wa maabara. Vilevile, kifungu hicho kinapendekezwa kurekebishwa ili kujumuisha tafsiri ya misamiati mipya iliyotumika katika Sheria. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kutoa tafsiri iliyokusudiwa ya misamiati hiyo kama ilivyotumika katika Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 12 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka rejea sahihi ya Sheria inayosimamia wataalamu wa

maabara ya afya. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kutoa ufafanuzi kuhusiana na Sheria husika inayosimamia usajili wa wataalamu wa maabara ya afya. Aidha, kifungu hicho kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza adhabu kwa watu wanaokiuka masharti ya Sheria. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuhakikisha adhabu inaendana na ukubwa wa kosa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 12A kinapendekezwa kuongezwa kwa kuweka wajibu kwa mtu aliyeidhinishwa kuendesha maabara binafsi kuwa na wajibu wa kusimamia shughuli za kila siku za maabara binafsi ya afya. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuhakikisha uwazi na uwajibikaji wa watu walioidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 13 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza wigo wa utambuzi wa maabara binafsi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwezesha umma kutambua aina mpya za maabara binafsi za afya zilizoongezwa. Kifungu cha 14 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka ukomo wa juu na wa chini wa adhabu kwa watu wanaoendesha maabara binafsi bila kusajiliwa au ambao usajili wao umesitishwa. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha adhabu zinazowekwa na sheria zinaendana na uzito wa makosa.

Mheshimiwa Spika, kifungu kipya cha 17A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka adhabu ya jumla kwa makosa ambayo adhabu yake haijatajwa katika Sheria. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kutoa mwongozo wa adhabu ambayo inaweza kutolewa kwa makosa yaliyotendwa chini ya Sheria hiyo pale ambapo sheria haijabainisha adhabu.

Mheshimiwa Spika, Kifungu kipya cha 17B kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka sharti la kinga kwa wajumbe wa Bodi, Msajili au wafanyakazi kutowajibishwa binafsi kisheria kwa makosa wanayoyafanya kwa nia njema wakati wa utekelezaji wa majukumu yao. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kumlinda msajili,

wajumbe wa bodi na watumishi ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao bila hofu ya kushtakiwa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 18 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kutoa mamlaka kwa Waziri ya kuainisha katika Kanuni majukumu mahususi na taratibu zinazopaswa kuzingatiwa na watu walioidhinishwa kuendesha maabara binafsi. Kifungu cha 21 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kutoa fursa ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa Bodi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kutoa haki ya kikatiba ya kukata rufaa.

Mheshimiwa Spika, Jedwali linapendekezwa kurekebishwa katika aya ya 1 kwa kupitia upya muundo wa Bodi ili kujumuisha uwakilishi wa kitaaluma wa sekta hiyo na kuwezesha utekelezaji bora wa shughuli za Bodi. Vilevile, aya ya 1A inapendekezwa kuongezwa ili kuainisha ukomo wa wajumbe wa Bodi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha uwajibikaji na utendaji bora wa wajumbe wa Bodi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, Aya ya 9 inapendekezwa kuongezwa ili kuipa Bodi mamlaka ya kuanzisha kamati zitakazoisaidia katika utekelezaji wa majukumu yake. Aya ya 10 inapendekezwa kuongezwa ili kujumuisha masharti kuhusu mgongano wa kimaslahi kwa wajumbe. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwezesha uendeshaji bora wa mikutano na kuimarisha ufanisi wa Bodi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Nane ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Huduma za Maktaba Tanzania, Sura ya 102 ambapo Sheria inapendekezwa kufanyiwa marekebisho ya ujumla kwa kufuta msamiati "*Director*" na badala yake kuweka neno "*Director General*". Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwianisha Sheria na Muundo wa Huduma za MaktabaTanzania.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha fasili ya msamiati "book" na kuongeza misamiati

mipya. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kutoa fasili mahsusi ya misamiati kama ilivyotumika katika Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 4 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza wigo wa kazi za Bodi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza wigo wa kazi za Bodi kwa nia ya kuimarisha usimamizi na udhibiti wa huduma za maktaba.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kushauriana na Kamati a Utawala, Katiba na Sheria, napendekeza marekebisho ya kifungu hiki kupitia Jedwali la Marekebisho ili kuipa Bodi mamlaka ya kuhakikisha kuwa vitabu na machapisho yanayotunzwa katika maktaba ni yale yanayokuza maadili ya kitaifa, mila na desturi na yasiyokuwa na maudhui yanayokyuka maadili hayo.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha adhabu kwa ukiukwaji wa kifungu hiki. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwianisha adhabu na hali halisi ya sasa ya kiuchumi. Aidha, marekebisho yanakusudia kuzuia ukiukwaji wa masharti ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 13 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kujumuisha vyanzo vingine vya mapato ya Bodi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza wigo wa vyanzo vya mapato ya Bodi kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 14 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza kiwango cha fedha kinachoweza kuhamishwa kutoka kwenye bajeti iliyotengwa kutoka shilingi elfu hamsini hadi shilingi milioni Hamsini. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuendana na mabadiliko ya thamani ya fedha ili kuhakikisha utekelezaji wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, Jedwali linapendekezwa kurekebishwa kwa kubainisha wajumbe wa Bodi. Lengo la marekebisho

yanayopendekezwa ni kuongeza ufanisi wa Bodi katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Tisa ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania, Sura ya 364 ambapo Sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa ujumla kwa kuweka cheo stahiki cha Mtendaji Mkuu wa Bodi. Lengo la marekebisho yanayoopendekezwa ni kuwianisha cheo hicho na muundo wa sasa wa Bodi ya Utalii Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza fasili ya misamiati mipya kwa lengo la kutoa fasili ya misamiati hiyo kama ilivyokusudiwa kutumika katika Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 5 cha Sheria kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza majukumu ya Bodi yanayohusiana na vifaa na shughuli za utalii. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufanisi katika kusimamia shughuli za utalii. Jedwali linapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha muundo wa Bodi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufanisi wa Bodi katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kushauriana na Kamati, napendekeza marekebisho ya aya (g) ya Jedwali la Sheria kupitia Jedwali la Marekebisho ili kuongeza wawakilishi kutoka Shirikisho la Utalii Tanzania kuwa sehemu ya wajumbe wa Bodi ya Utalii.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Utalii, Sura ya 65 ambapo Sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta rejea ya "*Director*" katika vifungu mbalimbali na badala yake kuweka rejea ya "*Director General*" ili kuhamisha majukumu ya kiutendaji ya kusimamia shughuli za utalii kutoka kwa Mkurugenzi wa Utalii kwenda kwa Bodi ya Utalii. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha ufanisi katika kusimamia shughuli za utalii kwa kuwa majukumu hayo

ya kiutendaji yatatekelezwa na Bodi ya Utalii na Wizara itabaki na jukumu la usimamizi wa jumla na majukumu ya kisera.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 2 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa kuongeza fasili ya msamiati "*Director General*" ili kuweka ufafanuzi wa msamiati huo kama ulivyotumika katika masharti mbalimbali ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 4 kinapendekezwa kurekebishwa ili kufafanua mamlaka ya Kamati ya kitaalamu ya ushauri. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kubainisha jukumu la ushauri la Kamati katika masuala mbalimbali yaliyo chini ya Sheria. Kifungu cha 6 kinapendekezwa kurekebishwa kwa madhumuni ya kuhamisha majukumu yote ya kiutendaji yanayohusiana na usimamizi wa shughuli za utalii kutoka kwa Mkurugenzi wa Utalii. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha ufanisi katika kusimamia shughuli za utalii kwa kuwa majukumu hayo ya kiutendaji yatatekelezwa na Bodi ya Utalii na Wizara itabaki na jukumu la usimamizi wa jumla na majukumu ya kisera.

Mheshimiwa Spika, Vifungu vya 13 na 34 vinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa sharti la kuchapisha katika Gazeti la Serikali orodha ya vituo vilivyosajiliwa au vilivyopangiwa madaraja, shughuli za utalii na waendeshaji wa utalii. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kurahisisha utaratibu wa kuchapisha taarifa zinazohusiana na vituo vya utalii, shughuli na waendeshaji wa utalii na kurahisisha upatikanaji wa taarifa za utalii kwa umma. Kifungu cha 14 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa sharti la kulipa ada za upangaji wa madaraja zinazolipwa na waendeshaji wa vituo vya utalii. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwahimiza waendeshaji wa utalii kupandisha madaraja vituo vyao vya utalii na kuboresha huduma za utalii. Kifungu cha 16 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa jukumu la Waziri katika kufuta usajili wa vituo vya utalii au shughuli za utalii. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwezesha utekelezaji bora wa majukumu ya kiutendaji ya Bodi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 17 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kumpa Mkurugenzi Mkuu wajibu wa kupendekeza vituo au shughuli kwa ajili ya kutangazwa na Waziri kama vituo au shughuli za utalii. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kutambua mamlaka ya kiutendaji yaliyowekwa kwa Bodi. Kifungu cha 36 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kubainisha muda halali wa leseni kuwa miezi kumi na miwili kuanzia tarehe ya kutolewa kwake. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuondoa utata na kuweka bayana usahihi wa kisheria hivyo kurahisisha usimamizi wa shughuli za kitalii. Kifungu cha 42 kinapendekezwa kurekebishwa na 43 kinapendekezwa kufutwa kwa kuondoa masharti ya vigezo na taratibu za usajili wa waongoza watalii. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuboresha usimamizi wa waongoza utalii ili kukuza sekta ya utalii na ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, Vifungu vya 50 na 53 vinapendekezwa kurekebishwa kwa kumjumuisha Mkurugenzi Mkuu katika masharti ya vifungu hivyo. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha masharti hayo na mapendekezo ya kumpa Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Utalii majukumu ya kiutendaji**.**

Mheshimiwa Spika, Jedwali la Kwanza la Sheria linapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha muundo wa Kamati ya Ushauri ya Wataalamu na kupunguza idadi ya mikutano ya lazima ya Kamati kutoka minne hadi miwili kwa mwaka. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa kazi za Kamati na kupunguza gharama za uendeshaji wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya mashauriano na Kamati, napendekeza marekebisho ya muundo wa Kamati ya Ushauri ya Wataalamu kupitia Jedwali la Marekebisho ili kuongeza wawakilishi kutoka sekta binafsi kuwa miongoni mwa wajumbe wa Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Moja ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Alama za Biashara na Huduma, Sura ya 326 ambapo kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha fasili ya misamiati iliyotumika katika

Sheria na kuweka fasili mpya ya misamiati iliyotumika kwenye Sheria. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kutoa ufafanuzi wa masharti katika Sheria.

Mheshimiwa Spika, Vifungu vipya vya 16A na 16B vinapendekezwa kuongezwa kwa ajili ya kutoa ulinzi wa alama za pamoja na usajili wa alama za uthibitisho. Lengo la marekebisho haya ni kuweka ulinzi wa alama za pamoja kwa njia ya usajili na kushughulikia usajili wa alama za uthibitisho ambazo baada ya usajili zitaweza kulindwa chini ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 19A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti kuhusu ulinzi wa alama ya biashara inayojulikana kwa mujibu wa Mikataba ya Kikanda au Kimataifa iliyoridhiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lengo la marekebisho haya ni kuweka ulinzi wa alama hizo za biashara chini ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 26 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumpa Msajili mamlaka ya kutangaza maombi ya usajili wa alama kabla ya kuyakubali. Lengo la marekebisho haya ni kutoa fursa kwa umma ya kutoa maoni yao kuhusiana na maombi yaliyowasilishwa pale ambapo Msajili anaona kuwa kuna mazingira ya kipekee ya kufanya hivyo kabla ya kukubali maombi hayo.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 28A kinapendekezwa kuongezwa ili kutambua alama za biashara na huduma zilizosajiliwa na Shirika la Miliki Bunifu Kanda ya Afrika, likibainisha Tanzania kama nchi teule, kabla ya kuanza kutumika kwa Itifaki ya Banjul katika Jamhuri ya Muungano. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha ulinzi wa alama za biashara na huduma zinazotambuliwa chini ya Itifaki ya Banjul ambayo Nchi yetu imetia saini na kuiridhia.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Mbili ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148. Hata hivyo, kama nilivyoeleza awali, napendekeza kuondolewa kwa mapendekezo ya marekebisho ya sheria hii katika

Muswada kwa kuwa marekebisho husika yaliwasilishwa na kushughulikiwa kupitia Muswada wa Fedha wa mwaka 2026.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa utawala wa sheria katika maendeleo ya Taifa ulielezwa vyema na Hayati Askofu Desmond Tutu aliposema kwamba, "*Strengthening the rule of law is an essential ingredient to enhance justice, peace, and economic and social progress*", yaani "*Kuimarisha utawala wa sheria ni nguzo muhimu katika kuendeleza haki, amani, pamoja na maendeleo ya kiuchumi na kijamii*." Kauli hii inatukumbusha kwamba utawala wa sheria ni msingi muhimu wa kujenga jamii yenye haki, taasisi zinazowajibika na mazingira yenye utulivu yanayowezesha shughuli za kijamii na kiuchumi kustawi. Vilevile, Kauli hii inaendana na mwelekeo wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, ambayo utekelezaji wake unahitaji uwepo wa taasisi madhubuti, uwajibikaji na mazingira ya kisheria yanayowezesha shughuli za kijamii na kiuchumi kufanyika kwa ufanisi. Hivyo, kuendelea kuimarisha utawala wa sheria ni sehemu muhimu ya kuweka msingi wa kufikia malengo ya maendeleo yaliyowekwa katika Dira 2050.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena, ninaomba Bunge lako tukufu liujadili Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2026) na kuupitisha pamoja na marekebisho yake katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Hamza S. Johari (Mb.),
MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI
1 Septemba, 2026

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Kabla ya kumwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, nina matangazo hapa kutoka kwa Katibu wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, mnataarifiwa kuwa semina ya *Kingdom Leadership Network Tanzania, World Vision Tanzania* na *The Tanzania Parliamentary Fellowship* kuhusu *Ethical Leadership and Servant Governance, Strengthening Integrity and Accountability in Public Service* iliyotangazwa kufanyika kesho Jumatano, tarehe 2 Septemba, 2026 imeahirishwa hadi hapo itakapotangazwa tena.

Sasa ninamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, na kwa niaba yake Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa *Advocate* Edwin Swalle.

MHE. EDWIN E. SWALLE – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026, *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill 2026]*.

Mheshimiwa Naibu Spika, utangulizi. Awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kuniwezesha kuja mbele ya Bunge lako Tukufu siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wote na kwa mujibu wa Kanuni ya 102(5) na Kanuni za Kudumu za Bunge 2025, ninaomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026, *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill 2026]*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba taarifa iliyobeba maoni ya Kamati iwekwe kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge, *(Hansard),* kama ilivyowasilishwa Mezani kwako.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Kikao cha Tisa cha Mkutano wa Pili wa Bunge la Kumi na Tatu, tarehe 6 Februari, 2026 kwa utaratibu ulioainishwa katika Kanuni ya 99 (1). Baada ya hatua hiyo, na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 100(1), ulitumia mamlaka yako kuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namna Kamati ilivyotekeleza jukumu la uchambuzi. Uchambuzi wa miswada ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 100(1) na Kanuni ya 139(14) ikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilitekeleza kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupokea na kujadili maelezo ya Serikali kuhusu maudhui ya Muswada yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Hamza Saidi Johari tarehe 3 Machi, 2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hatua hiyo, Kamati ilipokea na kujadili maoni ya wadau katika Mkutano wa kupokea maoni ya wadau *(public hearing)* uliofanyika tarehe 4 Machi, 2026 kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 100(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkutano huo, jumla ya wadau 45 kutoka vyama na asasi za kiraia 11 walifika na kutoa maoni yao mbele ya Kamati. Vyama na asasi hizo ni kama zinavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie fursa hii kuwashukuru sana wadau wote waliowasilisha maoni yao mbele ya

Kamati. Kwa sehemu kubwa, walisaidia sana Kamati kufanya uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa Muswada na mapendekezo ya maboresho ya Kamati. Kamati ilifanya kazi kwa kuchambua Muswada wote wenye jumla ya Ibara 161 zinazolenga kurekebisha Sheria 21 kama zilivyotajwa kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umeangazia Sheria zote 21 kwa kuzigawa katika sehemu kuu tatu kama ifuatavyo;-

(a) Uchambuzi kuhusu sheria ambazo marekebisho yake yameondolewa katika Muswada kutokana na sababu mbalimbali.

(b) Uchambuzi kuhusu sheria ambazo marekebisho yake yote yaliyokuwa kwenye Muswada yameridhiwa na Kamati na;

(c) Uchambuzi kuhusu sheria ambazo marekebisho yake yameboreshwa na Serikali kutokana na maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu hizi tatu zimechambuliwa na Kamati kama zilivyo kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi kuhusu sheria ambazo marekebisho yake yameondolewa katika Muswada kutokana na sababu mbalimbali; moja, marekebisho ya sheria nne ambazo ni Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania Sura 197, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura 148, Sheria ya Usimamizi wa Mahakama Sura 237, na Sheria ya Baraza la Vijana Sura 441, marekebisho yake yaliondolewa kwenye Muswada kutokana na sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Sheria ya Baraza la Vijana, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba Sheria hii inahitaji marekebisho makubwa ambayo kwa sehemu kubwa yanajumuishwa kwenye Muswada. Kwa sababu hizo, Kamati na Serikali walikubaliana kuondoa marekebisho ya Sheria hii ili kutoa

nafasi kwa Serikali kuifanyia kazi Muswada huu zaidi. Ufafanuzi kuhusu sheria ambazo zimeondolewa kwenye Muswada huu na sababu za kuondoa Sheria hizo ni kama unavyoonekana kwenye ukurasa wa saba hadi ukurasa wa tisa wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi kuhusu sheria ambazo marekebisho yake yote yameridhiwa na Kamati. Kamati kupitia uchambuzi wake ilijiridhisha kwamba marekebisho yaliyopo kwenye sheria nane kati ya sheria 21 yanajitosheleza, na Sheria hizo ni kama zifuatazo:-

(i) Sheria ya Nguvu za *Atom* Sura 188;
(ii) Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura ya 20;
(iii) Sheria ya Udhibiti na Kupambana na Rushwa Sura ya 95;
(iv) Sheria ya Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini Sura 174;
(v) Sheria ya Chuo cha Uhasibu Arusha Sura 240;
(vi) Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya kwanza;
(vii) Sheria ya Usimamizi wa Maabara Binafsi za Afya Sura 136; na
(viii) Sheria ya Alama za Biashara na Huduma Sura 326.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi kuhusu sheria ambazo marekebisho yake yameboreshwa na Serikali kutokana na maoni ya Kamati. Uchambuzi wa Kamati kwenye Muswada huu ulibaini kuwa jumla ya sheria tisa kati ya sheria 21 marekebisho yake yanayopendekezwa yanapaswa kufanyiwa maboresho ili yaweze kukidhi kikamilifu lengo lililokusudiwa. Sheria hizo ni kama zifuatazo:-

(i) Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu Sura 423;
(ii) Sheria ya Majina ya Biashara Sura 213;
(iii) Sheria ya Usafiri wa Anga Sura ya 80;
(iv) Sheria ya Kampuni Sura 212;
(v) Sheria ya Usajili wa Hataza Sura 217;
(vi) Sheria ya Magereza Sura 58;
(vii) Sheria ya Taifa ya Huduma za Maktaba Tanzania Sura 102;

(viii) Sheria ya Bodi ya Utalii Sura 364; na
(ix) Sheria ya Utalii Sura 65.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia maoni na ushauri wa Kamati, Serikali imeboresha Ibara mbalimbali kupitia jedwali lake na marekebisho. Uchambuzi wa baadhi ya Sheria na maoni umezingatiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu Sura 223. Pamoja na Kamati kukubaliana na mapendekezo ya Sheria hii ilikuwa na maoni mbalimbali yaliyolenga kuboresha marekebisho haya, na baadhi ya masuala hayo ni kama yafuatayo:-

(a) Katika fasili ya msamiati "*domestic and foreign politically exposed person*", mojawapo ya watu waliojumuishwa ni "kiongozi muhimu wa chama cha siasa *("important political party official")*. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa msamiati huo haujafasiriwa na Sheria, na hivyo unaweza kuleta utata katika utekelezaji wa Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, utata huo unaweza kusababishwa kutokana na miundo ya kiuongozi ya vyama vya siasa nchini na katika Bara la Afrika kwa ujumla. Hali hiyo inatokana na ukweli kwamba kila kiongozi katika chama cha siasa, kwa ngazi ya chini na ya juu ni mtu wa muhimu. Umuhimu huo umetofautiana kwa kulingana, chama na majira na nyakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na sababu hiyo, Kamati ilishauri msamiati huo ufasiriwe katika sheria. Serikali imekubali ushauri wa Kamati kwa kuboresha Ibara ya Tano ya Muswada kupitia jedwali la marekebisho ya Serikali.

(b) Kukosekana kwa fasili ya msamiati "miamala shuku", *("suspicious transaction"),* katika Sheria. Msamiati huo ni mojawapo ya msingi mkuu wa sheria hii. Hata hivyo, msamiati huo haukufasiriwa kwenye sheria. Jambo hili linaweza kuleta utata katika utekelezaji

wa sheria hii, na hivyo kushauri maneno hayo yafasiriwe. Serikali imekubali ushauri wa Kamati na kujumuisha fasili ya maneno hayo kwenye jedwali la marekebisho.

(c) Ibara ya 18(A) inayopendekezwa, imeweka masharti ambapo wataalamu mbalimbali wakiwemo mawakili na makamishna wa viapo, wanawajibika kuripoti kwenye kitengo cha kupambana na fedha haramu, *(FIU)*, taarifa ya miamala shuku ya wateja wao. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba;

(i) Sharti hili likiwekwa moja kwa moja bila ya kuwekewa mipaka, *(exception)*, linaweza kusababisha masharti ya Sheria hii yakakinzana na Ibara ya 16 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya kulinda haki ya faragha, ikiwemo faragha ya taarifa za wateja mbalimbali ambazo mawakili wanazipata pindi wanapohudumia wateja wao.

(ii) Masharti ya Ibara hiyo yasipowekewa mipaka, yanaweza kukinzana na masharti ya Sheria ya Mawakili Sura 341 ikisomwa kwa pamoja na Kanuni ya 30 na 31 ya Kanuni za Maadili ya Mawakili, (Maadili na Mwenendo wa Kitaaluma, za mwaka 2018 zinazotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 118 la tarehe 9 Machi, 2018). Sheria kupitia kanuni hizo zinawataka mawakili kutunza siri za wateja wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uchambuzi huo, Kamati ilishauri pendekezo hili liwekewe mipaka kwa kumlinda wakili pale ambapo atakuwa anatekeleza majukumu yake ya msingi na kutoa ushauri wa kisheria kwa mteja wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mashauriano, Serikali imeweka mipaka kwa kuboresha Ibara ya Nane ya Muswada huu. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa uamuzi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa jumla wa Kamati. Pamoja na maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kwenye Ibara mbalimbali za Muswada ambayo kwa sehemu kubwa

yamekubaliwa na Serikali kwa kuzingatia katika jadwali la marekebisho, Kamati ina maoni ya jumla kama ifuatavyo: -

(i) Baada ya Kamati kuishauri Serikali kuleta Muswada mahususi unaohusu Sheria ya Baraza la Vijana, Serikali ihakikishe kuwa inachukua hatua za kuleta mapendekezo hayo na maboresho mapema ili vijana wanufaike na uwepo wa Sheria ya Vijana inayokidhi maslahi yao;

(ii) Maboresho ya Sheria ya Chuo cha Uhasibu Arusha, Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini yanaweka muda wa uteuzi wa Wajumbe wa Bodi wa Baraza la Chuo kukaa madarakani kuwa miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kimoja. Hata hivyo, sifa za uteuzi hazijatajwa katika sheria. Serikali itengeneze kanuni *(rules)* zitakazoweka uwazi na sifa za uteuzi;

(iii) Serikali ilishatoa ahadi Bungeni kuwa upatikanaji wa viongozi na Wajumbe wa Bodi katika Mashirika ya Umma utaanza kufanyika kwa njia ya ushindani. Hata hivyo, bado Serikali imeendelea kuleta marekebisho ya sheria ambayo hayaakisi ahadi hii. Kwa kuwa Serikali imeeleza kuwa baadhi ya mashirika, upatikanaji wa viongozi na Wajumbe wa Bodi hautakuwa wa ushindani kama yalivyo kwenye Tume ya Nguvu za Atomu, Serikali itoe tangazo kupitia Gazeti la Serikali litakalotaja mashirika ambayo upatikanaji wa viongozi wake hautokani na ushindani;

(iv) Sheria ya Magereza imeboreshwa ambapo pamoja na mambo mengine wafungwa watapewa ujuzi mbalimbali ili waweze kurejea kwenye jamii wakiwa watu wema. Wafungwa ambao watakidhi vigezo vya ufundi na ujuzi katika fani zitakazofundishwa wapewe vyeti vya kufuzu mafunzo hayo ili waweze kutambulika na kupewa kazi ambazo wamejifunza pindi walipokuwa kwenye magereza na watakaporejea uraiani;

(v) Baadhi ya sheria zilitungwa zamani, mtindo wa uandishi wake ulikuwa wa kimapokeo zaidi yaani mtindo wa kale ukijumuisha matumizi ya aya ndefu, sentensi ndefu, na matumizi ya kauli

kutendwa *(passive voice)* badala ya kauli tenda *(active voice)* na matumizi ya lugha ya kale *(archaic language)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya sheria hizo ni Sheria ya Huduma za Maktaba iliyotungwa mwaka 1975. Kwa sasa dunia imebadili uelekeo na inachagiza uandishi wa kisasa wa sheria unaotumia lugha nyepesi *(plain language)* ambayo inaeleweka kwa urahisi kwa walengwa. Ili kuendana na mabadiliko ya kidunia, Serikali ilete mapendekezo ya kuzifuta na kuzitunga upya sheria ambazo zimeandikwa kwa mtindo wa kizamani ili walengwa waweze kuzielewa kwa urahisi zaidi; na

(vi) Serikali iendelee kuchukua hatua ya kurekebisha sheria ili kuweka misingi ya utawala bora na mgawanyo wa kazi kwa kutenganisha kazi ya kusimamia sera na kazi ya kusimamia utendaji wa kila siku kama ilivyofanya kwenye Sheria ya Bodi ya Utalii na Sheria ya Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Ninaomba kuhitimisha kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Spika wa Bunge (Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu) pamoja na wewe Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuongoza Bunge letu vema.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa dhati ninapenda kumshukuru na kumpongeza sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Hamza Saidi Johari Mbunge, kwa ushirikiano mkubwa alioipatia Kamati yetu kuandaa Muswada huu pamoja na kuwa tayari kusikiliza, kupokea na kuufanyia kazi ushauri wa Kamati kama ulivyotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ninamshukuru Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Dkt. Juma Zuberi Homera; Balozi Khamis Mussa Omar, Waziri wa Fedha; Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Zainab Athman Katimba; Mheshimiwa Mhandisi Mshamu Ali Munde, Naibu Waziri wa Fedha; na Mheshimiwa Laurent

Luswetula, Naibu Waziri wa Fedha, kwa ushirikiano wao mkubwa walioipatia Kamati wakati wa uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Kamati inapenda kuwashukuru watendaji wote wa Serikali wakiongozwa na Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali *(CPD)* Ndugu Onorius Njole kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha kuchambua Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwapongeza Wajumbe wa Kamati kwa umahiri wao, umakini na ushirikiano ambao wameutoa wakati wote wa kupitia na kuchambua Muswada huu ili hatimaye kazi iweze kukamilika na kutoa taarifa hii ambayo imetolewa leo. Ninaomba majina yao yazingatiwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu ninamshukuru sana Ndugu Baraka Leonard, Katibu wa Bunge kwa niaba ya watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026 *(The Written Laws Miscellaneous Amendment Bill, 2026)* pamoja na marekebisho yake kama ulivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA WA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI WA MWAKA 2026 ([*THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) BILL, 2026*])] - KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102(5) na Kanuni ya 139 (11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026** ***[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2026]***.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ulisomwa Bungeni Mara ya Kwanza katika Kikao cha Tisa cha Mkutano wa Pili wa Bunge la Kumi na Tatu tarehe 6 Februari, 2026 kwa utaratibu ulioainishwa katika **Kanuni ya 99 (1)**. Baada ya hatua hiyo, na kwa kuzingatia masharti ya **Kanuni ya 100 (1)** ikisomwa pamoja na **Kanuni ya 139 (14)**, ulitumia mamlaka yako kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, ili ufanyiwe uchambuzi.

1.1 Namna Kamati Ilivyotekeleza Jukumu la Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Miswada ya Sheria ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 100(1), Kanuni ya 139 (14) ikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025. Katika kuteleza jukumu hilo, Kamati ilitekeleza kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupokea na kujadili Maelezo ya Serikali kuhusu maudhui ya Muswada yaliyowasilishwa na

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza Saidi Johari, Mb, tarehe 3 Machi, 2026.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, Kamati ilipokea na kujadili maoni ya wadau katika Mkutano wa Kupokea Maoni ya Wadau *(Public Hearing)* uliofanyika tarehe 4 Machi, 2026 kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 100 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika Mkutano huo, jumla ya wadau 45 kutoka katika vyama na asasi za kiraia 11 walifika na kutoa maoni yao. Vyama na asasi hizo ni: -

(i) Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS);
(ii) Muungano wa asasi za kiraia zinazopigania na kutetea haki za ardhi Tanzania (TALA);
(iii) HAKI ARDHI;
(iv) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC);
(v) Restless Development Tanzania (RDT);
(vi) Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC);
(vii) Tourism Confederation of Tanzania (TCT);
(viii) Network for Voice of Sober Houses Tanzania (NFVOSH);
(ix) Voice for Youth (V4Y);
(x) Chama cha Wataalamu wa Maabara ya Tiba Tanzania (MeLSAT); na
(xi) Chama cha Wataalamu wa Patholojia Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati wadau wote waliowasilisha maoni ambayo kwa sehemu kubwa yaliisaidia Kamati katika uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa maoni ya wadau, Kamati ilifanya mashauriano na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu maboresho kwenye baadhi ya Ibara za Muswada. Baadhi ya vikao hivyo, Mwanasheria Mkuu aliambatana na Mhe. Juma Zuberi Homera (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar, (Mb.) Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zainabu Katimba, Mb Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, na Mhe. Laurent Deogratius

Luswetula (Mb), Naibu Waziri wa Fedha pamoja na watalaam mbalimbali wa Serikali.

1.2 Sheria zilizochambuliwa na Kamati

Mheshimiwa Spika, katika Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026 unalengo la kurekebisha Sheria ishirini na moja (21). Sheria hizo ni: -

(i) Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu, Sura ya 423 *(The Anti-Money Laundering Act, Cap. 423)*;
(ii) Sheria ya Nguvu za Atomu, Sura ya 188 *(The Atomic Energy Act, Cap 188)*;
(iii) Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197 *(The Bank of Tanzania Act, Cap.197)*;
(iv) Sheria ya Majina ya Biashara, Sura ya 213 *(The Business Names Act, Cap. 213)*;
(v) Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80 *(The Civil Aviation Act, Cap. 80)*;
(vi) Sheria ya kampuni Sura ya 212 *(The Companies Act, Cap 212)*;
(vii) Sheria ya Mwenendo wa makosa ya Jinai, Sura ya 20 *(The Criminal Procedure Act, Cap* 20);
(viii) Sheria ya Kuthibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95 *(The Drug Control and Enforcement Act, Cap 95)*;
(ix) Sheria ya Chuo cha ya Mipango na Maendeleo ya Vijijini, Sura ya 174 *(The Institute of Rural Development Planning Act, Cap 174)*;
(x) Sheria ya Chuo cha Uhasibu Arusha, Sura ya 240 *(The Institute of Accountancy Arusha Act, Cap 240)*;
(xi) Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya 1 *(The Interpretation of Laws Act, Cap 1)*;
(xii) Sheria ya Usimamizi wa Mahakama Sura ya 237 *(The Judiciary Administration Act, Cap 237)*;
(xiii) Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa, Sura ya 441 *(The National Youth Council Act, Cap 441)*;

(xiv) Sheria ya Usajili wa Hataza, Sura ya 217 *(The Patents (Registration) Act, Cap 217)*;

(xv) Sheria ya Magereza, Sura ya 58 (The Prisons Act, Cap 58);

(xvi) Sheria ya Usimamizi wa Maabara Binafsi za Afya, Sura ya 136 *(The Private Health Laboratories (Regulation) Act, Cap 136);*

(xvii) Sheria ya Taifa ya Huduma za Maktaba Tanzania, Sura ya 102 *(The Tanzania Library Services Act, (Cap. 102);*

(xviii) Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania, Sura ya 364 *(The Tanzania Tourist Board Act, (Cap. 364);*

(xix) Sheria ya Utalii, Sura ya 65 *(The Tourism Act, (Cap. 65);*

(xx) Sheria ya Alama za Biashara na Huduma, Sura ya 326 [*Trade and Service Marks Act, (Cap. 326);* na

(xxi) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 *(The Value Added Tax Act, Cap 148)*.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA NA MAPENDEKEZO YA MABORESHO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, kabla ya Kamati kukutana na Serikali ili kupokea maelezo ya mtoa hoja ambaye ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ilianza kwa kuuchambua Muswada wote wenye jumla **Ibara 161** zinazolenga kurekebisha **Sheria ishirini na moja (21)**. Kutokana na uchambuzi huo, uchambuzi wa maoni ya wadau na mashauriano na Serikali, Kamati ilikamilisha kazi yake ya uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi huu unaangazia sheria zote ishirini na moja zilizopo kwenye Muswada na umegawanyika katika sehemu tatu (3) ambazo ni:-

(a) Uchambuzi kuhusu Sheria ambazo marekebisho yake yameondolewa katika Muswada kutokana na sababu mbalimbali;

(b) Uchambuzi kuhusu Sheria ambazo marekebisho yake yote yaliyopo kwenye Muswada yameridhiwa na Kamati; na
(c) Uchambuzi kuhusu Sheria ambazo marekebisho yake yameboreshwa na Serikali kutokana na maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu uchambuzi wa sehemu hizi tatu ni kama ifuatavyo:-

2.1 Uchambuzi kuhusu Sheria ambazo marekebisho yake yameondolewa katika Muswada kutokana na sababu mbalimbali

Mheshimiwa Spika, Sheria nne marekebisho yake yaliondolewa kwenye Muswada kutokana na sababu mbalimbali. Sheria hizo na sababu zake ni kama zifuatazo:-

(a) **Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania Sura ya 197.**

Sheria hii marekebisho yake yaliondolewa na kuhamishiwa kwenye Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2026. Kuhamishiwa huko kulitokana na dhumuni la marekebisho ambalo lilikuwa ni kuiwezesha **BOT** kuikopesha Serikali mikopo ya muda mfupi. Uchambuzi wa Kamati kwa kushirikiana na Kamati ya Bajeti ulibaini kwamba, suala hilo linahusu bajeti na utendaji kazi wa **BOT**, mambo ambayo kwa kawaida hurekebishwa kupitia Sheria ya Fedha. Kutokana na sababu hizo, Kamati ilikubaliana na Serikali kuwa marekebisho ya Sheria yaondolewe katika Muswada ili maboresho yake yafanyiwe kazi katika Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2026.

(b) **Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148.**

Marekebisho ya sheria hii yalihamishiwa kwenye Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2026. Hatua hiyo ilitokana na dhumuni la marekebisho ambalo ilikuwa ni Kumtaka Kamishna wa **TRA** kufanya uamuzi kuhusu maombi ya kurejeshwa kwa kodi ya ongezeko la thamani (**VAT refund**) katika kipindi cha muda wa siku thelathini

badala ya muda wa siku tisini. Uchambuzi wa Kamati ulionesha kwamba, jambo hilo linagusa masuala ya kodi na utendajikazi wa TRA, mambo ambayo kwa kawaida hurekebishwa kupitia Sheria ya Fedha.

(c) **Sheria ya Usimamizi wa Mahakama Sura ya 237.**

Sheria hii ilikusudiwa kuboresha Tume ya Utumishi wa Mahakama. Hata hivyo, Serikali iliomba kuondoa mapendekezo ya marekebisho ya sheria hii kwa lengo la kuifanyia kazi zaidi ikiwa ni pamoja na kuongeza masuala mengine, ombi ambalo Kamati lilikubaliana nalo.

(d) **Sheria ya Baraza la Vijana, Sura ya 441.**

Sheria hii ilikusudiwa kurekebishwa ili kuweka masuala mbalimbali yanayohusu vijana. Miongoni mwa masuala hayo ni Nafasi ya uanachama katika Baraza la Vijana kuwa ya hiyari kwa vijana waliochaguliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata na Baraza la Vijana la Kata kuwa na jukumu la kuishauri Kamati ya Maendeleo ya Kata kuhusu masuala yahusuyo vijana kwenye Kata husika, na kuanzisha Kamati ya Usimamizi wa Uchaguzi ya Baraza la Vijana ambapo wajumbe wake watateuliwa na Waziri kutoka katika taasisi mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba sheria hii inahitaji marekebisho makubwa ambayo kwa sehemu kubwa hayakujumuishwa kwenye Muswada. Kwa sababu hizo, Kamati na Serikali walikubaliana kuondoa marekebisho ya sheria hii ili kutoa nafasi kwa Serikali kuifanyia kazi zaidi. **Ni matumaini ya Kamati kuwa, Serikali itawasilisha mapendekezo ya marekebisho ya sheria hiyo kwa wakati.**

2.2 Uchambuzi kuhusu Sheria ambazo marekebisho yake yote yameridhiwa na Kamati

Mheshimiwa Spika, Kamati kupitia uchambuzi wake ilijiridhisha kuwa marekebisho yaliyopo kwenye sheria nane (8) yanajitosheleza.

Sheria hizo ni Sheria ya Nguvu za Atomu, Sura ya 188, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20, Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa Haramu, Sura ya 95, Sheria ya Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini, Sura ya 174, Sheria ya Chuo cha Uhasibu Arusha, Sura ya 240, Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1, Sheria ya Usimamizi wa Maabara Binafsi za Afya, Sura ya 136, na Sheria ya Alama za Biashara na Huduma, Sura ya 326. Uchambuzi wa Sheria hizo ni kama ifuatavyo: -

2.2.1 Sheria ya Nguvu za Atomu, Sura ya 188

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati unaonesha kwamba sheria hii inarekebishwa ili kupunguza idadi ya wajumbe wa Bodi kutoka kumi na tano (15) hadi tisa (9). Mwenyekiti wa Bodi atateuliwa na Rais, na wajumbe wengine nane watateuliwa na Waziri mwenye dhamana.

Mheshimiwa Spika, Kamati katika uchambuzi wake ilipendekeza uteuzi wa wajumbe wa Bodi hii ufanyike kwa njia ya ushindani kama ambavyo serikali imekuwa ikieleza hapa Bungeni. Hata hivyo, Serikali ilieleza kwamba, kutokana na mashirika kutofautiana majukumu, baadhi yake viongozi wake watatokana na mamlaka za uteuzi ikiwemo Tume ya Nguvu za Atomu. Licha ya Kamati kukubaliana na Serikali**, inashauri kwamba Serikali itoe amri (order) kupitia tangazo la Serikali litakaloainisha mashirika ya umma ambayo uteuzi wa viongozi utatokana na mamlaka za uteuzi**.

2.2.2 Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20

Mheshimiwa Spika, sheria hii inarekebishwa ili kuwezesha makosa ya jinai yanayotendwa na watumishi katika sekta ya umma na sekta binafsi kuhusiana na ajira zao kushughulikiwa kijinai pasipo kusubiri kumalizika kwa masuala ya kimadai au kinidhamu.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, jambo hili si geni hapa Afrika. Kamati ilifanya utafiti wa suala hili kwenye nchi nyingine za jumuiya ya madola ikiwemo **Uingereza,**

Uganda, Kenya na Afrika ya Kusini. Katika nchi hizo, sheria zinaruhusu kuanzisha shauri la jinai pasipokusubiri kumalizika kwanza kwa shauri hilo katika mlengo wa madai au nidhamu. Kwa utafiti huo, Kamati ilikubaliana na marekebisho hayo.

2.2.3 Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa Haramu, Sura ya 95

Mheshimiwa Spika, sheria hii inarekebishwa ili kuweka masharti yanayohusu masuala mbalimbali katika kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya. Miongoni mwa masuala hayo ni:-

(a) Kurekebisha fasili ya neno "**cannabis**" na maneno "**cannabis plant**" ili misamiati hiyo ijumuishe mbegu na majani ya mmea wa bangi na sehemu yoyote ya mmea huo mtawalia;

(b) kubanisha kosa la kukutwa au kusambaza mbegu za mmea wowote uliokatazwa na sheria hii bila ya kujali dhumuni la matumizi yake;

(c) kufuta na kuandika upya kifungu cha 12 cha Sheria ili kuipatia Mamlaka ya Kupamba na Dawa za Kulevya mamlaka ya kutunga kanuni (rules) kuhusu masuala ya dawa za kulevya. Baadhi ya masuala yanayoweza kuwekwa katika kanuni hizo ni usimamizi, utoaji wa leseni na vibali, uzalishaji, utengenezaji, umiliki, usafirishaji, uingizaji nchini, usafirishaji nje ya Tanzania Bara masuala yanayohusu matumizi ya koka, ununuzi, uuzaji, uhifadhi, usambazaji, uteketezaji au upatikanaji wa dawa za kulevya au dawa za kisaikolojia; na

(d) kuweka masharti ya kumwezesha Afisa aliyeidhinishwa wa Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya kutoa amri ya kufanya upekuzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikuwa na hoja mbalimbali zilizohusu marekebisho ya sheria hii ikiwa ni pamoja na kutaka mamlaka ya kutunga Kanuni yawekwe kwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya dawa za kulevya. Hata hivyo, maelezo ya Serikali

kwenye Kamati yalionesha kuwa Waziri anayo mamlaka ya kutunga Kanuni (**regulations**), na Mamlaka inayotajwa katika sheria hii itatekeleza jukumu la kuanzisha kanuni ndogo (**rules**). Baada ya mashauriano hayo, Kamati ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali.

2.2.4 Sheria ya Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini, Sura ya 174

Mheshimiwa Spika, sheria hii inarekebishwa katika masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupunguza idadi ya Wajumbe wa Baraza la Chuo watakaoteuliwa na waziri kutoka idadi isiyopungua wajumbe **10** na isiyozidi **15** na kuwa na idadi isiyopungua wajumbe **7** na isiyozidi **10**. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa marekebisho yanayopendekezwa yanawezesha sheria hii kuendana na wakati wa sasa wa muundo wa serikali, na hivyo kukubaliana na Serikali.

2.2.5 Sheria ya Chuo cha Uhasibu Arusha, Sura ya 240

Mheshimiwa Spika, sheria hii inakusudiwa kurekebishwa ili kukidhi masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na: -

(a) Kuongeza wigo wa kazi za taasisi, ambapo mbali na kufundisha kozi ya uhasibu, taasisi itaweza kufundisha kozi zinazohusu Sayansi ya usimamizi na mafunzo ya uanagenzi yaani "**management sciences and apprenticeships**"; na

(b) Kupunguza wajumbe wa Baraza la Chuo watakaoteuliwa na Waziri kutoka wajumbe wasiozidi **15** na wasiopungu **10** na kuwa wajumbe wasiozidi **10**, na kwamba wajumbe hao watashika madaraka hayo kwa kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja badala ya kusubiri uteuzi wao kutenguliwa kama sheria ilivyo kabla ya marekebisho haya.

Mheshimiwa Spika, Kamati katika uchambuzi wake, ilikubaliana na marekebosho haya kwa kuwa yanalenga kuboresha utendaji wa taasisi na kuendana na wakati. Aidha, **Kamati inashauri Serikali kutengeneza mwongozo unaoweka taratibu za uteuzi wa wajumbe**

wa Baraza kwa lengo la kuwezesha kupatikana kwa wajumbe wa Baraza kwa uwazi na kwa kuzingatia sifa stahiki.

2.2.6 Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1

Mheshimiwa Spika, sheria hii inarekebishwa ili kuruhusu sheria ndogo kutengenezwa kwa lugha iliyotumika katika sheria kuu husika. Uchambuzi wa Kamati umeonesha kwamba, marekebisho haya yatasaidia sheria na kanuni kueleweka kwa watumiaji wengi wa lugha ya kiswahili, na hivyo kurahisisha uzingatiaji wa masharti yake.

2.2.7 Sheria ya Usimamizi wa Maabara Binafsi za Afya, Sura ya 136

Mheshimiwa Spika, sheria hii inarekebishwa ili kuweka masharti kuhusu masuala mbalimbali katika usimamizi wa maabara binafsi za afya. Miongoni mwa masuala hayo ni:-

(a) Kuoanisha Sheria hii na Sheria ya Watoa Huduma ya Afya, Sura ya 48 ili kujumuisha watalaamu wa sayansi ya maabara ya afya, wateknolojia wa maabara ya afya na wasaidizi wa maabara za afya kuwa mojawapo ya watoa huduma ya Afya kwa mujibu wa Sheria ya Watoa Huduma ya Afya, Sura ya 48;

(b) Kuongeza adhabu kwa mtu atakayetenda kosa la kusimamia maabara binafsi ya afya bila ya kuthibitishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa sheria, kutoka kutozwa faini **isiyopungua shilingi elfu hamsini** na badala yake kutozwa faini **isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi shilingi milioni tano.** Aidha, kwa mtu atakayekutwa na hatia ya kosa la kuendesha maabara ya afya isiyosajiliwa, adhabu inaongezwa kutoka kutozwa faini **isiyopungua shilingi elfu ishirini na isiyozidi shilingi laki moja,** na badala yake kutozwa faini **isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi shilingi milioni tano"**; na

(c) Kuweka sharti linalomtaka mtalaam aliyeidhinishwa kuendesha maabara ya afya, kuwajibika katika usimamizi wa shughuli za kila siku za maabara na kuhakikisha utekelezaji wa

mfumo bora wa usimamizi, badala ya mtu huyo kukasimu jukumu hilo kwa mtu mwingine asiyeidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa mapendekezo ya sheria hii yamekuja wakati muafaka, kwa kuwa yanalenga kutatua changamoto ya kuibuka kwa wimbi la watu wanaotoa huduma za maabara za afya pasipokuwa na utalaam wa masuala hayo. **Ni ushauri wa Kamati kuwa, Serikali isimamie kikamilifu utekelezaji wa sheria hii ili kulinda afya za watu.**

2.2.8 Sheria ya Alama za Biashara na Huduma, Sura ya 326

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba marekebisho ya sheria hii yanagusa masuala mbalimbali ikiwemo:-

(a) Kuweka fasili za misamiati mipya na kuboresha fasili ya msamiati "**trade or service mark**". Msamiati huu unaboreshwa ili ujumuishe ishara zisizo onekana ikiwemo msimbo mpau (barcode);

(b) Kuanzisha usajili wa alama za biashara au huduma jumuishi **(collective mark).** Alama hii ni ile ambayo inauwezo wa kutofautisha bidhaa au huduma za watu ambao ni wanakikundi au wanachama wa chama fulani dhidi ya bidhaa au huduma za watu ambao si wanakikundi au wanachama wa chama hicho;

(c) Kuanzisha usajili wa alama ya uthibitisho **(Certification Mark)** na vigezo vyake; na

(d) Kuweka masharti kuhusu ulinzi wa alama maarufu au zinazojulikana (**well known marks)** na vigezo vyake.

2.3 Uchambuzi kuhusu Sheria ambazo marekebisho yake yameboreshwa na Serikali kutokana na maoni ya Kamati

Mheshimiwa Spika, Wakati Kamati inachambua Muswada huu, ilibaini kuwa jumla ya sheria tisa **(9)** marekebisho yaliyopendekezwa yalihitaji kuboreshwa. Sheria hizo ni Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa

Fedha Haramu, Sura ya 423, Sheria ya Majina ya Biashara, Sura ya 213, Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80, Sheria ya kampuni Sura ya 212, Sheria ya Usajili wa Hataza, Sura ya 217, Sheria ya Magereza, Sura ya 58, Sheria ya Taifa ya Huduma za Maktaba Tanzania, Sura ya 102, Sheria ya Bodi ya Utalii, Sura ya 364 na Sheria ya Utalii, Sura ya 65.

Mheshimiwa Spika, Kupitia maoni na ushauri wa Kamati, Serikali imeboresho Ibara mbalimbali za Muswada kupitia jedwali lake la marekebisho lililowasilishwa hapa Bungeni. Uchambuzi wa sheria hizo ni kama ifuatavyo: -

2.3.1 Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu, Sura ya 423

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba sheria hii inarekebishwa katika masuala mbalimbali. Baadhi ya masuala hayo ni: -

(a) Kufasili msamiati **"Domestic politically exposed person;"** kuwa lina maanisha mtu ambaye ndani ya nchi amepewa au amewahi kupewa hadhi maalumu ikiwa ni pamoja na kupewa majukumu makubwa ya kiuongozi kama vile Mkuu wa Nchi au wa Serikali, mwanasiasa mwandamizi, afisa mwandamizi wa serikali, mahakama au jeshi, mtendaji mkuu mwandamizi wa shirika la serikali, pamoja na kiongozi muhimu wa chama cha siasa, na pia inahusisha wanafamilia wake au washirika wake wa karibu. Aidha, kwa mtu mwenye hadhi ya namna hiyo anayetokea nchi za nje, msamiati unaotumika ni **"Foreign politically exposed person;**

(b) Kutofautisha mbinu za utambuzi na ugunduzi wa miamala shuku kwa wateja wa kigeni wenye hadhi maalumu na wale wa ndani wenye hadhi maalumu; na

(c) Kuainisha mazingira ambayo wataalamu walioteuliwa wanaofanya biashara isiyo ya kifedha ambao ni mawakili, makamishna wa viapo, wanasheria au wahasibu wanapaswa kutoa

taarifa ya miamala shuku kwa Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu (**Financial Intelligence Unit-FIU**).

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kamati kukubaliana na mapendekezo ya Sheria hii, ilikuwa na maoni mbalimbali yaliyolenga kuboresha marekebisho hayo. Baadhi ya masuala hayo ni: -

(a) Katika fasili ya misamiati **domestic and foreign politically exposed person,** mojawapo ya watu waliojumuishwa ni **kiongozi muhimu wa chama cha siasa**, yaani **important political party official**. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa msamiati huo haujafasiliwa katika sheria, na hivyo unaweza kuleta utata katika utekelezaji wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, utata huo unaweza kusababishwa kutokana na miundo ya kiuongozi ya vyama vya siasa nchini na katika bara la afrika kwa ujumla. Hali hiyo inatokana na ukweli kwamba kila kiongozi katika chama cha siasa (wa ngazi ya chini, kati au juu) ni muhimu. Umuhimu huo unatofautiana kulingana na majira ya nyakati.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na sababu hiyo, Kamati ilishauri msamiati huo ufasiliwe katika sheria. Serikali imekubali ushauri wa Kamati kwa kuboresha **Ibara ya 5** ya Muswada kupitia jedwali la marekebisho la Serikali.

(b) Kukosekana kwa fasili ya msamiati "**higher business relationship**" yaliyopo kwenye Ibara ya 7 ya Muswada. Ibara hiyo inaweka hatua zinazopaswa kuchukuliwa na mtoa taarifa ili kugundua miamala shuku kwa wateja wa ndani ya nchi wenye hadhi maalumu. Katika kuweka vigezo, endapo mteja wa ndani hali yake ya uhusiano wa kibiashara ni ya hatari kubwa yaani "**higher business relationship**", vigezo vinavyotumika kwa mteja huyo vinafanana na vigezo vya mteja anayetoka nje ya nchi mwenye hadhi maalumu. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba maneno "**higher business relationship"** ambayo ndio msingi wa Ibara hiyo

hayajafasiliwa katika sheria. Jambo hilo linaweza kuleta utata katika utekelezaji wa sheria hii, na hivyo kushauri maneno hayo yafasiliwe. Serikali imekubaliana na ushauri huo na kujumuisha fasili ya maneno hayo kwenye jedwali la marekebisho. Kukosekana kwa fasili ya msamiati miamala shuku yaani **suspicious transaction** katika sheria. Msamiati huo ni mojawapo ya msingi mkuu wa sheria hii. Hata hivyo, msamiati huo haujafasiliwa kwenye sheria. Jambo hilo linaweza kuleta utata katika utekelezaji wa sheria hii, na hivyo kushauri maneno hayo yafasiliwe. Serikali imekubaliana na ushauri huo na kujumuisha fasili ya maneno hayo kwenye jedwali la marekebisho.

(c) Ibara ya **18A** inayopendekezwa, imeweka masharti ambapo wataalamu mbalimbali wakiwemo mawakili na kamishna wa viapo wanawajibika kuripoti kwenye Kitengo cha Kupambana na Fedha Haramu (**FIU)** taarifa ya miamala shuku ya wateja wao. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba:-

(i) sharti hili likiwekwa moja kwa moja bila ya kuwekewa mipaka (exceptions), linaweza kusababisha masharti ya sheria hii yakakinzana na Ibara ya 16 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 juu ya kulinda haki ya faragha ikiwemo faragha ya taarifa za wateja mbalimbali ambazo mawakili wanazipata pindi wanapowahuduma wateja wao;

(ii) masharti ya Ibara hiyo yasipowekewa mipaka, yanaweza kukinzana na masharti ya Sheria ya Mawakili, Sura ya 341 ikisomwa kwa pamoja na Kanuni ya 30 na 31 ya Kanuni za Mawakili (Maadili na Mwenendo wa Kitaalamu), za Mwaka 2018, zilizotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 118 la tarehe 9 Machi, 2018. Sheria kupitia Kanuni hizo inawataka mawakili kutunza siri za wateja wao;

(iii) Pendekezo linaweza kukiuka kanuni za msingi (basic principles) katika taaluma ya uwakili inayohusu wakili kutunza siri za mteja wake. Misingi hiyo inatambulika duniani kote; na

(iv) Nchi nyingine zimetambua wajibu huo kwa mawakili, lakini zimeweka mipaka ya utekelezaji wake ili kutambua wajibu wa

mawakili kwa wateja wao ya kutunza siri. Miongoni mwa nchi hizo ni **Afrika ya Kusini, Rwanda, Uganda na Kenya.**

Mheshimiwa Spika, Kutokana na uchambuzi huo, Kamati ilishauri pendekezo hili liwekewe mipaka kwa kumlinda wakili pale ambapo atakuwa anatekeleza jukumu lake la msingi la kutoa ushauri wa kisheria kwa mteja wake tofauti na pale ambapo atakuwa anajihusisha moja kwa moja katika kazi za mteja wake zilizoainishwa kwenye sheria.

Mheshimiwa Spika, baada ya mashauriano ya mara kwa mara, Serikali imeweka mipaka kwa kuboresha **Ibara ya 8 ya** Muswada. Katika maboresho hayo, wakili au Kamishna wa viapo hatawajibika kuripoti taarifa za wateja wake kuhusiana na miamala shuku pale ambapo taarifa hizo zinahusiana na shauri lililopo mahakamani au pale ambapo kuripoti kwake kumezuiwa na sheria nyingine.

2.3.2 Sheria ya Majina ya Biashara, Sura ya 213

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, sheria hii inarekebishwa kwa malengo yafuatayo:-

(a) Kuweka fasili ya msamiati "**designated non-financial business professional**", yaani **"wataalamu wa biashara wasio wa kifedha"**. Msamiati huo unawajumuisha wafanyabiashara wa kasino (wakiwemo wa mtandaoni na meli), madalali wa mali isiyohamishika, wafanyabiashara wa madini na vito vya thamani, mawakili, **wataalamu huru wa kisheria**, wahasibu na watoa huduma za kampuni; na

(b) Kuweka sharti ili kuwaruhusu watoa taarifa kama walivyoainishwa katika Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu, Sura ya 423 kupata taarifa za wamiliki manufaa kutoka kwa Msajili.

Mheshimiwa Spika, licha ya Kamati kukubaliana na marekebisho haya, uchambuzi wake ulibaini kuwa mapendekezo yameainisha

watalaam wa sheria wanaotambulika kwa jina la "**other independent legal professional".** Katika tasnia ya sheria, watalaam wa aina hii hawatambuliki kisheria.

Kamati ilishauri maneno hayo yaondolewe kwenye Muswada na badala yake yawekwe maneno "**commissioner for oaths**" kwa kuwa watalaam hao ndio wanaotambulika kisheria. Serikali imekubaliana na ushauri huo na kuboresha **Ibara ya 14** ya Muswada**.**

2.3.3 Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba marekebisho ya sheria hii yanahusu masuala mbalimbali. Baadhi ya masuala hayo ni:-

(a) Kumpa Waziri mwenye dhamana mamlaka ya kutunga kanuni katika masuala ya anga ikiwemo kuweka taratibu za Mamlaka ya anga kukamata au kuingilia ndege za kiraia, mbinu za mawasiliano na hatua za kulinda usalama wa ndege na watu waliomo ndani yake;

(b) Kuweka utaratibu wa Uchunguzi wa Ajali na Matukio ya Ndege ikiwa ni pamoja na kutambua Kitengo cha Uchunguzi wa Ajali na Matukio ya Ndege (**Aircraft Accident and Incident investigation Unit-AAIU**); na

(c) Kuweka wajibu kwa mtu yeyote au **AAIU** ya kutunza siri zinazohusu taarifa na nyaraka zozote zinazohusu uchunguzi unaofanywa na **AAIU**.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikuwa na maboresho ya sheria hii. Kutokana na maelezo yaliyotolewa na Serikali, Kamati iliridhia maboresho hayo kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho la serikali.

2.3.4 Sheria ya Kampuni, Sura ya 212

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, sheria hii inarekebishwa ili kukidhi masuala mbalimbali yanayohusu kampuni. Miongoni mwa masuala hayo ni:-

(a) Kuweka fasili za misamiati **"nominee", "nominator" na "nominee director"** kwenye sheria. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, misamiati hiyo inatokana na sheria hii kutambua na kuazisha suala la wateule wanaosimama badala ya wanahisa halisi au wakurugenzi halisi wa kampuni. Jambo hili ni mojawapo ya maeneo mapya yanayoibukia katika usimamizi wa kampuni;

(b) Kufuta na kuandika upya kifungu cha 8 cha Sheria ili katiba ya kampuni (MEMART) ibainishe malengo mahsusi pekee ya kibiashara ambayo kampuni inanuia kufanya mara baada ya kusajiliwa, badala ya kubainisha malengo mahsusi na malengo ya jumla kama sheria ilivyo kwa sasa;

(c) Kuweka sharti kuwa, Kampuni itakayoshindwa kubadili jina lake baada ya kuamriwa na Msajili wa Kampuni ndani ya muda wa wiki sita, itachukuliwa kuwa imepoteza hadhi yake ya usajili na itafutwa kwenye daftari la rejesta;

(d) Kuongeza takwa la msajili kuwa na rejesta ya mwanahisa mteule. Rejesta hiyo itapaswa kuwa na maelezo kama yatakavyoainishwa katika kanuni; na

(e) Kumpa Msajili wa Kampuni au afisa wake mamlaka ya kukagua taarifa mbalimbali za Kampuni kwenye ofisi au mahala kwingine zinapohifadhiwa. Ukaguzi huo unaweza kufanyika kwa kutoa notisi au bila notisi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba baadhi ya marekebisho ya sheria hii yalihitaji maboresho kwa lengo la kuhakikisha sheria inaendana na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050

ikiwa ni pamoja na kuchochea mazingira ya biashara nchini. Baadhi ya maboresho yaliyopendekezwa na Kamati ni:-

(i) Kusiwekwe ulazima kwa Kampuni kusajiliwa endapo tu Katiba ya Kampuni iliyowasilishwa kwa ajili ya usajili itabainisha malengo mahsusi pekee ya biashara ambayo Kampuni inakusudia kufanya mara baada ya kusajiliwa.

Mheshimiwa Spika, sababu za Kampuni kuwa na pendekezo hili kunatokana na msingi wa kisheria unaotambulika duniani na kwa muda mrefu kuhusu hadhi ya kampuni mara baada ya kusajiliwa. Hadhi hiyo inaeleza kuwa, Kampuni ikishasajiliwa inapata hadhi ya kuwa mtu (**artificial person),** na hivyo inaruhusiwa kufanya biashara yoyote halali kwa mujibu wa sheria. Biashara hiyo si lazima itajwe moja kwa moja kwenye Katiba ya Kampuni. Aidha, kuweka sharti kwamba Kampuni haitapaswa kufanya biashara ambayo haijaainishwa katika Katiba yake, na endapo itataka kufanya hivyo itapaswa kufanya marekebisho kwenye Katiba yake, licha ya kukiuka msingi mkuu wa sheria unaohusu hadhi ya Kampuni, lakini pia pendekezo hili linaweka ugumu kwa Kampuni kuanzisha biashara mbalimbali kadiri ya fursa zitakavyojitokeza. Kwa sababu hizo, Serikali imekubaliana na ushauri wa Kamati na kufuta **Ibara ya 29** ya Muswada katika jedwali la marekebisho.

(ii) Kuondoa mapendekezo yaliyopo kwenye **Ibara ya 31** ya Muswada yanayoweka sharti la Kampuni kufutiwa usajili wake endapo itakashindwa kubadili jina lake baada ya kuamriwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati ulionesha kuwa, jambo hili ni vigumu kujitokeza endapo mamlaka ya usajili (BRELA) itatekeleza jukumu lake ipasavyo na kwa kuzingatia sheria, Kanuni na miongozo iliyopo. Aidha, uchambuzi zaidi ulibaini kwamba, halitakuwa jambo jema Kampuni kuadhibiwa kutokana na makosa ambayo haikuyafanya. Serikali imekubaliana na maoni ya Kamati na hivyo kufuta **Ibara ya 31** kupitia jedwali la marekebisho la Serikali.

(iii) Msajili au Maafisa wake kukagua taarifa mbalimbali za Kampuni kwenye ofisi au mahala kwingine zinapohifadhiwa baada ya kutoa notisi au bila notisi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipendekeza kuboreshwa kwa pendekezo hili, kwa lengo la kupunguza mamlaka za ukaguzi kwenye maeneo ya biashara na sehemu mbalimbali za uzalishaji. Hata hivyo, Serikali ilieleza kuwa, pendekezo hili halilengi kukagua biashara au maeneo ya uzalishaji bali nyaraka pekee za Kampuni. Vilevile ilielezwa kuwa, uwepo wa sharti hili utasaidia kutatua changamoto zinazohusu udanganyifu na ukiukwaji wa sheria ambazo kwa sasa zimeendelea kukithiri.

Mheshimiwa Spika, licha ya Kamati kukubaliana na Serikali, ilipendekeza kutengenezwe Kanuni itakayoweka utaratibu wa utekelezaji wa sharti hili. Aidha**,** Kamati ilishauri kwamba, sheria ielekeze kwamba maafisa watakaotekeleza jukumu hili, wawe ni wale tu walioruhusiwa badala ya jukumu hilo kutekelezwa na afisa yoyote wa **BRELA**. Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati kwa kuboresha Ibara ya **35** ya Muswada kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho.

2.3.5 Sheria ya Usajili wa Hataza, Sura ya 217

Mheshimiwa Spika, Kamati kwa sehemu kubwa ilikubaliana na mapendekezo ya marekebisho ya sheria hii. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, pendekezo la **Ibara ya 84** ya Muswada linalompa Waziri mamlaka ya kuziondolea ulinzi wa kisheria kwa muda usiozidi miaka kumi baadhi ya vumbuzi zinazoweza kusajiliwa kama hataza zinazohusu bidhaa au mchakato wa uzalishaji wa bidhaa linakiuka misingi ya kikatiba ikiwa ni pamoja na mvumbuzi kutolindwa na sheria na kuweza kuporwa haki yake ya uvumbuzi.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha haki za wavumbuzi zinalindwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania hususani haki ya kulindwa na sheria, haki ya kumiliki mali ikiwemo miliki bunifu, haki ya kupata ujira kutokana na kazi halali ikiwemo kazi za ubunifu

na uvumbuzi, Kamati ilishauri pendekezo hili liondolewe kwenye Muswada. Serikali imekubaliana na ushauri huo kwa kufuta **Ibara ya 84** ya Muswada kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho la serikali.

2.3.6 Sheria ya Magereza, Sura ya 58

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, pamoja na masuala mengine, marekebisho yaliyoletwa katika sheria hii yanaakisi mtazamo wa kisasa wa magereza kuwa sehemu ya mafunzo badala ya sehemu ya mateso. Baadhi ya masuala yanayoonesha uelekeo huo yaliyopo kwenye Muswada ni yafuatayo:-

(a) Kubainisha kwa uwazi majukumu makuu na huduma zinazotolewa na Magereza kuwa ni Ulinzi na salama wa wafungwa **(safe custody);** Huduma za mahabusu **(remand services);** Urekebishaji wa wakosaji **(rehabilitation);** na Kuwezesha urejeo wa wakosaji katika jamii **(reintegration);**

(b) Kuweka mfumo wa usimamizi wa magereza katika ngazi za mikoa na wilaya;

(c) Kulipa mamlaka Jeshi la Magereza kuanzisha programu za urekebishaji wa wafungwa ikiwemo elimu, mafunzo ya ufundi, huduma za kiroho na huduma za msaada wa kisaikolojia;

(d) Kuweka masharti ya msaada kwa wafungwa baada ya kuachiwa huru ikiwemo kuunganishwa na taasisi za Serikali na huduma za kijamii; na

(e) Kuongeza jukumu kwa Waziri mwenye dhamana la kutengeneza kanuni kuhusu utaratibu wa kurekebisha wafungwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sehemu kubwa Kamati ilikubaliana na marekebisho ya sheria hii. Hata hivyo, Kamati ilibaini kwamba, **Ibara ya 98** inayofuta neno **young prisoner**, na badala yake kuweka neno "**child prisoner**", pendekezo hili halikuzingatia mikataba ya kimataifa inayohusu watoto pamoja na sheria ya mtoto, Sura ya 13. Uchambuzi ulionesha kwamba, kifungu cha 120(1) Cha Sheria ya Mtoto kimekataza mtoto kufungwa gerezani, na badala yake kupewa adhabu mbadala ikiwa ni pamoja na kupelekwa shule iliyothibitishwa (**approved school**) ili kumrekebisha tabia.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na sababu hizo, Kamati ilishauri pendekezo hili liondolewe kwenye Muswada. Serikali imekubaliana na ushauri wa Kamati kwa kurekebisha Ibara ya 98 ili kuondoa neno "**child prisoner"** lililopo kwenye Muswada kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Spika, licha ya Kamati kukubaliana na kupongeza marekebisho ya sheria ya magereza, **Kamati inashauri Serikali iweke mkakati utakaohakikisha marekebisho hayo yanatekelezwa kikamilifu kwa magereza kuwa chuo cha mafunzo, kwani uzuri wa sheria si katika masharti yake pekee, bali katika utekelezaji wa masharti hayo**. Aidha, kwa wafungwa ambao watapata ujuzi wa kutosha katika kazi mbalimbali, **ni muhimu wakapewa vyeti vya kufuzu mafunzo hayo ili ujuzi wake uweze kutambulika pindi watakaporejea kwenye jamii**.

2.3.7 Sheria ya Huduma za Maktaba Tanzania, Sura ya 102

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba marekebisho ya sheria hii yanalenga kuboresha huduma za maktaba nchini, ikiwa ni pamoja na kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Baadhi ya masuala hayo ni:-

(a) kuweka fasili mpya ya msamiati **"book"** yaani kitabu. Fasili mpya inaongeza wigo wa vitu au taarifa ambazo zinatambulika kuwa ni kitabu ikiwemo taarifa

zilizochapishwa au zisizochapishwa zinazotumika kwenye maktaba au katika kituo chochote cha nyaraka;

(b) Kuweka masharti ya kuiwezesha Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania kuweza kutoa huduma ya kusimamia mitihani ya ngazi ya shahada na kutoa cheti cha shahada;

(c) Kuiwezesha Bodi ya Huduma za Maktaba kusimamia masuala ya maadili katika utekelezaji wa majukumu yake kwa ajili ya ustawi wa jamii; na

(d) Kuongeza wigo wa kazi za kiuandishi kwa kujumuisha kazi zilizopo katika mfumo wa kielekroniki, mfano kazi zilizopo katika mfumo wa sauti ya kuonekana (audio-visual), mifumo ya kidijitali na filamu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kamati kukubaliana na marekebisho yaliyowasilishwa, uchambuzi ulionesha kuwa pendekezo la **Ibara ya 128** ambalo linaipatia Bodi kusimamia masuala ya maadili katika utekelezaji wa majukumu yake kwa ajili ya ustawi wa jamii, jukumu hilo limejificha na hivyo si rahisi kueleweka. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, uandishi uliotumika katika sheria sio wa kisasa unaotaka aya za vifungu vya sheria kuwa fupi na zinazojitosheleza. Hali hii inatokana na ukweli kwamba, sheria hii ilitungwa mwaka **1975**, na mara ya mwisho ilirekebiswa **mwaka 1995**. Ili kurahisisha uelewekaji wa sharti hilo, Kamati ilishauri Serikali ifanya maboresho ya kiuandishi. Ushauri huo umekubaliwa na serikali.

Mheshimiwa Spika, licha ya serikali kuboresha Ibara hiyo, **Kamati inashauri Serikali kuleta Muswada wa kufuta na kutunga upya sheria hii, ili uandishi wake uendane na matakwa ya kisasa, na hivyo kurahisisha uelewekaji wake kwa wananchi. 2.3.8 Sheria ya Bodi ya Utalii, Sura ya 364 na Sheria ya Utalii, Sura ya 65**

Mheshimiwa Spika, Katika uchambuzi wa marekebisho haya, Kamati imebaini kwamba dhumuni kuu la kurekebishwa kwa sheria ya Bodi ya Utalii ni kuiongezea mawanda ya kazi Bodi ya Utalii ili iweze

kufanya kazi nyingi za kiutendaji katika sekta ya utalii ambazo kwa sasa kazi hizo zinatekelezwa na Wizara ya Utalii kwa mujibu wa sheria ya Utalii, Sura ya 65. Lengo ni kuhakikisha Bodi ya Utalii inawajibika na masuala ya utendaji katika sekta ya utalii, na Wizara ya Utalii inabaki na jukumu la kusimamia sera zinazohusu sekta ya utalii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii ambayo sasa inatenganisha majukumu ya kiutendaji na majukumu ya kisera na hivyo kuweka mgawanyo wa kazi katika misingi inayokubalika. Misingi hiyo ni pamoja na Wizara kusimamia sera, huku taasisi na mashirika ya umma yakibaki na usimamizi wa shughuli za kiutendaji. **Ni matumaini ya Kamati kuwa, Serikali itaendelea kuchukua hatua kama hizi katika wizara na taasisi nyingine ili kuendeleza misingi ya utawala bora.**

Mheshimiwa Spika, licha ya Kamati kuridhia marekebisho hayo, uchambuzi wake ulionesha kwamba baadhi ya maeneo yalihitaji maboresho kama vile:-

(a) Uteuzi wa Wajumbe wa Bodi ya Utalii. Ibara ya 137 ya Muswada inafuta uteuzi wa uwakilishi wa wajumbe wa Bodi ya Utalii waliopo na kuweka uteuzi kutokana na uwakilishi mwingine. Hata hivyo, marekebisho hayo yanaondoa uwakilishi wa moja kwa moja ya wajumbe wa Bodi wanaotokana na majukwa na mashirikisho ya sekta binafsi katika sekta ya utalii.

Mapendekezo yaliyopo, yanaweza kusababisha sekta binafsi ikakosa uwakilishi katika ujumbe wa Bodi. Ili kuendana na malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 inayosisitiza sekta binafsi kushirikishwa kikamilifu, Kamati ilishauri sehemu hii iboreshwe kwa kutambua uwakilishi wa shirikisho la vyama vya utalii. Serikali imekubali ushauri huo na kuboresha Ibara ya 137 ya Muswada kupitia jedwali la marekebisho la Serikali.

(b) Uteuzi wa wajumbe wa Kamati ya Kitalaamu ya Kumshauri Waziri mwenye dhamana ya Utalii. Katika marekebisho

haya Kamati imependekeza maboresho katika masuala mawili kama ifuatavyo:-

(i) Sifa za uteuzi wa Mwenyekiti wa Kamati hii hazijaainishwa, na hivyo kuweka uwezekano wa kuteuliwa kwa Mwenyekiti asiyekidhi vigezo. Kamati ilipendekeza maboresho ili Mwenyekiti wa Kamati hii awe na utalaam na uzoefu katika masuala ya utalii, na hivyo kumuwezesha kutoa ushauri wa kitalaamu pamoja na wajumbe wenzake. Serikali imekubaliana na ushauri wa Kamati kwa kuboresha **Ibara ya 153**, na sasa Mwenyekiti atatokana na sekta binafsi na atapaswa kuwa na uzoefu wa miaka isiyopungua kumi katika sekta ya Utalii.

(ii) Wajumbe wengine wa Kamati ya Kitaalamu ya ushauri wanatokana na taasisi za serikali. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, jambo hili linakinzana na matakwa ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050. Vilevile, wajumbe kutoka serikalini wanayo nafasi ya kumshauri Waziri pasipokusubiri kikao cha Kamati Maalumu ya Ushauri, kwa kuwa ni sehemu ya majukumu yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, Kwa sababu hiyo, Kamati ilishauri Kamati hii ijumuishe wajumbe kutoka sekta binafsi. Serikali imeridhia ushauri wa Kamati kwa kujumuisha wajumbe watatu kutoka mashirikisho matatu katika sekta ya utalii kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho la Serikali.

SEHEMU YA TATU

3.0 USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, pamoja na maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kwenye Ibara mbalimbali za Muswada ambayo kwa sehemu kubwa yamekubaliwa na Serikali kwa kuyazingatia katika jedwali la marekebisho, Kamati ina maoni ya ujumla kama ifuatavyo:-

(i) Baada ya Kamati kuishauri serikali kuleta Muswada muhsusi unaohusu Sheria ya Baraza la Vijana, Sura ya 441 Kamati inasisitiza kuwa, Serikali ihakikishe inachukua hatua za kuleta mapendekezo ya maboresho hayo mapema ili vijana wanufaike na uwepo wa sheria inayokidhi maslahi yao.

(ii) Marekebisho ya Sheria ya Chuo cha Uhasibu Arusha na Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini yanaweka muda wa uteuzi wa Wajumbe wa Baraza la Chuo kukaa madarakani kuwa miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kimoja. Hata hivyo, sifa za uteuzi hazijatajwa katika sheria. Serikali itengeneze Kanuni (rules) zitakazoweka uwazi katika uteuzi na sifa za uteuzi.

(iii) Sheria ya Usimamizi wa Maabara Binafsi za Afya imerekebishwa ili kuhakikisha ufanisi katika usimamizi na uendeshaji wa maabara binafsi za afya. Kumejitokeza wimbi la watu wasiokuwa na utalaamu wa maabara au afya ambao wanatoa huduma za afya kwa binadamu. Ili kukomesha hali hiyo, Serikali ihakikishe inasimamia kikamilifu masharti ya sheria hii kwa lengo la kulinda afya za watu.

(iv) Serikali ilishatoa ahadi Bungeni kuwa upatikanaji wa viongozi na wajumbe wa Bodi katika mashirika ya umma utaanza kufanyika kwa njia ya ushindani. Hata hivyo, bado serikali imeendelea kuleta marekebisho ya sheria ambayo haya akisi ahadi hii. Kwa kuwa Serikali imeeleza kuwa baadhi ya mashirika upatikanaji wa viongozi na wajumbe wa Bodi hautakuwa wa ushindani kama ilivyo kwenye Tume ya Nguvu za Atomu, Serikali itoe tangazo kupitia Gazeti la Serikali litakalotaja mashirika ambayo upatikanaji wa viongozi wake hautokani na ushindani.

(v) Sheria ya Magereza imeboreshwa ambapo pamoja na mambo mengine, wafungwa watapewa ujuzi mbalimbali

ili waweze kurejea kwenye jamii wakiwa watu wema. Wafungwa ambao watakidhi vigezo vya ufundi na ujuzi katika fani zitakazofundishwa, wapewe vyeti vya kufuzu mafunzo hayo ili waweze kutambulika na kupewa kazi walizojifunza pindi watakaporejea kwenye jamii.

(vi) Baadhi ya Sheria zilitungwa zamani, mtindo wa uandishi wake ulikuwa wa kimapokea zaidi (mtindo wa kale) ikijumuisha matumizi ya aya ndefu, sentensi ndefu, matumizi ya kauli kutendwa (passive voice) badala ya kauli tenda (active voice), na matumizi ya lugha ya kale (archaic language). Mojawapo ya sheria hizo ni sheria ya Huduma za Maktaba iliyotungwa mwaka 1975.
Kwa sasa, dunia imebadili uelekeo na inachagiza uandishi wa kisasa wa sheria unaotumia lugha nyepesi (plain language) ambayo inayoeleweka kwa urahisi kwa walengwa. Ili kuendana na mabadiliko ya kidunia, Serikali ilete mapendekezo ya kuzifuta na kuzitunga upya sheria zilizoandikwa kwa mtindo wa kizamani ili walengwa waweze kuzielewa kwa urahisi.

(vii) Serikali iendelee kuchukua hatua ya kurekebisha sheria ili kuweka misingi ya utawala bora na mgawanyo wa kazi kwa kutenganisha kazi ya kusimamia sera na kazi ya kusimamia utendaji wa siku kwa siku kama ilivyofanya kwenye sheria ya Bodi ya Utalii na Sheria ya Utalii.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha kwa kukushukuru wewe binafsi Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mhe. Daniel Baran Sillo, Mb na Naibu Spika kwa kuendelea kuliongoza vema Bunge lako Tukufu. Aidha, kwa dhati napenda kumshukuru na kumpongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Mhe. Hamza Johari, Mb kwa

ushirikiano mkubwa alioipatia Kamati yetu, kuandaa Muswada huu pamoja na kuwa tayari kusikiliza, kupokea na kuufanyia kazi ushauri uliotolewa na Kamati.

Vilevile, namshukuru Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Juma Zuberi Homera, Mb, Khamis Mussa Omar, Mb Waziri wa Fedha, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Zainab Athman Katimba, Mb, Mhe. Mhandisi Mshamu Ali Munde, Mb na Naibu Waziri wa Fedha na Mhe. Laurent Deogratius Luswetula, Mb Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano wao mkubwa walioipatia Kamati wakati wa uchambuzi wa Muswada huu.

Vilevile, Kamati inapenda kuwashukuru watendaji wote wa Serikali wakiongozwa na Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali ***(CPD)*** Ndg. Onorius Njole kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha kuchambua Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza wajumbe wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kupitia na kuchambua Muswada huu na hatimaye kukamilika kwa Taarifa hii. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mb- **Mwenyekiti**
2. Mhe. Edwin Enosy Swalle, Mb - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Aziza Sleyum Ally, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Asha Hussein Saleh, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Esther Edwin Malleko, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Maryam Ussi Yahya, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Nassoro Rashid Nassoro, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Dkt. Neema Peter Majule, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Nyamizi Simon Mhoja, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mb - Mjumbe

15. Mhe. Sikudhani Yasini Chikambo, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Timida Mpoki Fyandomo, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Dkt. Yahaya Esmail Nawanda, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Yohana Stephen Msita, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Zena Maulid Katambo, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Hussein Nassoro Amar, Mb - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, nimshukuru Ndg. Baraka Leonard, Katibu wa Bunge kwa niaba ya Watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, inaliomba Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments)) Bill, 2026*)** pamoja na Marekebisho yake, kama ulivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mb
MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA
1 SEPTEMBA, 2026

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti kwa kuwasilisha taarifa kwa ufasaha na umakini mkubwa, hongera sana Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti kwa niaba ya Mheshimiwa Mwenyekiti.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupokea maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye ndiye mtoa hoja, na baada ya kupata maoni na mapendekezo ya Kamati yetu, tunaingia kwenye sehemu ya mjadala.

Kwa mamlaka ya kiti, tunaongeza muda hadi tumalize shughuli iliyokuwa mbele yetu. Tutaanza na Mheshimiwa Esther Edwin Malleko atafuatiwa na Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi, Mheshimiwa Nyamizi Simon Mhoja, ajiandae.

MHE. ESTHER E. MALLEKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika Muswada wa maboresho ya sheria mbalimbali ambazo zimeletwa kwetu wakati huu. Nitajikita moja kwa moja kwenye kuchangia katika Sheria ya Bodi ya Utalii Sura ya 364 na Sheria ya Utalii Sura ya 65.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza sana Serikali kwa marekebisho ya sheria hizi ambazo zimeweza kutenganisha majukumu ya kitaasisi ambapo majukumu ya Bodi ya Utalii yatakwenda kwenye kufanya majukumu ya kiutendaji na majukumu ya kisera yatabaki kwenye Wizara ya Utalii. Basi kutokana na mgawanyiko huo wa hatua hizo muhimu ambazo zimefanyika, majukumu haya yataenda kuzingatia masuala ya misingi ya utawala bora. Marekebisho haya muhimu yanaweka dira na maendeleo ya dira ambayo tunaenda kuifikia ya 2050.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanya maboresho hayo, sisi Wajumbe wa Kamati tuliweza kuishauri Serikali katika yale maboresho ambayo wameyafanya ambayo yanaweza kuleta tija kubwa katika suala zima la utalii katika nchi yetu kwa sababu, kama dira inavyoelekeza, Wizara hii ya Utalii ndiyo itaenda kuingiza pato kubwa katika nchi yetu, lakini pia itaenda kuongeza ajira katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyojua Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi imeweka ajira milioni nane na sisi tunategemea ajira hizo zitatokana pia na sekta hii ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunakwenda moja kwa moja kwenye kuishauri bodi baada ya kupata mamlaka hayo kamili. Kwa sasa bodi inaenda kuwa na nguvu kubwa ambapo itaenda

kuitangaza Tanzania Kimataifa. Kutokana na kazi hiyo kubwa tunategemea wataenda kuingiza watalii wengi zaidi, na watatengeneza masoko mengine mapya tofauti na yale tuliyokuwa nayo mwanzoni ili watalii wengi zaidi waweze kuja nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kubwa ambalo Kamati iliona na kushauri, tumeona kwamba baada ya kupewa majukumu haya ya kiutendaji bodi itaweza kuongeza ufanisi na kazi ya kiutendaji. Pia, bodi itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi ya kibiashara, pamoja na kiutendaji bila kukwama kwenye masuala au taratibu zile za Kiserikali ambazo mwanzoni zilikuwa zinawakwamisha kufikia malengo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kutokana na majukumu hayo waliyopewa, itaenda kupunguza mwingiliano wa majukumu kwa sababu kila idara itakuwa inafanya majukumu yake, kwamba sasa Wizara itasimamia masuala ya kisera, lakini Bodi itasimamia masuala ya kiutendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua sasa Bodi inaenda kuwa mtekelezaji, na bodi hii itapimwa kwa yale mambo kwa kazi kubwa watakayoenda kuifanya baada ya kupewa jukumu hili muhimu. Sisi tunategemea baada ya kupewa jukumu hili muhimu, Wizara ya Utalii itaenda kuwa wasimamizi wa kuangalia ni namna gani bodi hii inaenda kutimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tutaenda kuipima bodi hii kwa majukumu watakayokuwa wanaenda kuyafanya na tutawapima kwa watalii watakavyoongezeka nchini kujua ni kiasi gani na asilimia ngapi ya watalii wataongezeka nchini? Pia, tutawapima kwa mapato yanayoongezeka nchini kutokana na Wizara hii ya Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tutawapima ni watalii kiasi gani wameingia nchini, wanakaa kwa siku ngapi? Pia, katika kukaa nchini, hapa tunaitaka Bodi iende kutengeneza kanda za kitalii ili

wale watalii wanapofika nchini waweze kuzunguka katika maeneo mbalimbali tofauti, na wakae nchini kwetu siyo chini ya siku 10 ili tuweze kupata fedha nyingi za kigeni, na pia waweze kutembelea vivutio vingi vilivyopo nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka kujua matumizi ya watalii hawa kwa siku yatakuwa ni kiasi gani ili tuweze kupima weledi na kazi kubwa inayoenda kufanywa na bodi hii. Kubwa zaidi tunataka kuona ni ajira ngapi zitazalishwa kutokana na majukumu waliyopewa hii bodi kwa sababu tunataka kuona ajira zinapatikana kwa Watanzania kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaishauri Bodi hii iweze kuongeza vivutio na kuvitangaza kwa ukubwa zaidi. Ni matumaini ya Kamati kwamba Serikali itaendelea kuchukua hatua kama hizi kwa Wizara na taasisi nyingine ili kuendelea kuweka misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kamati iliona kuna maeneo mengine ya kufanya maboresho ambayo ni katika namna ya kuteua wale Wajumbe ambao watakwenda kwenye Bodi ya Utalii. Kutokana na Ibara ya 137 ya Muswada huu, wale Wajumbe ambao ni wawakilishi kutoka kwenye sekta binafsi walikuwa hawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Kamati tulishauri kwamba wale Wajumbe ambao wanatoka kwenye sekta binafsi waweze kuingizwa kwa sababu wao wanajua mambo mengi yanayoendelea kwenye mambo ya utalii kwa sababu siku zote wao ndio wanafanya biashara hii. Kwahiyo, wanajua changamoto zinazotokana na sekta hii ya utalii, wanajua ni wakati gani au ni changamoto gani wanakutana nazo katika gharama za uendeshaji, ushindani wa Kimataifa uliopo na wanajua mahitaji sahihi ya watalii.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Esther Malleko.

MHE. ESTHER E. MALLEKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi, atafuatiwa na Mheshimiwa Nyamizi Simon Mhoja, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally ajiandae.

MHE. ABDULLAH ALI MWINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia wasaa huu na mimi kuchangia kwenye Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026 *(The Written Laws Miscellaneous Amendment Bill, 2026)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ningependa kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutujalia afya na uzima na kutujalia kufika hapa leo na kuweza kuchangia katika Muswada huu muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ninapenda kuchukua fursa hii kuishukuru sana Serikali pamoja na Mwanasheria Mkuu. Imekuwa rahisi sana kufanya naye kazi kama Mjumbe wa Kamati. Tunapata ushirikiano mkubwa sana. Ukiangalia mzigo wa sheria hizi, tumepata sheria 21 ambazo zilikuwa zinarekebishwa, lakini juu ya kazi yote kubwa hiyo kwa sehemu kubwa 90% na zaidi tulikubaliana ndani ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi katika uchangiaji wangu ningependa kuchangia *general principles* halafu nitagusa *specific* kwenye eneo la *BRELA* na urekebishaji wa Sheria za Kampuni. *General principles:* sheria yoyote inayokuja kwenye Kamati yetu iwe sheria mpya au urekebu wa sheria kuna misingi ambayo tunaitizama na tunaipitia, kupitia kusimamia na kuzingatia misingi hiyo. Tunatizama sera, tunazingatia Ilani na tunazingatia *Vision 2050.*

Mheshimiwa Naibu Spika, *legislative process.* Njia ya kutengeneza sheria *is a means to an end.* Ni njia ya kufikiria kule ambako tunataka kufika na siyo *destination* yenyewe. Hutengenezi

tu sheria ili uwe na utaratibu fulani, hapana. Sheria lazima ziende kule ambako tunataka kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hili Bunge la kwanza ambalo limeanza kutekeleza *Vision 2050,* hizi sheria zote tulizitazama kwa mizania na kwa miwani hiyo. Ni muhimu sana sheria inayokuja izingatie yale ambayo tunataka kuyatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Vision 2050* itatekelezwa 70% na sekta binafsi, 30% ndiyo inatekelezwa na Serikali. Ninamshukuru Mheshimiwa Waziri, yupo hapa ametuelekeza na ametueleza vizuri sana katika hilo. Sasa ili tufike huko, mfumo mzima wa biashara na mfumo mzima wa sekta binafsi *(private sector)* lazima kazi zao zifanywe kwa njia ambayo ni rahisi ili tuweze kufikia huko tunakofika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tufikie uchumi wa dola trilioni moja, lazima sekta binafsi ichangie kwa kiwango kikubwa. Sekta binafsi *engine* yake, (kiini cha sekta binafsi) ni biashara ndogo na biashara za kati. Sasa kila sheria inayopita macho yetu na miwani yetu inatazama yale mambo mahususi ya kitaalamu wanayotaka kurekebisha, lakini kwa mapana yake hii sheria itatufikishaje kule? Inarahisisha biashara? Inarahisisha *private sector?* Inaimarisha soko huria? Kwa mantiki hiyo, na kwa utangulizi huo, nirudi kwenye Sheria ya Kampuni hususan uendeshaji na *registration* ya kampuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kwetu taasisi ambayo ni ndiyo mhifadhi *(depository)* wa taarifa za makampuni ni *BRELA*. Adui mkubwa wa ufisadi, adui mkubwa wa ujangili, adui mkubwa wa utakatishaji fedha ni uwazi. Msingi wa kuweka *BRELA* ni kuhakikisha kila kampuni vielelezo vyake vyote viko wazi, na ni sekta moja na taasisi moja muhimu sana. Vilevile, uendeshaji wa *BRELA* unaweza ukawa kikwazo kwa sekta binafsi hasa hizi kampuni ndogo na kampuni za kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa lazima tuwe na mizania, *enforcement* i-*balance* na uwezeshaji ili zile kampuni zikue, sasa kwa sehemu kubwa kampuni kubwa na *requirements* za *BRELA*

zinaendana. Kampuni kubwa zina *resources* za kufanya *returns* kwa wakati mzuri, lakini *BRELA* hivi karibuni wamekuwa wanaongeza ukiritimba hasa katika *small and medium enterprises.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kivipi? Sheria ya Kampuni inaruhusu kampuni ndogo ndogo au kampuni kufanya mambo mahususi na kufanya mambo ambayo yana ujumla. Kwa mfano, mimi ninaweza nikawa *consultant*...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Hitimisha Mheshimiwa, muda wako umeisha.

MHE. ABDULLAH ALI MWINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi ninaomba nimalizie. Sikujua kama dakika 10 zinaisha haraka sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimalizie kwa kusema maneno machache kwamba kiujumla tumekubaliana na Serikali lakini kuna misingi ambayo taasisi lazima itazame. Taasisi nyingine zinatengeneza mambo mengi ili kufanya *revenue collection.* Mheshimiwa Waziri hapa anataka kila taasisi ijitegemee, lakini vilevile lazima taasisi iwezeshe, na *mandate* kuu ya *BRELA* ni kuwezesha biashara ndogo ndogo kukua na siyo kuhakikisha wanafanya *revenue collection. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kimsingi kabisa na mwisho kabisa, ni kwamba Waheshimiwa hapa waangalie *BRELA* na wawaelekeze kwamba sheria inaruhusu kampuni kuwa *general,* lakini misingi na mifumo ya *BRELA* inakataza, kwa njia ya kutengeneza kampuni nyingi na kupata *revenue* nyingi, lakini inaharibu ule mwelekeo na ile *Vision 2050* ambayo tunataka biashara zikue…

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. ABDULLAH ALI MWINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha na ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Nyamizi Simon Mhoja, atafuatiwa na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally na Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo ajiandae.

MHE. NYAMIZI S. MHOJA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Muswada huu ambao uko mbele yetu. Kwanza kabisa ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima na uhai na leo hii tuko pamoja tunachangia Muswada huu ambao tuliujadili kama Kamati muda mrefu uliopita, kwa hiyo ninashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ninaipongeza Kamati kwa sababu sheria zilikuja nyingi kama wenzangu waliotangulia walivyosema, lakini Kamati ilizingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana uongozi wa AG kwamba tulifanya naye kazi vizuri na anafikika kwa ushauri, pamoja na Wizara ya Katiba na Sheria. Kwa hiyo kazi ilikuwa ni rahisi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaenda moja kwa moja kwenye Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20. Haki ni haki hata kama ni jinai au madai, lakini haki ni haki. Sheria hii imerekebishwa ili kuwezesha makosa ya jinai yanayotendwa na watumishi wa sekta binafsi au sekta ya umma kwamba makosa yao yanayohusianishwa na ajira zao yaende sambamba. Kwa sababu awali ya yote mtumishi aidha wa Serikali au sekta binafsi, akikutwa na kosa aidha kule ofisini kwake, inamaanisha moja kwa moja, inaanza kutekelezwa mambo ya maadili, kwanza hatua za kimaadili ofisini zimalizike ndipo aende mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Sheria hii ya Marekebisho inataka kwamba, huyu mtumishi ana uwezo wa kufunguliwa makosa ya jinai yote kwa pamoja. Hii Sheria si tu Watanzania sisi wa

kwanza kutekeleza, hapana. Kuna nchi za Jumuiya za Madola na sisi kama wanachama na Kamati imefanya huo utafiti imegundua kwamba, mfano Nchi ya Uingereza na Nchi za Uganda, Kenya hata *South Africa*, hii Sheria wanatekeleza. Kwamba Sheria zote hazisubiri taratibu za kiutumishi, hazisubiri mambo ya kimaadili yafanyike ndiyo huyu mtumishi aweze kufunguliwa madai ya jinai. Kwa hiyo, tukiitekeleza hii Sheria, hatutakuwa wa kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaiunga mkono hii hoja na haya marekebisho na kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuweze kuipitisha hii Sheria ili iweze kuwa na manufaa kwa watumishi wa umma na sekta binafsi. Kwa sababu, kwanza itaokoa muda na haki ya mtumishi awe wa sekta binafsi au sekta ya umma, atapata haki yake kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho ninaweza kuongelea ni suala la Sheria ya Magereza, Sura ya 58. Ukweli usiopingika kwamba magereza inachukuliwa kama sehemu ya mateso, lakini haya marekebisho ya sheria, yanataka kwamba magereza iwe sehemu ya mafunzo, iwe sehemu ya kuwarekebisha wanaofungwa kule. Kwa hiyo, ninaomba Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono kwa sababu, moja kwa moja tutatengeneza jamii ambayo ina maadili mazuri na hasa sasa hivi ambapo tuna wimbi kubwa la uvunjifu wa maadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wale wafungwa watakapopata elimu ya mafunzo kule wakiwa gerezani, gereza liwe sehemu ya mafunzo. Wakipata elimu ya mafunzo ya *VETA*, ufundi stadi na chochote kile ambacho watakipata kule, watakaporudi kwenye jamii, inamaanisha watakuwa watu wema katika jamii, lakini kutumia ule ujuzi ambao wanaupata au wameupata kutoka magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati tulishauri kabisa kwamba, huyu mfungwa atakapopata elimu ya ujuzi, mfano VETA na akakidhi kabisa, basi huyu apewe cheti ili anaporudi kwenye jamii, iweze kumuuza na kupata kazi na kuachana na mambo ya upotovu wa

mambo ya kinidhamu mtaani. Atakuwa mtu mwema na itamsaidia yeye mwenyewe kujiendeleza kiuchumi na mambo yatakuwa mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na hilo…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. NYAMIZI S. MHOJA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, ninaomba niliombe Bunge lako Tukufu liweze kupitisha Muswada huu ambao una manufaa kwa jamii na imelenga kabisa katika Dira yetu ya 2050. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo na Mheshimiwa Asha Hussein Saleh ajiandae.

Mheshimiwa Aziza hayupo, Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia Muswada ambao uko mbele yetu. Nami kama Mwanakamati, niseme ninaunga mkono hoja ambayo iko mbele yetu. Ninaishukuru Serikali kwa kuleta hizi Sheria, japokuwa zilikuwa nyingi, lakini tulifanyia kazi kulingana na muda tuliokuwa nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda kwa kuanza, niishauri Serikali, Sheria nyingi tulizonazo, tuipe Mamlaka na nguvu ile Tume yetu ya Kurekebisha Sheria. Ninapendekeza hizi Sheria mara nyingi ziwe zinaanzia kule ili tupate maoni mwafaka kwa sababu hao wana ujuzi wa kurekebisha hizi Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Wanakamati ambao wamechangia hapo awali, lakini kwa upande wangu kwa sababu muda ni mfupi, nitajielekeza kwenye baadhi ya Sheria. Sheria

mojawapo nitakayoanza nayo, ni Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Usimamizi wa Maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii ni sheria nzuri na ukiangalia kwenye soko ambalo tunalo na ukisoma takwimu za ulimwengu, kati ya eneo ambalo tunapaswa kuliangalia kwa umakini ni hizi *pharmaceuticals*. Ninashukuru Serikali imelileta hili na kuweka masharti magumu kidogo kwa wale ambao wanafanya biashara ya maabara bila kuwa na vibali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia magonjwa tuliyonayo sasa hivi, mengi yanatokana na madawa, mengi yamepitwa na wakati, mengine yanauzwa kiholela. Hata hivyo, kwa Sheria hii, ninaipongeza Serikali kwamba wanaoanzisha maabara, wasianzishe kiholela, wawe na leseni na wale wanaofanya kwenye maabara, wawe ni walewale ambao wamesajiliwa badala ya mtu anapewa kibali cha kuanzisha maabara, halafu anamkaimisha mtu mwingine. Madhara yake ni makubwa sana kwenye jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana sasa hivi tunashuhudia magonjwa ya figo mengi, *cancer* zisizo na kifani na hesabu, ni kutokana na haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ninashukuru kwamba ile *threshold* ya adhabu ya mtu atakayepatikana na kosa la kuendesha maabara bila kusajiliwa, au bila kuwa na watumishi ambao wanakidhi viwango, imepandishwa kutoka shilingi 50,000 kwenda sasa shilingi 1,000,000 na isizidi shilingi 5,000,000 kwa wale ambao watakutwa na makosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya pili ambayo ninaishukuru Serikali, ninamshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali hili imelileta, tumelitafuta kwa muda mrefu sana. Sheria ya Usafiri wa Anga kuanzisha Kitengo cha kuchunguza ajali zinazotokana na usafiri wa anga. Ninashukuru tumechukua *Canadian model*, lakini pamoja na kuanzisha hiki kitengo, nishauri, hiki kisiwe kitengo, lakini tu kwa

kuanza tuendelee nacho hicho kama kitengo, lakini tunakoelekea, iwe *full-fledged* Mamlaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Canada, wanacho kitengo kama hiki na masharti waliyoyaleta pale ni kama ya Canada. Hata hivyo, kile ni kitengo kinachojitegemea, kina Mamlaka kamili, kina fedha na bajeti inayojitegemea. Taarifa zake, kama tulivyofanya Marekebisho ya Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80, kipengele cha 15(a), (b) na (c), ninaipongeza Serikali kwa kuja na hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, sasa tuangalie, kwa sababu tunaongelea *inter-modality* ya usafiri, ifanye *investigation* ya usafiri wa anga, lakini tutafakari sasa kuangalia sana usafiri wa reli, usafiri wa barabara kama Canada wanavyofanya kwamba ni *Investigation Bureau* au *Authority*, lakini ninaangalia *modes* zote za usafiri wa anga, reli, barabara na hivyo tunaweza tukapata taarifa sahihi ambazo zinaweza kutusaidia kuzuia ajali hizi za usafiri katika nchi yetu kwa siku za usoni, lakini niwapongeze kwa kuja na hiki kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Sheria ya Kuzuia Madawa ya Kulevya…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Naibu Spika, hii ninawashukuru. Tukiangalia jamii yetu, vijana wetu wameathirika. Niwaombe, kwenye kutekeleza hizi Sheria hasa zinazoathiri maisha ya vijana wetu na maisha yetu wenyewe, tuzipe kipaumbele katika kutekeleza. Tatizo letu siyo sheria, tatizo letu ni utekelezaji wa zile sheria. Kwa hiyo, niwaombe wale ambao wamekasimiwa mamlaka ya kutekeleza hizi sheria, tuzitekeleze kama zilivyo lakini na utu ndani yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa muda…

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa…

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: …muda ulikuwa ni mfupi na Sheria zilikuwa nyingi, lakini tunashukuru na ninaunga hoja mkono. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kikoyo. Mheshimiwa Asha Hussein Saleh, atafuatiwa na Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle na Mheshimiwa Nassriya ajiandae.

MHE. ASHA HUSSEIN SALEH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ya kujadili Miswada hii iliyokuwepo mbele yetu aliyotuletea hapa mtoa hoja. Muswada ya Sheria ya Maboresho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana mtoa hoja ambapo kama Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, tulikaa pamoja, tukajadili na hatimaye leo akaweza kutuletea hapa Miswada hii iliyokuwa mizuri kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajielekeza katika Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu, Sura ya 423. Kwa kweli sina mengi isipokuwa nitoe ushauri, kwa vile tulikaa tukajadili na mambo mazuri akatuletea hapa, basi nina ushauri mdogo katika Sheria hii, kwamba tuweke mifumo imara ili wataalamu wakiwa wanafanya uchunguzi, waweze kubaini miamala shuku kwa usiri mkubwa kulingana na matakwa ya sheria za nchi zilizowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Fuoni, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Asha. Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, atafuatiwa na Mheshimiwa Nassriya na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji) ajiandae.

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze tena kuchangia Muswada huu. Nitumie nafasi hii tena kuunga mkono hoja ambayo iko Mezani kwako na niwaombe Waheshimiwa Wabunge waupitishe Muswada huu, kwa

sababu kimantiki huu Muswada umelenga kuboresha utendaji wa taasisi na mamlaka mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitumie nafasi hii kuishukuru sana na kuipongeza Wizara ya Katiba na Sheria, lakini kipekee Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ukitazama maudhui ya Muswada huu, kwa kiasi kikubwa ni utekelezaji wa ahadi ya Serikali ndani ya Bunge, la kurekebisha sheria mbalimbali ili kuzipa taasisi na mamlaka za Serikali kutimiza wajibu wake vizuri. Hii ni wazi kwamba Serikali imeanza vizuri kuelekea Dira 2050. Kwa hatua hii, tunaishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kwa upekee nimshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye kwa muda mwingi amekuwa tayari kusikiliza pale ambapo Kamati inatoa maoni. Katika hili, tunamshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kazi nzuri ambayo anafanya kwa Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo moja ambalo ninapenda kuchangia mchana huu, ni eneo la wadau waliokuja kwenye Kamati ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria. Kwenye Taarifa yetu tumesema juu ya umuhimu wa wadau waliokuja kwenye Kamati na hapa ninaomba niwatambue kwa ufasaha wadau wote ambao walikuja kwenye Kamati kutoa maoni yao kwenye Kamati ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja walikuwa ni Chama cha Wanasheria Tanganyika *(TLS);* Pili, ilikuwa ni Kituo cha Sheria cha Haki za Binadamu; Tatu, ilikuwa ni Shirika Lisilo la Kiserikali *(TALA)*, Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania, Chama cha Wataalamu wa Maabara ya Tiba Tanzania, Chama cha Wataalamu wa Patholojia Tanzania. Taasisi hizi za wadau ambazo zilikuja mbele ya Kamati, zilikuwa na mchango mzuri sana kwenye Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wetu kama Kamati, kwa sababu Serikali na Mwanasheria Mkuu wa Serikali yuko hapa, wana mpango kabambe wa kuboresha Miswada na Sheria mbalimbali,

hawa wadau wanaokuja kwenye Kamati, wanapitia changamoto nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, wanakuja kwenye Bunge ambalo wanapaswa kufuata itifaki mbalimbali hapa ndani. Ushauri wetu kama Kamati kwa siku za baadaye na Bunge lako Tukufu ikikupendeza, huko mbele ya safari tuone uwezekano wa Kamati yako ya Bunge ya Sheria, Utawala na Katiba, iwe na uwezo wa kuwa na *public hearing* hata nje ya viwanja vya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Kamati ya Bunge inaweza kwenda kufanya *public hearing* Dar es Salaam au Mwanza na maeneo mengine ya kanda ili kuwapa nafasi wadau kufika mbele ya Kamati ili kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo ni muhimu kwa sababu wako wadau wengi wenye michango ya kutosha, ambao wangependa kuja kwenye Kamati, lakini kwa sababu ya gharama, na ugumu wa kuifuata Kamati hapa Bungeni, wanakosa nafasi ya kuja mbele ya Kamati yako.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo yangu machache kwa mchana huu, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Edwin Swalle, Makamu Mwenyekiti wa Kamati yetu. Mheshimiwa Nassriya Nassir Ali, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, mtoa hoja ajiandae.

(Hapa Mhe. Nassriya Nassir Ali, alichangia kupitia Mtaalamu wa Lugha ya Alama)

MHE. NASSRIYA NASSIR ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kwa mara nyingine. Pamoja na kwamba

tunatumia dakika tano, lakini mimi ni kiziwi, ninatumia mkalimani, wakati mwingine nitaomba kuongezewa angalau ziwe dakika 10 kwa sababu ninatumia lugha ya alama, mkalimani anatumia sauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaipongeza Wizara ya Katiba na Sheria na Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa ajili ya Muswada huu. Muswada huu ni mzuri na nimeona Muswada unalenga masuala ya biashara, utalii, Muswada ambao nimeona unafaa, nimepitia vipengele na mpaka nikahisi mwili unanisisimka. Nikajiuliza huu Muswada tunapeleka Bungeni, vipi kuhusu watu wenye ulemavu, sijaelewa hapo. Kama Muswada utapitishwa, utapitishwa kuhusiana na kulenga Dira ya Mwaka 2050, tutapitisha kweli Muswada huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninahitaji majibu kuhusu Muswada, kwa nini tunakwama Muswada wa watu wenye ulemavu ili uweze kuendana na Dira ya Mwaka 2050, ili uweze kutekelezwa. Mkataba wa Umoja wa Mataifa Tanzania hatukuweza kuuridhia, hivyo, ninaomba majibu kwa unyenyekevu mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, ninaomba majibu kwa unyenyekevu mkubwa sana tuurudie kuujadili Muswada huu, tukae pia na watu wenye ulemavu ili tuweze kuupitisha ndani ya Bunge lako Tukufu ili uweze kuendana na Dira ya Mwaka 2050. Mungu ibariki Tanzania, ahsante na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Nassriya Nassir Ali, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo atafuatiwa na Mtoa hoja.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa nafasi hii na ninaomba nichangie maeneo machache. Kwanza, nikushukuru kwa nafasi uliyonipa kwa sababu ninachangia hoja hapa Bungeni kwa mara ya kwanza tangu maamuzi makubwa yafanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kutumia nafasi hii kuongeza sauti kumpongeza sana Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi,

kwa kupendekezwa na hatimaye kuidhinishwa na Bunge hili Tukufu, kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Muswada ambao amewasilisha hapa; lakini muhimu sana kwa kazi kubwa anayofanya katika ku-*harmonize* sheria zetu ili ziendane na Dira ya 2050. Anafanya kazi nzuri na ametusaidia sana katika eneo hilo kuhakikisha kwamba sheria zetu zinakaa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, nimpongeze pia kwa uwasilishaji wa Muswada huu ambao kwa kweli ni sehemu nzuri ya utekelezaji wa dira. Ninataka kutumia nafasi hii kuchangia kwenye eneo moja tu ambalo Kamati imeliweka vizuri. Kamati imeshauri kwamba, Serikali itoe amri ama *order* kupitia Tangazo la Serikali litakaloainisha Mashirika ya Umma ambayo uteuzi wake utazingatia kigezo cha ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kutumia nafasi hii kueleza kwamba, tayari Serikali imeshabainisha katika Mashirika 300 na zaidi tuliyonayo, Serikali imebainisha Mashirika 96 ambayo yameomba na sisi kama Serikali tumeridhia yaende kufanya kazi, yawe huru kujitegemea. Kwa hivyo, yanakidhi vigezo ambavyo Serikali imeviweka, kwa maana kwamba vinaweza kujitegemea na vikajiendesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, vinaweza kuruhusiwa kwenda kwenye msingi wa kupata viongozi wake kwa njia ya ushindani na tunatumia vigezo vingi, lakini angalau 11. Moja, tunazingatia maslahi na malengo ya kimkakati katika nchi katika kuchangia kwenye uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaangalia uchangiaji wake katika mapato yale ambayo siyo ya kikodi, unyeti wake kwa maana ya *sensitivity*, uwezo wa kujiendesha kwa mapato yake ya ndani. Kwa

hivyo, kama Shirika linaweza kujiendesha kwa mapato yake ya ndani linaruhusiwa kuweza kuajiri watumishi wake na vigezo vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, utolewaji wa huduma ambazo hazina mtoa huduma mbadala. Kwa hiyo, yapo Mashirika ya Umma ambayo hakuna mwingine anayeweza kutoa hizo huduma zake. Kwa hivyo, lazima tuzingatie katika kuwapa hiyo nafasi; uwezo wa kujiendesha, uhitaji wa maamuzi ya haraka, uchangiaji katika pato la Taifa, mchango wa ajira katika nchi, utoaji wa huduma na mchango wa taasisi kwenye masuala ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiusalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hivi ni vigezo ambavyo Msajili wa Hazina amevibainisha na kwa kutumia vigezo hivi tumeweza kubainisha Mashirika 96 ambayo tunadhani haya yanaweza kwenda kujiendesha na hivyo, yanaruhusiwa kuingia moja kwa moja kwenye ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, tumeshaandaa na kama ambavyo Kamati imeshauri tutawasilisha katika mamlaka husika na kibali kikipatikana, basi Mashirika haya yanaweza yakaenda kwenye kasi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme wazi kwamba zipo taasisi na Mashirika ya Umma ambayo tayari kama ambavyo mnaona viongozi wake kuanzia bodi na wale menejimenti wanapatikana kwa njia ya ushindani na hiyo haipori mamlaka za uteuzi. Mamlaka ya Uteuzi kama ni Mheshimiwa Rais hii ni michakato tu, lakini hatimaye Mamlaka ya Uteuzi itafanya uteuzi husika na kama Mamlaka ya uteuzi ni Mheshimiwa Waziri husika, basi michakato inafanyika, lakini bado Waziri husika ataenda kufanya uteuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tayari niseme kwamba, suala hili linatekelezwa, linaendelea kutekelezwa na Muswada wa Sheria ambao utakuja ule wa *Public Investment Act,* utakuja tu kuainisha na kukamilisha. Tayari tunavyozungumza hapa Mashirika mengi tu viongozi wake kwa maana ya Bodi na Menejimenti

inafanyika kwa njia ya ushindani, lakini Mamlaka za Uteuzi zinabaki palepale *otherwise* ushauri huu ni mzuri na tunaupokea na Serikali inaenda kuutekeleza katika ngazi na njia mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, ahsante sana. Sasa nimwite Mtoa hoja, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Hamza Johari. *(Makofi)*

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ya kufanya majumuisho ya mjadala kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2026)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya Waheshimiwa Wabunge nane wamechangia Muswada huu na Wabunge wote nane wamechangia kwa kuzungumza ndani ya Bunge lako hili Tukufu na hakuna Mbunge ambaye amechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge ambao waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi, Mheshimiwa Nyamizi Mhoja, Mheshimiwa Oscar Ishengoma Kikoyo, Mheshimiwa Asha Saleh, Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Edwin Swalle, Mheshimiwa Nassriya Ali na Mheshimiwa Kitila Mkumbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utabaini kwamba, katika kazi hii tuliyoifanya na leo tunakamilisha Muswada huu, katika maeneo karibu yote kwa kiasi kikubwa tumekuwa na muafaka kati ya Serikali na Kamati ya Bunge. Niseme tu kwamba, sababu kubwa iliyofanya tuwe na muafaka ni kwa sababu ya ule uelewa tulionao kama Serikali, kwamba, katika nchi za kidemokrasia mamlaka yako kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo basi, mamlaka ya kutunga sheria ni ya wananchi na wanatekeleza mamlaka hayo kupitia Bunge. Kwa hiyo, ni vyema na ni *very good practice* sisi kama Serikali tunapokaa na Kamati ambapo ndiyo *thrust* kubwa ya *legislative process* ambao wanawakilisha Wabunge wote kwa niaba ya wananchi kusikiliza maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaangalia tulikuwa na Miswada 21, Miswada ambayo tulikuwa tumejiandaa vizuri, lakini baada ya kupata maoni ya Kamati na kupata uelewa maana hao ndiyo wananchi, ilibidi tuuache Muswada wa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197. Ilibidi tuuache baada ya kupata uelewa wa Sheria ya Kodi Ongezeko la Thamani, Sura ya 148, lakini tuiache Sheria ya Usimamizi wa Mahakama, Sura ya 237 hata kama tulitamani, lakini tuache pia Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa, Sura ya 441.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitupa maoni kwamba ikafanyiwe kazi vizuri na kwa kina halafu ije ikiwa imeboreshwa na sisi kwa moyo mkunjufu na kwa kuwa tunatambua dhana hiyo kwamba sheria zinatungwa na wananchi tulikubaliana na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilikuwa na maoni katika maeneo mengi ambayo yalihitaji kuboreshwa na ndiyo maana ukiliangalia jedwali la maboresho lina mambo mengi ambayo yalitokana na maoni ya Kamati. Tukifanya hivyo kwa kuhakikisha kwamba, tumechukua maoni yote ya Kamati vizuri tunakuwa tumetekeleza ile dhana ya kuhakikisha kwamba sheria zinatungwa na wananchi kwa niaba ya Bunge lao Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, niseme tu kwamba, kazi ya Bunge leo hii imekuwa rahisi kwa sababu Serikali na Kamati tulielewana na tumekuja na Muswada ambao una *consensus* na hiyo ndiyo dhana bora ya utungwaji wa sheria, *the best practice* kwenye *legislative process.*

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji wameendelea kusisitiza kwa kiasi kikubwa yale ambayo tumekubaliana kama maboresho ambayo tumeyachukua kwenye Muswada huu. Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi amejikita zaidi kwenye dira na kuhakikisha kwamba tunakuwa na sheria ambazo zitatufikisha kwenye lengo hilo lililowekwa kwenye dira na ninakubaliana naye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ile Dira ya 2050 tunazungumzia pato la Taifa kuwa Dola za Kimarekani 1,000,000,000,000 na nilikuwa ninaangalia hapa kwenye *exchange rate* ya leo kwa fedha za Kitanzania zitakuwa trilioni 2,600, lakini inataka kwamba lengo hilo kwa kiasi kikubwa uchangiaji wake utoke katika sekta binafsi, lengo hili ni kubwa *but it's achievable. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutalifikia tu lengo hili kama tutahakikisha kwamba ule mfumo mzima wa kisheria au *legal framework* au sheria zetu zinaoana na malengo hayo ya dira, zisipooana dira itakuwa inatuelekeza huku sheria zinavuta huku, hatutafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kusaidiana na Tume ya Kurekebisha Sheria tumedhamiria kwa dhati kuhakikisha kwamba, sheria zote kama alivyoelekeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba tuhakikishe sheria zote zinaoanishwa kuendana na dira. Kwa hiyo, niwahakikishie Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi na Mheshimiwa Oscar Ishengoma Kikoyo ambao wamezungumzia baadhi ya maeneo hayo yote, vilevile tutayaangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa labda kwa kifupi niwaambie; maana tumeanza kutekeleza dira, Julai, 2026, baadhi ya sheria ambazo kwa mwaka huu na mwaka unaofuata na unaofuata ile miaka ya awali ambazo zinaenda kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni mfumo, tunatumia neno mfumo kwa sababu mfumo unaweza kufanya kazi katika sheria

iliyopo au pengine inaweza kutakiwa kutungwa nyingine au inaweza kutakiwa kufutwa sheria fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni Mfumo wa Sheria za Nishati tutaziangalia vizuri na kuoanisha na dira. Pili, ni Mfumo wa Sheria za Viwanda, Biashara na Uwekezaji na mapitio ya Sheria ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Si tunataka 70% itoke sekta binafsi? Sasa hiyo ndiyo zile za awali ikiwemo Sheria ya Manunuzi ya Umma *(Public Procurement Act)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuangalia pia Mfumo wa Sheria za Kodi, kwa hiyo tukizungumza mfumo unaangalia mambo yote katika kodi na sheria zilizopo. Mfumo wa Sheria za Ardhi, Mfumo wa Sheria zinazohusu Wanawake, Watu Wenye Ulemavu, Wazee na Watoto. Mheshimiwa Nassriya Ali wala asiwe na wasiwasi tunaenda kuangalia mfumo mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa Sheria za Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi. Hivi *NEMC* hii tuliyonayo ndiyo ile tunayoitaka? Sheria zingine katika maeneo ya mazingira. Mfumo wa Sheria zinazohusiana na vijana, Mfumo wa Sheria za Maliasili na Utalii, Mfumo wa Sheria za Ajira, Mfumo wa Sheria za *National Cyber Security and Data Protection*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tunaenda kwenye *technology* na mambo ya *AI* hasa *cyber security* tunafanya nini ikiwemo *AI (Artificial Intelligence)* huko *thrust* itakuwa kubwa. Mfumo wa Sheria za Madini, Mfumo wa Sheria za Hifadhi ya Jamii, Biashara ya Kidigitali na Biashara ya Mtandao *(E-Commerce),* Mfumo wa Sheria za Utafiti, Sayansi na Teknolojia, Mfumo wa Sheria za Elimu, Afya na Maji na Mfumo wa Sheria za Mipango Miji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nitarudia Mfumo wa Sheria za Mipango Miji, Mfumo wa Sheria za Bima, Mfumo wa Sheria za Ushirika na Mfumo wa Sheria za Kilimo. Hizi sheria kwa hatua hizi za awali tunaanza kuzifanyia kazi, lakini ikiwemo Mfumo wa Sheria za Udhibiti amezungumza vizuri Mheshimiwa Oscar Ishengoma Kikoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Mifumo ya Sheria za Udhibiti, Mheshimiwa Oscar Kikoyo tutaangalia zile mamlaka za udhibiti zote ikiwemo hizo ambazo ziko kwenye hiyo sekta uliyozungumza ya uchukuzi. Kwa hiyo, hizi ni kwa uchache za kuanza nazo, dhamira yetu ni kubwa na kazi hii imeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo letu ni kuhakikisha kwamba, sheria hizi tunazioanisha na Dira ya 2050 na kwa vitendo siyo kwa maneno. Kwa hiyo, mara kwa mara kwa kutumia Bunge lako Tukufu, tutakuwa tunakuja na Miswada hii na hata wakati tunaleta Miswada hii ambayo, Muswada huu ambao tunaendelea nao na mwingine kesho. Kesho nitakuwa na Muswada mwingine, zoezi na *spirit* ni hiyo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana sana Kamati kwa kazi kubwa, weledi na maoni yao ambayo ndiyo yametuwezesha kufikia mafanikio haya katika Muswada huu husika. Kwa namna ya kipekee, ninavyohitimisha ninaomba kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Naibu Spika kwa namna ulivyoongoza vizuri kikao chetu cha leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna ambavyo analiongoza Bunge letu. Pia, niwashukuru Wenyeviti wote wa Kamati za Bunge kwa kazi nzuri wanazozifanya. Kwa namna ya kipekee nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro; Makamu wake, Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle; pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa ushirikiano waliouonesha kwa Serikali wakati wa kuchambua Muswada huu. Kazi yetu ilikuwa nyepesi, kazi yetu ilikuwa nzuri na ilikuwa *very interesting* kuifanya kwa sababu ya ushirikiano na *spirit* tuliyokuwa nayo. Tunawashukuru sana kwa michango yao mizuri na hatimaye tulipokea na kuweza kuboresha kupitia jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pia shukrani kwa Katibu wa Bunge kwa ushirikiano wake mzuri anaotupatia, pamoja na watendaji wote kutoka Mhimili huu wa Bunge. Ninatoa shukrani

zangu za dhati kwa Wizara ya Katiba na Sheria, nimshukuru Mheshimiwa Waziri, lakini ninawashukuru Waziri wa Fedha; Wizara ya Fedha; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Wizara ya Afya; Wizara ya Uchukuzi; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; Wizara ya Maliasili na Utalii; na wadau wengine wote kwa ushirikiano walioutoa kwa ofisi yangu katika mchakato mzima wa kushughulikia Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii pia kuwashukuru watumishi wote hasa Mwandishi Mkuu wa Sheria, Onorius John Njole, pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano mkubwa ambao wamenipatia wakati tunawasilisha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea maoni mazuri ambayo yanalenga kuboresha si Muswada tu, bali hata masharti mengine ya Sheria Mama. Kwa ujumla, maoni na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni ushahidi kwamba suala la marekebisho ya sheria kwa lengo la kuboresha utekelezaji madhubuti wa sheria zilizopo zinamhusu kila mmoja wetu katika Bunge hili na ni jambo endelevu. Ndiyo maana kila mwaka Serikali inakuja na Muswada wa aina hii, ili kuboresha masharti ya sheria zetu na kuzifanya ziende na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kusema kwamba, marekebisho ya sheria ndiyo chachu ya maendeleo, maendeleo ya kiuchumi. Niliwahi kum-*quote* Mohammed bin Rashid Al Maktoum, alipokuwa anaulizwa siri ya mafanikio na maendeleo ya Dubai ni nini? Jibu lake lilikuwa ni kwamba *law reforms* (mabadiliko ya sheria) ambayo waliyafanya. Sababu yake ya pili ilikuwa *the same, law reforms.* Sababu yake ya tatu, *law reforms. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi tutahakikisha kwamba wazo alilolisema Mheshimiwa Dkt. Ishengoma, la kuhakikisha kwamba Tume yetu ya Kurekebisha Sheria *(Law Reform Commission)* inaimarishwa ili iweze kufanya kazi zake vizuri, hiyo ni ajenda yetu na tutahakikisha kwamba tunaifanyia kazi. Tuwe na *strong law reform*

ambayo ina *lawyers,* ina wachumi, ambao wanaweza kufanya kazi za kitafiti vizuri na kuhakikisha kwamba, tunaoanisha sheria zetu na Dira ya Maendeleo ya 2050.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI: Kamati ya Bunge Zima.

NAIBU SPIKA: Kamati ya Bunge Zima.

KAMATI YA BUNGE ZIMA

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae.

Katibu.

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2026)*

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3
Kifungu cha 4

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 5

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Kifungu cha 6
Kifungu cha 7

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 8
Kifungu cha 9
Kifungu cha 10

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Kifungu cha 11
Kifungu cha 12

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilifutwa na Kamati ya Bunge Zima)

Kifungu cha 13

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 14

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 18

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Kifungu cha 19
Kifungu cha 20

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 21

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Kifungu cha 22

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 23

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)

Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27
Kifungu cha 28

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya Mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 29

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilifutwa na Kamati ya Bunge Zima)

Kifungu cha 30

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 31

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilifutwa na Kamati ya Bunge Zima)

Kifungu cha 32
Kifungu cha 33
Kifungu cha 34

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 35
Kifungu cha 36

(Vifungu vilivyotajwa hapo vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Kifungu cha 37
Kifungu cha 38

Kifungu cha 39

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 40

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Kifungu cha 41
Kifungu cha 42
Kifungu cha 43
Kifungu cha 44
Kifungu cha 45
Kifungu cha 46
Kifungu cha 47
Kifungu cha 48
Kifungu cha 49
Kifungu cha 50
Kifungu cha 51
Kifungu cha 52
Kifungu cha 53
Kifungu cha 54
Kifungu cha 55
Kifungu cha 56
Kifungu cha 57
Kifungu cha 58
Kifungu cha 59
Kifungu cha 60
Kifungu cha 61
Kifungu cha 62
Kifungu cha 63
Kifungu cha 64

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 65
Kifungu cha 66
Kifungu cha 67
Kifungu cha 68
Kifungu cha 69
Kifungu cha 70
Kifungu cha 71
Kifungu cha 72
Kifungu cha 73
Kifungu cha 74
Kifungu cha 75
Kifungu cha 76
Kifungu cha 77
Kifungu cha 78
Kifungu cha 79
Kifungu cha 80

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilifutwa na Kamati ya Bunge Zima)

Kifungu cha 81
Kifungu cha 82
Kifungu cha 83
Kifungu cha 84
Kifungu cha 85
Kifungu cha 86
Kifungu cha 87
Kifungu cha 88
Kifungu cha 89
Kifungu cha 90
Kifungu cha 91
Kifungu cha 92
Kifungu cha 93
Kifungu cha 94
Kifungu cha 95

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 96

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Kifungu cha 97

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 98

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Kifungu cha 99
Kifungu cha 100
Kifungu cha 101
Kifungu cha 102
Kifungu cha 103
Kifungu cha 104
Kifungu cha 105
Kifungu cha 106
Kifungu cha 107
Kifungu cha 108
Kifungu cha 109
Kifungu cha 110
Kifungu cha 111
Kifungu cha 112
Kifungu cha 113
Kifungu cha 114
Kifungu cha 115
Kifungu cha 116
Kifungu cha 117
Kifungu cha 118
Kifungu cha 119
Kifungu cha 120

Kifungu cha 121
Kifungu cha 122
Kifungu cha 123
Kifungu cha 124
Kifungu cha 125
Kifungu cha 126
Kifungu cha 127

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 128

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Kifungu cha 129
Kifungu cha 130
Kifungu cha 131
Kifungu cha 132
Kifungu cha 133
Kifungu cha 134
Kifungu cha 135
Kifungu cha 136

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 137

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Kifungu cha 138
Kifungu cha 139
Kifungu cha 140
Kifungu cha 141

Kifungu cha 142
Kifungu cha 143
Kifungu cha 144
Kifungu cha 145
Kifungu cha 146
Kifungu cha 147
Kifungu cha 148
Kifungu cha 149
Kifungu cha 150
Kifungu cha 151
Kifungu cha 152

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 153

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Kifungu cha 154
Kifungu cha 155
Kifungu cha 156
Kifungu cha 157
Kifungu cha 158

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 159

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Kifungu cha 160
Kifungu cha 161

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilifutwa na Kamati ya Bunge Zima)

Marekebisho ya Mpangilio mpya wa namba kutoka kifungu cha 13 – 159 kuwa Kifungu cha 11 – 149

(Mpangilio uliotajwa hapo juu ulipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Hapa Bunge Lilirejea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae.

Mtoa Hoja, Taarifa.

T A A R I F A

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 105 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2026, ninapenda kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka *2026 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2026),* ibara kwa ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2026],* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa kanuni zetu, ninaomba niwahoji kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2026)*.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2026 Ulipitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Katibu.

NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali zipatazo ishirini na moja kwa lengo la kuondoa Mapungufu ambayo yamejitokeza wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika sheria hizo *(A Bill for an Act to amend certain Written Laws in order to keep the Laws updated with some challenges observed in its implementation)*

(Kusomwa Mara ya Tatu)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua hii Bunge limekamilisha kazi yake ya kupitisha Muswada huu wa Sheria kama ambavyo umewasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hatua iliyobaki ni

hatua ya kwenda kwa Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kuidhinisha na kuwa sheria kamili.

Nichukue nafasi hii kumpongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Serikali kwa ujumla kwa Muswada wenye manufaa makubwa kwa Taifa na hasa tunapoelekea Dira ya 2050. Pia, niipongeze Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri mliyofanya kwa kupitisha Muswada huu wa Sheria. Ninawapongeza sana pia Wabunge wote mliopata nafasi ya kuchangia katika mjadala, kwa kazi ambayo tumeikamilisha muda huu. Ninawapongeza wote, niwatakie kila la kheri katika utekelezaji wa kazi hii njema.

Baada ya kusema haya, ninatangaza rasmi kwamba tumefika mwisho wa Shughuli za Bunge kwa leo, ninaahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

(Saa 7.56 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 2 Septemba, 2026, Saa Tatu Asubuhi)